# Matendo ya Mungu Wetu Mpole

## Utukufu wa Pambazuko la Siku Mpya Juu ya Sifa za Mungu

Jay A. Schulberg



# Matendo ya

# Mungu Wetu Mpole

## Utukufu wa Pambazuko la Siku Mpya

## Juu ya Sifa za Mungu

Hali ya Mungu asiyekuwa na fujo:

Somo la kutoa Changamoto kwa Imani Potovu

Kumhusu Mungu na kutoa Mtazamo

Mbadala wa Kutia Moyo

Jay A. Schulberg

Hati miliki © 2017 Jay A. Schulberg

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki ambayo inaweza tumiwa au kutolewa upya kwa njia yoyote ile, picha, vifaa vya kielectroniki, au mitambo, ikiwemo kuchapisha nakala, kurekodi, kuweka kwenye kanda au mfumo wowote wa kuhifadhi na kurejesha ujumbe bila idhini iliyoandikwa kutoka kwa mwandishi isipokuwa kununukuu kwa kifupi ilivyo katika Makala na mapitio muhimu.

Nukuu za maandiko zimetolewa kwenye toleo la Bibilia la Mfalme Yakobo.

Kimechapishwa
na

Fatheroflove.info

# Yaliyomo

Umewahi Staajabu?....................................................................6
Inajalisha Kweli? .......................................................................8
Mfumo Wetu Mkamilifu ..........................................................10
Chemchemi Yetu ya Uzima .....................................................12
Aliumbwa kwa Mfano Wake .....................................................14
Bwana Mdanganyifu ................................................................16
Dhambi Ni Nini? .......................................................................18
Mbona Kuna Shetani? ..............................................................21
Joka wa Uharibifu .....................................................................29
Uteka wa Ayubu ........................................................................32
Mbona Tunasoma Bibilia Visivyo ............................................39
Mbona hatumuelewi Mungu.....................................................41
Jinsi Mungu Huangamiza .........................................................46
Hasira ya Mungu ni Nini?.........................................................48
Jinsi Mungu Hufanya Vita .......................................................61
Sodoma and Gomora................................................................64
Vipi Kuhusu Gharika?...............................................................67
Ushuhuda wa Msalaba .............................................................73
Mungu Sio Mtawala Jeuri .........................................................75
Muumbaji na Mpaji Wetu .......................................................84
Tunawezaje Kuwa na Uzima wa Milele?..................................90
Lazima Tuogope Hukumu?.......................................................97
Hukumu Ya Mungu Inaonekana Jinsi Gani? ..........................107
Mungu Ni Mnyenyekevu .........................................................112

Mungu Ni Mtumishi, Sio Bwana wa Mtumwa .................................... 115
Upendo wa Mungu Hauna Mipaka .................................................... 118
Ufalme wa Mungu ........................................................................... 120
Mungu Hutupa Uhuru wa Kweli ........................................................ 125
Vidokezo ......................................................................................... 129

Utangulizi

# Umewahi Staajabu?

Kwa lugha iliyokubalika kisheria, Majanga ambayo ni kwa sababu ya nguvu za maumbile na hayangeweza kingwa kwa vyovyote vile yanarejelewa kama *matendo ya Mungu*. Kirai hiki mara nyingi kinaongezwa katika sera za bima. Tulitoa wapi wazo kuwa Mungu anawajibu kwa mabaya yanayotendeka katika ulimwengu wetu? Je, anaamua kiholela wakati na mahali pa matukio kama vile kimbunga, tetemeko la ardhi, tufani, mafuriko, na majanga mengine ya maumbile ambayo hutendeka? Je, Mungu hufanya jambo kusababisha mambo haya yatendeke? Je, huchochea ulimwengu asili ili kufanya mapenzi yake yatimie? Na mbona anafanya mengi ili kuzuia maafa mengi katika ulimwengu wetu? Hatimaye, Mungu alikuwa na jukumu lipi katika ukatili tunaousoma katika Bibilia? Je, aliafikia ukatili yeye mwenyewe?

Bibilia hutoa majibu kwa maswali haya, lakini tunapaswa kutafuta kwa ndani zaidi ili kuyapata. Na pia tunahitajika kuwa tayari kusikia kile ambacho Mungu anasema kujihusu na jinsi anavyotenda kazi hata kama inatia changamoto kwa imani tuliyonayo kumhusu.

Kitabu hiki kitachunguza tabia ya Mungu kama inavyodhihirishwa na Bibilia—matendo yake ni nini na, kama muhimu tu, wala sio nini. Wengi wanaamini kuwa Mungu hutupenda tunapofuata sheria zake lakini anakasirishwa na makosa yetu na huwaadhibu wale ambao wanaenda kinyume na amri zake. Lengo la somo hili ni kuonyesha, kutoka kwenye Bibilia kuwa Mungu *hajawahi* tenda kama mwangamizi ila tu kama Muumbaji, Mpaji, na Mkombozi.

*Lakini hekima itokayo mbinguni kwanza ni safi, kisha inapenda amani, ya upole, iliyo tayari kusikiliza maneno ya watu wengine, yenye unyenyekevu, iliyojaa huruma na matunda mema, isiyopendelea mtu, tena ya kweli..*

*—Yakobo 3:17*

# 1

# Inajalisha Kweli?

Mbona ni muhimu kufahamu jinsi Mungu alivyo? Je, inajalisha vile tunafikiria jinsi Mungu alivyo? Na je, inajalisha hata tukifikiria kumhusu kwa yote? Majibu kwa maswali haya yanapatikana katika msingi wa *kila kitu* muhimu kufahamu. kile ambacho tunaamini kumhusu Mungu na tabia yake huamua tabia yetu wenyewe—na tabia yetu ni muhimu zaidi kuliko utajiri wote wa mali ambao ulimwengu unatupa.

Yesu akamwambia, “Mimi na Baba Yangu tu Umoja.” (Yohana 10:30). Mungu Baba na Mwana wa Mungu ni *wamoja* katika lengo—*umoja* katika tabia. Uhusiano wao ni umoja wa uwiano mkamilifu. Mwandishi wa Waebrania anasema kuwa Yesu ni kwa Mungu Baba “Mwana ni mng’ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake” (Ebr. 1:3). Utukufu wa Baba ni zaidi ya mapambo yake; ni tabia yake, Mungu alipita mbele ya Musa na kutangaza tabia yake:

> Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi. (Kut. 34:6–7)

Kumjua Mungu kama *kweli* alivyo hutupatanisha naye. Maarifa haya ni ya kuponya na ya kutoa uzima. Sikia alichokisema Yesu katika ombi lake kwa Baba yake: “Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma.” (Yohana 17:3). Yesu alionyesha kwa maneno yake na uzima hasa jinsi Mungu Baba

alivyo. Alisema, “Amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo lo lote peke yake, Yeye aweza tu kufanya lile analomwona Baba yake akifanya, kwa maana lo lote afanyalo Baba, Mwana pia hufanya hivyo hivyo” (Yohan 5:19).

Tunapojua kuwa Mungu *daima* anatupenda na ni mwenye rehema, tutavutwa kwake na upendo na uaminifu. Tunahakikisho la upendo wa Mungu na mapenzi yake mema kwetu kila wakati, kwa sababu njia zake *kamwe* hazibadiliki. Mungu anasema katika Malaki 3:6, “Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu.” Hageuki kamwe kama tulivyo. Tunaweza kuwa wakarimu, wenye upendo, na wenye kuwaza mradi tu tunafanyiwa haki na kuheshimiwa, lakini tunapokumbana na wale wanaotudhuru, ni mwelekeo wetu kukasirika na kutaka kulipiza kisasi. Mungu *kamwe* hajibu kwa hasira au kwa kulipiza kisasi.

Maneno ya Mungu yanathibitisha kuwa Yesu habadiliki wala Baba hubadilika: “Yesu Kristo ni Yeye yule jana, leo na hata milele” (Ebr. 13:8). “Kila kitolewacho kilicho chema na kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kutoka kwa Baba wa mianga, ambaye Kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka” (Yakobo 1:17). Maneno haya Pia yanatuhakikishia kuwa Mungu wetu mpole hana upande katili.

*Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi takauona utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli.*

*—Yohana 1:14*

# 2

# Mfumo Wetu Mkamilifu

Katika moyo wa Mahubiri ya Mlimani, Yesu anatupa mfumo mkamilifu wa jinsi ya kuishi katika ulimwengu katili.

> Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Mpende jirani yako na umchukie adui yako.' Lakini mimi ninawaambia: Wapendeni adui zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi, ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa maana Yeye huwaangazia jua lake watu waovu na watu wema, naye huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. Kama mkiwapenda wale wanaowapenda tu, mtapata thawabu gani? Je, hata watoza ushuru hawafanyi hivyo? Nanyi kama mkiwasalimu ndugu zenu tu, je, mnafanya nini zaidi ya wengine? Je, hata watu wasiomjua Mungu, hawafanyi hivyo? Kwa hiyo iweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.'' (Matt. 5:43–48)

Kifungu hiki kinatufunza nini kumhusu Mungu? Yesu anasema, "Mpende jirani yako," na anafuatisha na, "Ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni." Na anahitimisha na, "Kwa hiyo iweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu." Yesu anatuagiza kuwahudumia adui zetu kama vile Baba yetu wa Mbinguni anavyowahudumia adui zake. Anataka tuelewa kuwa kanuni za juu anazoweka mbele yetu katika Mahubiri ya Mlimani zinaweza fikia *tu* kama tukiziona zikianzishwa kutoka kwa Mungu mwenyewe.

Katika maisha ya Yesu, tunapata mfumo wetu mkamilifu wa jinsi ya kuwahudumia adui zetu. Hakuna hata wakati mmoja alilipiza kisasi dhidi ya wale waliomkosea yeye. Kuanzia kwa

kusalitiwa kwake, na kukamatwa kwake hadi kusulubishwa, alipoomba watesi wake wasamehewe— “Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo!” Wakagawana nguo Zake kwa kupiga kura. ” (Luka 23:34)—alidhihirisha upendo tu.
Wakati Yesu hakukaribishwa katika Kijiji cha Samaria, wanafunzi wake Yakobo na Yohana walifikiria kuwa kijiji hicho kilifaa kuangamizwa kwa moto: “Wanafunzi Wake, yaani, Yakobo na Yohana walipoona hayo, wakasema: “Bwana, unataka tuagize moto ushuke kutoka mbinguni ili uwaangamize; (kama Eliya naye alivyofanya)?” Yesu akageukia, akawakanya.(Akasema, Hamjui ni roho ya namna gani mliyo nayo.) kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa. Wakaondoka wakaenda mpaka kijiji kingine.” (Luka 9:54–56).

Njia bora ya kufahamu jinsi Mungu alivyo ni kwa kujifunza maisha ya Yesu. Hakumuua yeyote wala kutishia kufanya hivyo. Yesu hakumuumiza yeyote. Hakumhukumu yeyote. Wakati Filipo, kwa niaba ya wanafunzi, alimuuliza Yesu awaonyeshe Baba, alijibu:

> “Filipo, nimekaa nanyi muda huu wote hata usinijue? Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba. Sasa wawezaje kusema, ‘Tuonyeshe Baba?’ Je, huamini ya kuwa Mimi niko ndani ya Baba, naye Baba yuko ndani Yangu? Maneno ninayowaambia siyasemi kwa ajili Yangu mwenyewe, bali Baba akaaye ndani Yangu ndiye atendaye hizi kazi. (Yohana 14:9–10)

Tunapoingia kwenye funzo ambalo litaleta changamoto kwa hali ya theolojia, wacha tuamue kuhifadhi maneno ya Yesu na mfano wake mkamilifu katika mstari wa mbele wa mawazo yetu.

# 3

## Chemchemi Yetu ya Uzima

Na kazi kiasi ya awali ya msingi ikianzisha ukweli kuwa Mungu daima ni mwenye upendo, tutachunguza matendo ya Mungu katika Bibilia ambayo yanaonekana kinyume cha kanuni ambazo zilifundishwa na Yesu. Katika kitabu cha Isaya, tunapata umaizi mkubwa kuhusu njia na mawazo ya Mungu:

> Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. (Isa. 55:8–9)

Njia na mawazo ya Mungu yako juu sana katika kusudi na tabia. Ufafanuzi huu wa kweli kumhusu Mungu ni mgumu kwetu kuushika. Katika uamuzi wetu wa kujihalalisha, tunafikiria kuwa Mungu ni kama sisi. Tunakasirika, hivyo tunafikiria kuwa Mungu lazima akasirike kama sisi tufanyavyo. Tunapelekwa kulipiza kisasi tunapokosewa, hivyo tunafikiria kuwa Mungu lazima awe na hali sawa ya kulipiza kisasi anapokosewa. Mungu anatwambia vinginevyo:

> Ndivyo ulivyofanya, nami nikanyamaza; Ukadhani ya kuwa Mimi ni kama wewe. Walakini nitakukemea; Nitayapanga hayo mbele ya macho yako. (Zaburi. 50:21)

Mungu alipoumba ulimwengu wetu, hakuazimia utende kazi kivyake. Kwa Mungu kutohusishwa na ulimwengu wetu haitakuwa kinyume tu na kusudi lake, itamaanisha kuwa

maisha hayawezi endelea katika sayari yetu—"Kwa kuwa katika Yeye tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima wetu" (Matendo 17:28). Mungu ni mpaji wa kila pumzi ambayo tunatumia.

Mungu ndiye chemchemi na mdumishaji wa uzima. Hata hivyo, kuna kitu kimoja ambacho kinaweza tutenganisha naye—dhambi. Lakini dhambi ni nini? Mara nyingi tunafikiria dhambi kuwa kama mambo mabaya tuyatendao au kuvunja Amri za Mungu. Wazo ni kuwa wakati mwingine dhambi inaweza pimwa, na baadhi yetu wakiwa na kiwango cha juu au hata kidogo kabisa. Katika Bibilia, tunajifunza kuwa mambo mabaya tuyatendao ni dalili za maradhi yaliyoingia ndani ambayo wote tumerithi kutoka kwa wazazi wetu wa kwanza. Maradhi haya ni kuamini uongo kuwa Mungu anatafuta mapenzi yake tu. Uongo huu wa Shetani uliusiwa kwa jamii ya mwanadamu katika Bustani ya Edeni, na umeumbuka sura yetu ya Mungu tangia wakati huo.

Mungu alipoumba Adamu na Hawa na kuwaweka katika bustani, walipewa agizo moja—na moja tu:

> Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika. (Mwanzo. 2:16–17)

Ni rahisi kuelewa mbona Mungu aliuweka "mti wa uzima" (Mwanzo. 2:9) katika bustani, lakini ni vigumu kwetu kuthamini *mbona* aliweka "ujuzi wa mema na mabaya" katika mazingira haya kamilifu. Katika wazo la kwanza, tunaweza ona uwepo wa mti huo, na onyo dhidi ya kula kutoka kwake, kama makaribisho ya maafa.

# Aliumbwa kwa Mfano Wake

Katika Mwanzo tunapata urithi: “Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu: … Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.” (Mwanzo. 1:26–27). Inamaanisha nini kuumbwa kwa mfano wa Mungu, na mfano wa Mungu *ni* nini? Tutagundua mfano wa Mungu ni nini tutakapopata ufafanuzi unaoelezea Mungu ni nani? Ufafanuzi hasa unapatikana katika 1 Yohana 4:8: “Mungu ni upendo.” Kumbuka kwamba fungu halisemi tu “Mungu ni mwenye kupenda,” kama upendo ni moja wapo wa tabia zake nyingi, bali linasema tu, “Mungu ni upendo.” Kingine chochote ambacho tunaweza fahamu kumhusu Mungu lazima kiwe na ulinganifu na ufafanuzi huu. Hivyo basi, kama Mungu alivyomkamilifu, tunaweza hitimisha kimantiki kuwa upendo wa Mungu uwe mkamilifu pia, bila kuegemea hisia za kibinafsi. Zaidi ya hayo, upendo wake lazima uwe *haubadiliki* kama vile yeye *habadiliki*.

Kama tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, basi lazima tumeumbwa na Mungu *kushuhudia* upendo. Sasa upendo, kuwa upendo, hauwezi amurishwa au kwa njia yoyote ile kulazimishwa. Unaweza tu kutolewa bure kama uchaguzi. Hili linawezafahamika virahisi kama tutafikiria mtu ambaye alikosa upendo akiabiri basi akiwa na bunduki lililojaa risasi akidai upendo kutoka kwa abiria kwa kuwatishia kufa. Je, mtindo huu utazalisha upendo?

Tuseme tungejaribu mtindo mwingine usio wa kutisha sana wa kupata upendo kwa kuunda roboti iliyowekwa iseme “Nakupenda” tunapokutana nayo. Je, hili litapelekea uwepo wa upendo wa kuridhisha na wenye maana kwa msingi wa mahusiano? Je, mtindo huu, ambao unaweza kosa kupata upendo kwetu, unaweza tenda kwa Mungu?

Wacha turejee kwenye bustani ya Edeni na mti huo wa kutatanisha uliokatazwa. Kama Mungu hangeumba mti huo, ingewezekana jamii ya mwanadamu kupenda kama Mungu apendavyo? Kwa upendo, kuwa upendo, unahitaji kutolewa kwa kujitolea, tunaweza pia kuwa na uhuru wa kutopenda. Upendo daima ni chaguo; upendo hauwezi kuamurishwa au kushurutishwa.

Kama Mungu angeumba wazazi wetu wa kwanza na kuwaweka katika bustani bila kuwapa njia inayoonekana ambapo wangechagua *kutompenda* na kumwamini yeye, haingewezekana kwao kupenda kama jinsi Mungu mwenyewe hupenda. Kama tu Mungu ni chemchemi ya uzima wetu, pia yeye ni chemchemi ya upendo halisi—uzima na upendo haviwezi tenganishwa. Kuumbwa kwa mfano wa Mungu kuna mpa kila mmoja wetu uwezo wa kuwa rafiki mwenye upendo kwa Muumbaji wetu.

Mungu hakuweka mti wa ujuzi wa mema na mabaya na vikwazo vya kuwakataza kula matawi yake kama jaribu la kiholela la utiifu wetu kwake, bali kama hakikisho kuwa anathamini uhuru wetu wa uchaguzi sana kiasi ya kwamba alikuwa tayari kuhatarisha kuwa tungechagua kile ambacho tungechagua na kutanga mbali naye. Tukifahamu mbona Mungu aliweka mti uliokatazwa katika bustani, hatutamshtaki kuwa dikteta anayejihudumia. Kulikuwa na mmoja, hata hivyo, aliyekuwa tayari kumshtaki Mungu kwa kila kitu.

# 5

## Bwana Mdanganyifu

> Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. *Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.*
>
> —Mwanzo 3:1–5, (mkazo umetiliwa)

Mwanzo, wacha tutambue utambulisho wa nyoka huyu anenae. Joka ni nani? “Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani, aupotoshaye ulimwengu wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake.” (Ufu. 12:9). Hawa hakuwa akizungumza na nyoka mwerevu tu, bali na Shetani—bwana wa udanganyifu mwenyewe.

Nyoka kwa uchongeza wa hila alimshtaki Mungu kuwa aliwadanganya Adamu na Hawa na kuzuia kitu kizuri kwao. Zaidi ya hayo, kama wangekula tunda tu, macho yao yangefunguka, na wangekuwa kama “miungu, wakijua mema na mabaya.” Ni nani mwanamke alichagua kuamini, Mungu au Shetani?

> Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala. Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo. Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone. Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi? (Mwanzo. 3:6–9)

Adamu na Hawa walipokula tunda la mti waliokatazwa, macho yao yalifunguka (walijitambua), na walitaka kujificha kutoka kwa Mungu. Jibu la Mungu lilikuwa lipi? Alikuja akiwatafuta. Maneno yake ya kwanza yalikuwa, "mko wapi?" alitafuta maridhiano na wanawe ambao sasa wamejitenga naye.

> *Kwa maana Mwana wa Adamu amekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."*
>
> *—Yesu (Luka 19:10)*

# 6

# Dhambi Ni Nini?

Sasa, tukirejelea swali: dhambi ni nini? Kupata ufafanuzi sahihi, ni muhimu kwanza tutambue hasa kilichoenda murama kwa, "mti wa ujuzi wa mema na mabaya." Katika Mwanzo 3:6, mwanamke aliona sifa tatu za kutamanika za mti huo:

1. "Mti ulifaa kwa chakula." Kwa sura ya nje hili linaweza onekana kuwa kweli, isingekuwa ni kwa ukweli kwamba mti ulikuwa umekatazwa kama chanzo cha chakula. Tatizo halikuwa kwa tunda lenyewe lakini mwanamke sasa alikuwa akilitazama kama *lafaa*.

2. Mti ulikuwa "wapendeza kwa macho." Kila kitu ambacho Mungu aliumba katika bustani kilikuwa kikamilifu, hivyo basi kwa kweli mti ungekuwa "wapendeza kwa macho." Mwanamke aliona sifa moja zaidi ya mti.

3. "Mti wa kutamanika kwa maarifa." Kweli? Je, mti huu ulikuwa na sifa ya ajabu? Nyoka alikuwa sawa? Je, kuwa na ujuzi wa mema na mabaya *kweli* kungetamanika? Na kuwa na ujuzi wa mema na mabaya kuna maana gani? Je, nikupokea ujumbe tu?

Fungu linahitimisha kwa "basi alitwaa matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala." Hili mara nyingi linafahamika kuwa dhambi ya kwanza ya mwanadamu, lakini dhambi ni *gani*? Nini kilikuja mwanzo—kula tunda au kuamini uongo wa Shetani kumhusu Mungu?

Tatizo la msingi lilikuwa wakati ambapo Hawa aliamini uongo wa nyoka kuwa Mungu alikuwa mbinafsi akizuia kitu kizuri kwao. Dhambi sio tendo lenyewe tu, kama dhambi ni ya

kuwekewa kiwango. Dhambi, ni msingi, ni hali ya ugonjwa wa akili ambao humuona Mungu kama ambaye ana ubinafsi na hivyo kukosa kumwamini.

Dhambi inaweza fananishwa na ugonjwa. Katika ugonjwa kuna kisababishi cha msingi kama vile ugonjwa unaosababishwa na vijidudu, magonjwa ya metaboli, au mfumo wa kinga kukosa kufanya kazi. Visababishi hivi vya msingi hupelekea uwepo wa dalili moja au zaidi: homa, kichefuchefu, maumivu, kizunguzungu, uchovu, na mengine mengi. Kwa dhambi, kisababishi cha msingi ni kuamini uongo kumhusu Mungu na, kwa sababu hiyo, kujikengeusha kutoka kwake ambaye upendo wake ni kwa wengine. *Dhambi* yetu ya nje (dalili) ni matokeo ya kuamini kuwa Mungu ni mbinafsi (kisababishi cha ugonjwa). Yesu, katika mazungumzo yake na walimu wa sheria na mafarisayo, alitumia mfano huu wa dhambi kuwa ugonjwa ambao unahitaji uponyaji:

> Baadhi ya walimu wa sheria na Mafarisayo walipomwona akila pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, wakawauliza wanafunzi Wake, ‘‘Mbona Yesu anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?” Yesu aliposikia haya akawaambia, “Walio wazima hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa. Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.” (Marko 2:16–17, mkazo umetiliwa)

Dhambi ni ya kufisha kwa sababu hututenganisha na Mungu, chemchemi ya uzima wote. Katika utengano huu ambao hutendeka, kamwe sio Mungu ambaye hujitenga kutoka kwetu —daima ni sisi ambao hujitenga kutoka kwake. Adamu na Hawa walijawa na hofu kwa Mungu kuliko Shetani—ambaye wangemhofu. Baada ya kula tunda, Bibilia inasema, “Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu

asiwaone." (Mwanz. 3:8). Tumekuwa tukijificha kutoka kwa Mungu wetu mpole tangu siku hiyo.

Tutafanya vyema kugundua kwamba Mungu alipowaonya Adamu na Hawa wasile tunda la mti waliokatazwa, hakusema, "siku hiyo mtakayokula tunda la mti huo, nitawaua." Alisema, "Siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika." Mwanaume na mkewe walipokula kutoka kwa mti huo, mchakato wa kufa ulianza ndani yao siku hiyo hiyo waliyojitenga kutoka kwa chemchemi yao ya uzima. Ni dhambi (kuamini uongo kuwa Mungu ni mbinafsi na sio wa kuaminiwa) hilo ni la kufisha, sio Mungu: "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti" (Rom. 6:23). Mungu hayuko kwenye biashara ya dhambi, na halipi mshahara wa dhambi.

Pia inaonekana kuwa Adamu na Hawa walipokula tunda la mti waliokatazwa, walipokea mengi zaidi ya maarifa ya akilini ya mema na mabaya. Pasipo kujua walijikabidhi pamoja na vizazi vyao katika *kushuhudia* maarifa ya mema na mabaya. Hawangejua *kuhusu* mabaya tu; watawaza kuyahusu, watakuwa watumwa kwayo, na kwa sababu hiyo watajua uchungu, mateso, hofu, na kifo.

Mwanadamu hakuwa peke yake katika mateso ya matokeo ya kuepukika dhambi ilipoingia ulimwenguni mwetu. Maumbile yote yaliathirika na ukosefu wa uiano kati ya maumbile na muumbaji ambao ulianzishwa na dhambi ya Adamu na Hawa: "Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote vimekuwa vikilia kwa uchungu kama utungu wa wakati wa mwanamke kuzaa hata sasa." (Rom. 8:22). Ulimwengu ukawa mahali hatari kwa mwanadamu na wanyama. Tangia mafuriko ya siku ya Nuhu, dunia ikawa wazi kwa hali ya hewa ya vurugu, matetemeko ya ardhi, volkano, na majanga mengine ya nguvu za maumbile. Nguvu za kikatili zinazoonekana kwa maumbile hazitoki kwa Mungu; zinapatikana kwa sababu tu tumemweka Mungu mbali nasi.

# 7

# Mbona Kuna Shetani?

Marejeleo tayari yamewekwa kwa kiumbe halisi wa kiroho aliyewekwa katika upinzani na Mungu. Kiumbe huyu anarejelewa katika Bibilia kama Shetani, ibilisi, joka, lewiathani, na Lusifa na vile vile kwa majina mengine.

Ikilinganishwa na miaka mia mbili iliyopita, asilimia ndogo zaidi ya watu katika ustaarabu wa magharibi siku hizi wanaamini ndani ya ibilisi halisi. Katika utamaduni wetu wa kisasa, Shetani daima ameachia katika ulimwengu wa ushirikina na ujinga. Ni kwa kuwa na mawazo haya akilini, na katika majibu kwa maswali, ndio tutachunguza kisa cha Bibilia cha shetani (adui).

Shetani anatambuliwa katika Bibilia kama malaika aliye asi. Neno *asi* linaashiria kuwa asilia Shetani alikuwa kiumbe mkamilifu ambaye alichagua Kuasi dhidi ya Muumbaji wake. Kwa nini aliasi dhidi ya Mungu ni siri, ukizingatia mazingira kamilifu ya mbinguni. Inavyoonekana, alishikilia nafasi ya kuheshimika na yenye ushawishi miongoni mwa malaika. Katika kipindi fulani cha wakati, mbegu ya kiburi ilimea na kukua ikipelekea katika kutoridhika na nafasi yake mbinguni. Hili hatimaye lilifika kilele kwa uasi wazi dhidi ya Mungu

Shetani hakuwa peke yake katika uasi wake. Alifanikiwa kupata kuungwa mkono na malaika wengine wengi, ingawaje wengi wa malaika walichagua kusalia watiifu kwa Mungu. Vita ambavyo vilitokea kutoka kwa uasi wa Shetani na wafuasi wake havikuwa vita vilivyohusisha silaha halisi kama zile ambazo zinatumika katika migogoro ya ulimwengu huu. Mungu alishinda katika vita hivi vya mbinguni kwa kutumia upendo dhidi ya ubinafsi, ukweli dhidi ya uongo, uwazi dhidi ya usiri,

mantiki dhidi ya kutowaza, uvumilivu dhidi ya kukata tamaa, na uaminifu dhidi ya tuhuma.

Ni jambo lenye busara kuamini kuwa mbinu ambazo zilitumiwa na Shetani kwa Hawa katika bustani ya Edeni kumsababisha kukengeuka kutoka kwa Mungu ni mbinu sawa na zile ambazo alitumia mwanzoni ili kupata wafuasi kwa mpango wake mbinguni. Hadi wakati huo, swali kuhusu haki ya Mungu halikuwa limeletwa mbele ya malaika wa mbinguni. Hawakuwa na njia kujua kwa uhakika Kabisa kama mashtaka ya Shetani dhidi ya Mungu yalikuwa na uhalali, au hayakuwa nao. Kwa sababu hii Shetani alikuwa amepewa fursa ya kudhihirisha njia yake ya utawala.

Tunaweza uliza mbona Mungu hakumwangamiza adui wake katika mwanzo wa uasi. Je, hilo halingezuia kuenea kwa uasi? Hapana, hili lingedhibitisha tu kwa malaika kuwa mashtaka ya Shetani dhidi ya Mungu *yalikuwa* ni halali. Kama Mungu angemwangamiza Shetani, kitendo hicho kingekuwa kimekiuka uhuru na kuufanya wazo tupu bila kiini. Kuna jambo lingine kando na hili. Ili kuwa dhabiti katika somo letu la Bibilia, uzito wa ushahidi unadhihirisha kuwa Mungu haangamizi kamwe—dhambi huangamiza. Shetani hatimaye ataangamizwa. Uangamizi huu hautatoka kwa Mungu, bali kwa dhambi za Shetani mwenyewe:

> Tena neno la Bwana likanijia, kusema, Mwanadamu, umfanyie maombolezo mfalme wa Tiro, umwambie, Bwana MUNGU asema hivi; Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri. Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako, akiki, na yakuti manjano, na almasi, na zabarajadi, na shohamu, na yaspi, na yakuti samawi, na zumaridi, na baharamani, na dhahabu; kazi ya matari yako na filimbi zako ilikuwa

> ndani yako; katika siku ya kuumbwa kwako zilitengenezwa tayari. *Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako.* Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi; kwa sababu hiyo nimekutoa kwa nguvu katika mlima wa Mungu, kama kitu kilicho najisi; nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto. *Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako;* nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama. Kwa wingi wa maovu yako, katika uovu wa uchuuzi wako, umepatia unajisi patakatifu pako; *basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza,* nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao. Wote wakujuao kati ya kabila za watu watakustaajabia; umekuwa kitu cha kutisha, *wala hutakuwapo tena hata milele.* (Ezek. 28:11–19, mkazo umetiliwa)

Mfalme wa Tiro, kwa kufaa, ni mfano wa Shetani katika kisa hiki. Shetani aliumbwa mkamilifu, bila chembe ya kiburi au ubinafsi. Anguko lake kutoka kwa ukamilifu lilikuwa kupenda kwake, na hakuwa na udhuru kwa uamuzi aliouchagua. Alijawa na kiburi kwa sababu ya uzuri wake. “moto” ambao utamteketeza Shetani hautatoka kwenye chanzo cha nje; utatoka ndani ya Shetani mwenyewe. Moto huu ni ubinafsi wake mwenyewe. Ni moto huu kutoka ndani yake ambao

utamteketeza. Shetani hatakuwepo—“wala hutakuwapo tena hata milele.”

> Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, *Nitakiinua* kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; *Nami nitaketi* juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. *Nitapaa* kupita vimo vya mawingu, *Nitafanana na yeye Aliye juu.* (Isa. 14:12–14, mkazo umetiliwa)

Lusifa (jina asili la Shetani) alianguka kwa sababu alitafuta kujiinua. Yesu aliwafunza wafuasi wake, “Kwa kuwa ye yote anayejikweza atashushwa, na ye yote anayejinyenyekeza atakwezwa” (Matt. 23:12). Lusifa alileta fedheha yake mwenyewe. Maneno yake “Nitafanana na yeye Aliye juu” yanasaliti ukweli kuwa alitamani tu nafasi ya Mungu. Hakuwa na azimio lolote la kuonyesha tabia ya Mungu (njia pekee ambayo kiumbe aliyeumbwa anaweza *fanana* na Mungu).

Tunapochunguza kifungu hiki, pia inafaa kufahamika kuwa mawazo yaliyoonyeshwa kumhusu Mungu ni ya Lusifa na wala sio maelezo halisi ya nia ya Mungu. Lusifa kwa sababu ya umajinuni wake wa kujiinua nafsi, alifikiria kuwa Mungu alikuwa na nia sawa ya ubinafsi.

> Basi palikuwa na vita mbinguni: Mikaeli na malaika zake wakapigana na hilo joka, nalo joka pamoja na malaika zake likapigana nao. Lakini joka na malaika zake wakashindwa na hapakuwa tena na nafasi kwa ajili yao mbinguni. Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani,

> aupotoshaye ulimwenguni wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake. (ufu. 12:7–9)

Kifungu hiki kinaelezea vita vya mbinguni ambapo Shetani alianza kazi yake ya udanganyifu. Kazi yake haijafungiwa katika pembe ndogo ya sayari; amedanganya "ulimwenguni wote."

> Yesu akawaambia, "Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama umeme wa radi. (Luka 10:18)

Yesu anazungumza hapa kuhusu kasi ya anguko la Shetani kutoka kwa uaminifu hadi kwa uasi.

> kwa sababu tumefanywa kuwa maonyesho kwa ulimwengu wote, kwa malaika na kwa wanadamu pia. (1 Kor. 4:9)

> Na wale waliowahubiri ninyi Injili kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni. Mambo ambayo hata malaika wanatamani kuyafahamu. (1 Petro 1:12)

Shetani alipoasi mbinguni, akichukua idadi ya malaika naye, malaika waaminifu waliosalia hawakufahamu kikamilifu kilichokuwa kikitendeka na mbona. Ujumbe wa injili ni wao, kama vile ulivyo wetu, na wanavutiwa sana katika juhudi za kujikana nafsi za Mungu juu ya dunia za kumuokoa mwanadamu kutoka kwa kujiangamiza. "Injili ya milele" (Ufu. 14:6) ni hakikisho kuwa ulimwengu utapata uhuru milele kutoka kwa shaka kuhusu uaminifu wa Mungu: "Mnawaza nini juu ya Bwana? Yeye atakomesha kabisa; mateso hayatainuka mara ya pili." (Nah. 1:9).

> Kisha Yesu akaongozwa na Roho Mtakatifu kuingia nyikani ili akajaribiwe na Ibilisi. Baada ya kufunga siku arobaini mchana na usiku, hatimaye akaona njaa. Mjaribu akamjia na kumwambia, "*Kama Wewe ndiye Mwana wa Mungu*, amuru mawe haya yawe mikate." Lakini Yesu akajibu, "Imeandikwa, 'Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'" Ndipo ibilisi akamchukua Yesu mpaka mji mtakatifu wa Yerusalemu na kumweka juu ya mnara mrefu mwembamba wa hekalu, akamwambia, "*Kama Wewe ndiye Mwana wa Mungu* jitupe chini, kwa kuwa imeandikwa, '"Atakuagizia malaika zake, nao watakuchukua mikononi mwao ili usije ukajikwaa mguu wako kwenye jiwe.'" Yesu akamjibu, "Pia imeandikwa: 'Usimjaribu Bwana Mungu wako.' " Kwa mara nyingine, ibilisi akamchukua Yesu mpaka kwenye kilele cha mlima mrefu na kumwonyesha falme zote za dunia na fahari zake, kisha akamwambia, "Nitakupa hivi vyote kama ukinisujudia na kuniabudu." Yesu akamwambia, "Ondoka mbele yangu, Shetani! Kwa maana imeandikwa, 'Utamwabudu Bwana Mungu wako, nawe utamtumikia Yeye peke yake.'"Ndipo ibilisi akamwacha, nao malaika wakaja na kumtumikia. (Matt. 4:1–11, mkazo umetiliwa)

Shetani alimjia Yesu kama mjaribu; lengo lake dhahiri likiwa kuzuia uaminifu na utegemezi wa Yesu kwa Baba yake. Shetani aliafikia mafanikio kwa kutumia njia sawa na zile alizotumia kwa Hawa katika bustani ya Edeni. Shetani alikuwa ameamua kuzuia lengo la Yesu la kuja ulimwenguni huu kukomboa mwanadamu kwa kumjaribu Yesu atumie nguvu zake za kiungu ili kujinufaisha. Mdanganyifu alikata tamaa kwa kumzuia Yesu kutofanikiwa katika huduma yake ya

kudhihirisha *ukosefu wa ubinafsi* wa Mungu— ambao ungemfunua Shetani kama mdanganyifu aliye.

Katika jaribu moja ibilisi alimpa Yesu "falme za ulimwengu" kama Yesu angemwinamia na kumwabudu. Ni muhimu kufahamu kuwa Yesu hakushindana na madai ya ibilisi ya utawala juu ya "falme za ulimwengu." Mungu alipomuumba binadamu mwanzo, alimpa binadamu "na nchi yote pia" (Mwa. 1:26), lakini Adamu na Hawa walipoamini uongo wa Shetani kumhusu Muumbaji wao, kimsingi walimkabidhi ibilisi utawala huu. Tunaona udanganyifu, ukandamizaji, matumizi ya nguvu, na kukosekana kwa usawa katika "falme za ulimwengu." Katika ufalme wa Mungu hakuna matumizi ya nguvu wakati wowote ule au katika hali yoyote ile. Hakuna ulinganifu wowote kati ya ufalme wake na falme za ulimwengu huu, ambazo hutegemea utawala wa sheria badala ya sheria ya upendo.

> Sitasema nanyi zaidi, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu anakuja, naye hana kitu Kwangu. (Yohana14:30)

Yesu anadhibitisha kuwa ni Shetani ambaye ni "mkuu wa ulimwengu huu." Tunapokataa uwepo wa Shetani na athari zake ambazo zimeenea katika sayari yetu, bila kujua tunaweka lawama juu ya Mungu kwa sababu ya kuteseka kwetu.

> Mwe na kiasi na kukesha, maana adui yenu Ibilisi, kama simba angurumaye huzungukazunguka akitafuta mtu ili apate kummeza. (1 Petro 5:8)

> Shetani ndiye adui yetu—sio Mungu.

> Vaeni silaha zote za Mungu ili kwamba mweze kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana

> kwetu si juu ya nyama na damu, bali dhidi ya falme, mamlaka, dhidi ya wakuu wa giza na majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. (Efe. 6:11–12)

Tunapogundua kuwa sisi sote ni waathiriwa wa udanganyifu kumhusu Mungu uliowekwa katika jamii ya mwanadamu, hatutawatazama wengine kama adui zetu, bali kama waathiriwa wenzetu katika udanganyifu huu mkubwa.

> Walikuwa na malaika kutoka kwenye hilo shimo lisilo na mwisho kama mfalme wao, ambaye jina lake kwa Kiebrania ni Abadonib na kwa Kiyunani ni Apolioni. (Ufu. 9:11)

"Malaika kutoka kwenye hilo shimo lisilo na mwisho" anarejelea Shetani. Apolioni jina ambalo amepewa hapa, linamaanisha *mwangamizi* katika Kiyunani. *Shetani* ni mwangamizi. Tutakuwa na udhuru wowote kwa ufanisi wa kumpa Mungu wetu mpole cheo sawa?

*Mwivi huja ili aibe, kuua na kuangamiza. Mimi nimekuja*

*ili wapate uzima kisha wawe nao tele.*

—Yesu (Yohana 10:10)

# 8

## Joka wa Uharibifu

Mapigo ambayo Mungu alituma dhidi ya Misri yanaonekana kuwa baadhi ya matendo ya makusudi zaidi ya Mungu ya kuangamiza. Kwa sura ya nje kunaonekana kutokuwepo kwa njia nyingine ya kufasiri matukio haya ya Bibilia. Kumbuka, ijapokuwa, fungu tulilosoma awali: "Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana." (Isa. 55:8).

Musa aliagizwa na Mungu kuwaongoza wana wa Israeli kutoka kwenye utumwa wa Misri na kuwa huru. Alikuwa aende mbele za Farao ili kumuonya dhidi ya majanga ambayo yangetokea katika nchi yake. Mungu alipokutana na Musa jangwani, alimpa funzo la kitu ambacho Musa na Haruni wangeonyesha baadaye mbele za Farao ambacho kingeonyesha mtawala hasa ni nini jukumu la Mungu lingekuwa katika matukio ya majanga yajayo:

> Bwana akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Akasema, Ni fimbo. Akamwambia, Itupe chini; akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake. Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; (akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake) (Kut. 4:2–4)

> Akasema, Je! Hayuko Haruni, ndugu yako, Mlawi? Najua ya kuwa yeye aweza kusema vizuri… Naye atakuwa msemaji wako kwa watu, hata yeye atakuwa mfano wa kinywa kwako, nawe utakuwa mfano wa Mungu kwake.

> Nawe utatwaa fimbo hii mkononi mwako, na kwa hiyo utazifanya zile ishara. (Kut. 4:14, 16–17)

Musa alikuwa aende mbele za Farao kama mwakilishi wa Mungu. Lengo la Mungu katika udhihirisho huu lilikuwa liwe zaidi kuliko onyesho la nguvu tu; lilikuwa ni mfano wa kutambua mwangamizi wa *kweli*. Wakati Musa, kama mwakilishi wa Mungu, alishika fimbo mkononi mwake, ishara ya nguvu za maumbile zikidhibitiwa na Mungu. Hakuna madhara yoyote yangekuja Misri kama Mungu amedhibiti nguvu za maangamizi za maumbile. Musa alipoitupa chini fimbo, ikawa nyoka, ishara ya maovu na maangamizi. Hii ilikuwa ishara ya nguvu za maumbile inje ya udhibiti wa Mungu na chini ya udhibiti wa Shetani— mwangamizi.

Mamia ya miaka kabla ya wakati wa Musa na baada ya Yusufu (ambaye alikuwa ameuzwa utumwani na nduguze wa kambo) alikuwa amefasiri ndoto za kusumbua za Farao, kulikuwa na mipango bora zaidi kwa wana wa Israeli. Farao alimwinua Yusufu katika mahali pa sifa njema na kuheshimika kwa kutafsiri ndoto za unabii na utabiri wake katika kuandaa taifa kwa njaa ya miaka saba. Familia ya Yusufu ilikuwa imekaribishwa kwa moyo mkunjufu. Wamisri walionyesha shukurani zao kwa Yusufu na Mungu aliyemwabudu. Mungu aliweza kulibariki taifa kwa utajiri. Miaka mingi baada ya kifo cha Yusufu, hata hivyo, Wamisri walisahau kumhusu na Mungu wake na wakawafanya wana wa Israeli kuwa watumwa ambao walikuwa wamefanikiwa na kuongezeka katika nchi. Wamisri, kwa matendo yao, walikuwa wakituma ujumbe kuwa hawakuwa wakitaka uwepo wa Mungu. Walikuwa na miungu yao wenyewe na hawakuta kumkiri Mungu wa watumwa wao. Mungu hakuweza tena kuendeleza hatua zake kikamilifu za kuwabariki na kuwalinda na wakati huo huo kuwaruhusu Wamisri uhuru wao wa kujitenga kutoka kwake.

Iwapo kwa wakati wowote baada ya mapigo kuanza, Farao angegeuka kutoka kwa mwenendo wake pekutevu na kuwaruhusu Waisraeli waende, Mungu angedhibiti nguvu za maumbile tena, na mapigo yangeisha. Mtawala huyu mkaidi hakufanya hili, na Misri iliachwa katika uharibifu. Jukumu la Mungu katika mapigo ya Misri linakuwa wazi tunapozingatia ujumbe wa ishara ambazo Mungu alitoa katika fimbo na nyoka.

Msaada zaidi wakumuondoa Mungu katika mashtaka ya uangamizi kwa mambo ya maumbile unapatikana katika kitabu cha 1 Wafalme. Nabii Eliya katika unyonge wa huduma yake alikuwa akimjifichia Yezebeli katika pango, ambaye alikuwa ameyatishia maisha yake. Mungu alimjia nabii wake aliyekimbia:

> Naye akamwambia, Unafanya nini hapa, Eliya? Akasema, Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga; nami nimesalia, mimi peke yangu; nao wanitafuta roho yangu, waiondoe. Akasema, Toka, usimame mlimani mbele za Bwana. *Na tazama, Bwana akapita;* upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; 12 na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto; lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto *sauti ndogo, ya utulivu*. (1 Wafalme 19:9–12, mkazo umetiliwa )

Mungu wetu mpole bado ananena kwa kusikika zaidi katika sauti yake tulivu.

# 9

# Uteka wa Ayubu

Kitabu cha Ayubu kinatoa ushahidi wazi wa jukumu la Shetani katika matendo ya kuteseka na kuangamiza. Pia kinatupa mtazamo juu ya eneo katika vita kati ya Mungu na nguvu za uovu. Ayubu, "mtu mkamilifu na mwelekevu" (Ayubu 1:8), alijipata ameshikwa katika moto mkubwa katika matukio haya muhimu ya vita vya kiroho:

> Ilikuwa, siku moja ambayo hao wana wa Mungu walikwenda kujihudhurisha mbele za Bwana, Shetani naye akaenda kati yao. Bwana akamwuliza Shetani, Umetoka wapi wewe? Ndipo Shetani akamjibu Bwana, na kusema, Natoka katika kuzunguka-zunguka duniani, na katika kutembea huku na huku humo. Kisha Bwana akamwuliza Shetani, Je! Umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? Kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mkamilifu na mwelekevu, mwenye kumcha Mungu na kuepukana na uovu. Ndipo Shetani akamjibu Bwana, na kusema, Je! Huyo Ayubu yuamcha Bwana bure? Wewe hukumzingira kwa ukigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibarikia, nayo mali yake imeongezeka katika nchi. Lakini nyosha mkono wako sasa, uyaguse hayo yote aliyo nayo, naye atakukufuru mbele za uso wako. Bwana akamwambia Shetani, Tazama, yote aliyo nayo yamo katika uwezo wako; lakini usinyoshe mkono wako juu yake yeye mwenyewe. Basi Shetani akatoka mbele za uso wa Bwana. (Ayubu 1:6–12)

Shetani mara moja alipanga kuangamiza kila kitu ambacho Ayubu alikuwa nacho, ikiwemo wana na binti zake. Katika uangamizi uliofuata, Shetani aliamua kutumia mashambulizi ya adui "Waseba" (v. 15) and "Wakaldayo" (v. 17), "Moto wa Mungu … kutoka mbinguni" (v. 16), and "upepo wenye nguvu ukatoka pande za jangwani" (v. 19).

Wakati ambao ni wazi katika kitabu cha Ayubu mwangamizi ni nani, wasomi wengi bado wanasumbuliwa na mateso ya Ayubu kwa sababu inaaminika kimakosa kuwa Mungu *alimruhusu* Shetani amtese Ayubu. Wazo ni kuwa kwa sababu Mungu ana uwezo wote, angemzuia Shetani asimshambulie Ayubu. Hata hivyo, uwezo wa Mungu haukuwa suala faafu kwa wakati huo; imekuwa na daima itakuwa kuhusu kanuni za utawala wa Mungu —Mungu ni thabiti katika kuwapa viumbe wake wenye akili aliowaumba uhuru, au hana? Uhuru, kuwa huru, lazima uwe hauwezi kurudishwa nyuma; kumaanisha kuwa hauwezi badilishwa na hauwezi ukakumbukwa—bila kuzingatia hali.

Katika kisa cha Ayubu, kulikuwa, kwa kuongeza, kitu kingine cha msingi kando na sifa ya Mungu—sayari yetu. Shetani alikuwa akiweka mikakati ya kuumaliza ulimwengu wetu (himaya iliyochukuliwa na adui) kama ufalme huru wake mwenyewe: "Bwana akamwuliza Shetani, Umetoka wapi wewe? Ndipo Shetani akamjibu Bwana, na kusema, Natoka katika kuzunguka-zunguka duniani, na katika kutembea huku na huku humo." (Ayubu 1:7).

Kama tutachukua uhuru wa kuangalia kwa kina kwa kufikiri, kimsingi Shetani alikuwa akimwambia Mungu, "Nimekuwa kuzunguka-zunguka duniani kote na inaonekana kuwa niko na uungwaji mkono mkubwa kwa mwenendo wangu; nadai haki yangu ya kutawala dunia kikamilifu." Katika drama yote inayofuata, Mungu (kwa shukurani) Alikuwa hatua moja

mbele za Shetani—Mungu alimjua mtumishi wake mwaminifu. Ayubu alisalia mwaminifu kwa Mungu licha ya kuteseka matata ya pili zaidi ya ushambulizi wa kishetani kama Bibilia inavyorekodi. Mwishowe, aliyahifadhi maisha ya Ayubu, na “akaugeuza uteka wa Ayubu, hapo alipowaombea rafiki zake” (Ayubu 42:10), ambao kwa kweli walikuwa katika hatari zaidi kuliko Ayubu mwenyewe—hawakumjua Mungu.

Kitabu cha Ayubu kinatupa umaizi wa vita vya kiroho ambavyo vinaendelea hivi leo kati ya Mungu na nguvu za giza. Tutakapoweza kuwa na taswira ya kitu chenye utata wa kueleweka cha hiari ya kukunjika ambacho Mungu huona wazi, tutaanza kuthamini uzito wa changamoto anayakumbana nayo.

Sisi kama viumbe wenye akili hatuko peke yetu katika ulimwengu wetu. Kuna viumbe wengi wa kiroho tunaogawanya nafasi nao—Shetani na jeshi lake la malaika walioasi. Wakipewa hali yetu ya ubinafsi na ile ya mapepo, dunia yetu ni jukwaa la migongano mingi ya hiari ya kujinufaisha kila siku. Kile ambacho ni kigumu hasa kwetu kufahamu ni jinsi Shetani na jeshi lake la mapepo linaweza mzuia au kumstahimili Mungu.

Linaweza kuwa jambo la kutusumbua tutakapotambua kuwa Mungu huwa hana udhibiti wote na utawala wa kila kitu katika sayari yetu. Hata hivyo, Mungu hana hamu ya kudhibiti maisha yetu binafsi, wala sio hali yake kufanya hivyo; alituumba tuwe huru viumbe wenye akili—sio gumegume.

Katika mwanzo wa kitabu cha Ayubu, wahusika watatu wakuu wanafunuliwa: Mungu, Shetani, na Ayubu. Katika mwisho wa kitabu Shetani hatajwi kwa jina. Mbona akosekane katika hitimisho hili muhimu la mkutano mkubwa na Mungu?

Sura nzima ya arobaini na moja ya Ayubu inaangazia kiumbe wa kustajabisha ambaye Mungu aliumba anayerejelewa kama “lewiathani.” Lewiathani ni nini au ni nani? Je, Bibilia inatoa kigezo chochote cha kutusaidia kutambua kiumbe hiki? “Katika siku hiyo Bwana, kwa upanga wake ulio mkali, ulio

mkubwa, ulio na nguvu, atamwadhibu lewiathani, nyoka yule mwepesi, na lewiathani, nyoka yule mwenye kuzonga-zonga; naye atamwua yule joka aliye baharini" (Isa. 27:1). Ni nini "nyoka yule mwepesi," "nyoka yule mwenye kuzonga-zonga," na "yule joka aliye baharini" inarejerea? "Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani, aupotoshaye ulimwenguni wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake." (Ufu. 12:9). Wacha tuchunguze sura ya arobaini na moja ya Ayubu kwa mtazamo wa sifa za Shetani katika maelezo ya kiumbe huyu:

> Je! Waweza wewe kumvua mamba kwa ndoana? Au, kuufunga ulimi wake kwa kamba? Je! Waweza kutia kamba puani mwake? Au kutoboa taya yake kwa kulabu? *Je! Atakusihi sana? Au, atakuambia maneno ya upole? Je! Atafanya agano pamoja nawe, Umtwae kuwa mtumishi wako milele? Je! Utamchezea kama ndege? Au, kumfunga kwa ajili ya wasichana wako? Je! Vikosi vya wavuvi watamfanyia biashara? Watamgawanya kati ya wafanyao biashara? Je! Waweza kuijaza ngozi yake na vyuma vyenye ncha, Au kichwa chake kwa vyusa? Mwekee mkono wako; Vikumbuke vile vita, wala usifanye tena. Tazama, kumtamani ni bure; Je! Hatambwaga chini huyo atakayemtazama? Hapana aliye mkali hata akathubutu kumwamsha; Bali ni nani awezaye kusimama mbele yangu mimi?* Ni nani aliyetangulia kunipa hata nimlipe? Kila kilicho chini ya mbingu nzima ni changu. Sitanyamaa kusema habari za via vyake, Wala nguvu zake kuu, wala umbo lake zuri. Ni nani awezaye kumbambua magamba yake? Ni nani atakayepenya dirii yake maradufu? Ni nani awezaye kuifungua milango ya uso wake? Meno yake yatisha kandokando yake. *Magamba yake yenye nguvu ndiyo*

*fahari yake, Yamefungamana pamoja kama kwa kufungwa kwa muhuri. Jinsi yalivyoshikamana Hata upepo hauwezi kupita kati.* Yamefungamana pamoja; Yameshikamana, hata hayawezekani kutengwa. Kwa kuchemua kwake mwanga humemetuka, Na macho yake yanafanana na makope ya alfajiri. Mienge iwakayo hutoka kinywani mwake, Na macheche ya moto huruka nje. *Moshi hutoka katika mianzi ya pua yake, Kama nyungu ikitokota, na manyasi yawakayo. Pumzi zake huwasha makaa, Na miali ya moto hutoka kinywani mwake. Katika shingo yake hukaa nguvu, Na utisho hucheza mbele yake. Manofu ya nyama yake hushikamana; Yanakazana juu yake; hayawezi kuondolewa. Moyo wake una imara kama jiwe; Naam, imara kama jiwe la chini la kusagia. Anapojiinua, mashujaa huogopa; Kwa sababu ya woga wao huvunjwa moyo. Mtu akimpiga kwa upanga, haumwingii; Wala fumo, wala mshale, wala mkuki wenye ncha. Yeye huona chuma kuwa kama nyasi, Na shaba kama mti uliooza. Mshale hauwezi kumkimbiza; Na mawe ya teo kwake hugeuka kuwa kama makapi. Marungu huhesabiwa kama mabua; Naye hucheka mshindo wa mkuki ukitupwa. Pande zake za chini ni kama vigae vikali; Hutandika malazi kama kuweka chombo cha kupuria nafaka juu ya matope. Yeye huchemsha kilindi mfano wa nyungu; Hufanya bahari kuwa kama mafuta. Hufanya mapito yake kung'aa nyuma yake Hata mtu angedhani kilindi kina mvi. Juu ya nchi hapana aliyefanana naye, Aliyeumbwa pasipo oga. Yeye hutazama kila kitu kilicho juu; Ni mfalme juu ya wote wenye kiburi.* (Ayubu 41, mkazo umetiliwa)

Mungu anatumia lugha ya mifano katika sura hii kuelezea adui mwenye nguvu na asiyekuwa na huruma ambaye hatuna nguvu za kupigana na adui huyu sisi wenyewe. Mungu anashiriki katika pambano kuu na adui wa kutisha wakufikirika, lakini Mungu amejitolea kupigana vita hivi kwa niaba yetu bila kutegemea matumizi ya nguvu katika wakati wowote au hali yoyote.

Shetani amemfanya Mungu kuonekana kama yeye alivyo: mwenye hasira, mwenye kisasi, asiyesamehe, kutumia nguvu, mshika-sheria, mhukumu, na mkali, ilihali kwa wakati huo huo, kwetu anaonekana kama "malaika wa nuru" (2 Kor. 11:14), lakini Mungu anaona wazi kile ambacho hatuwezi ona—jinsi mdanganyifu alivyo na ujuzi katika hila zake.

Tukiwa na maelezo haya ya mfano ya adui wa Mungu, tunaweza pata ufahamu wa vita vya kila siku ambavyo Mungu anapigana kwa kila mmoja wetu. Mungu haingilii kati kuwaondoa wana wake katika njia ya madhara wakati Shetani anavuka mipaka yake katika kukata tamaa kwake kuzuia au kuwaangamiza wale wasikivu wa Roho Mtakatifu. Kuingilia kati huku kwote inavyoonekana ni kwetu, wakati mengi sio. Kwa hivyo, Mungu ataendelea kukusanyiwa lawama kila siku kwa mateso tunayoyaona katika ulimwengu wetu. Natarajia yale ambayo Ayubu aliyapitia yatatusaidia kutambua kuwa Mungu *hawezi* zuia ajali zote, misiba yote, magonjwa yote, au vifo vyote kwa wakati huo huo akiheshimu mapenzi ya viumbe wake wenye akili.

Kuna jambo lingine ambalo Mungu huliona wazi. Yeye tu ndiye mwenye uwezo wa kuwepo binafsi—*Shetani hana*. Shetani ni kiumbe aliye chagua uovu, na uovu unategemea wema kikamilifu kwa uwepo wake. *Wakati* viumbe wenye akili katika ulimwengu huu wanafahamu ukweli huu, katika muktadha wa ufunuo kuhusu uaminifu wa Mungu, atamruhusu

Shetani, mwanzilishi wa uovu; kwa kujiangamiza binafsi; nini kinaweza kuwa haki kuliko hilo?

*Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.*

—Isaya 41:10

# 10

# Mbona Tunasoma Bibilia Visivyo

Bibilia haikuandikwa kama imla kutoka kwa Mungu, "bali watu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu." (2 Petro 1:21). Bibilia iliandikwa na watu kwa kutumia maneno ya, na katika muktadha wa utamaduni, usuli na hisia za kipekee za kila mwandishi.

Mbona mara nyingi inaonekana katika Bibilia kuwa Mungu *si* mwangamizi? Ili kujibu swali hili itasaidia kwanza kuangazia utamaduni wa kidini wa nchi za kale za Bibilia. Jambo moja ni dhahiri—wana wa Israeli, wahusika wakuu katika visa vya Bibilia, walizungukwa na athari ya ibada ya sanamu. Licha ya maonyo wazi waachane na ibada ya sanamu, walizidi kuathiriwa na mazoea ya jirani zao ya kuabudu sanamu. Ufahamu wa Mungu wa Israeli ulikuwa umepotoshwa na utamaduni uliokuwepo.

Mungu alitamani kujidhihirisha kwa watu. Hata hivyo, kudhihirisha utukufu wa tabia yake kikamilifu kwao kungewapeleka mbali zaidi naye. Mungu alijishusha katika kiwango cha watu aliokuwa anataka kufikia, na alihitaji kuzungumza lugha yao ili kufanya hivyo. Alikuwa hiari kufahamika visivyo katika mahusiano yake na watu wa Israeli ili kuwaokoa kutoka kwa kujiangamiza mwenyewe.

Hata zaidi, katika nchi za kale za Bibilia, watu chini ya athari za mapepo waliumba miungu ambayo ilikuwa katili na ilikasirika virahisi. Waliamini kuwa majanga ambayo waliteseka kwayo yalisababishwa na miungu hii yenye hasira. Hivyo, watu walileta dhabihu kutuliza hasira yao na wakaiinamia katika sherehe zao za kidini.

Katika Agano la Kale, machache zaidi yanatajwa kuhusu Shetani, kiumbe ambaye kwa *kweli* ndiye wa kulaumiwa kwa mateso na vifo katika ulimwengu wetu. Kama Shetani angetambuliwa kama anaye wajibikia majanga yote ambayo

watu wanapitia, uangalifu wao ungeelekezwa kwake badala ya Mungu. Waisraeli wangemchukulia Shetani kama mungu mwingine ambaye alikuwa na nguvu za kuvutia juu ya nguvu za maumbile. Hili lingewapelekea kutoa dhabihu kwake, na kwa kufanya hivyo wangemwabudu Shetani badala ya Mungu.

Mungu alitafuta kuzuia hili lisitendeke kwa kuruhusu yeye mwenyewe aonekane kuwa sio chemchemi ya vitu vizuri tu ambavyo watu hupokea bali vitu *vibaya* vile vile. Mungu alikuwa na wasiwasi zaidi juu ya watu na athari ambayo kufunuliwa mapema kwa utambulisho wa mwangamizi ingeleta kwao zaidi ya sifa yake mwenyewe. Hata kwa kutosheka huku kwa Mungu, watu bado walitoa heshima kwa uwepo wa mapepo kupitia kwa ibada ya sanamu: "Walitoa sadaka kwa pepo, si Mungu" (Kumb. 32:17).

Waisraeli wa kale hawakuwa tayari kwa ufunuo dhahiri wa Mungu mpole na tabia ya upendo. Wangemkataa tu Mungu hata kama angekuja kwao akionekana jinsi kweli alivyo—upendo wakujikana nafsi. Walitaka mungu ambaye angewapigania na kutumia ukatili dhidi ya adui zao. Waisraeli walimtaka mungu aliye kama *wao wenyewe*. Badala ya kuukubali ukweli kuwa "Mungu akaumba mtu kwa mfano wake" (Mwa. 1:27), walikuwa wameamua *kumuumba Mungu kwa mfano wao wenyewe*. Hili linatupa (kama tuko tayari kuliangazia) ufahamu wa jinsi jamii ya mwanadamu imehusiana na Mungu kimsingi tangu miaka ya kale hadi siku zetu.

# 11

## Mbona hatumuelewi Mungu

Mungu alipotembea kati yetu, hakutambuliwa au kukaribishwa na kuanzishwa kwa dini:

> Walipokuwa wanatoka, mtu mmoja aliyekuwa amepagawa na pepo na ambaye hakuweza kuongea aliletwa kwa Yesu. Yule pepo alipotolewa, yule mtu aliyekuwa bubu akaongea. Ule umati wa watu ukastaajabu na kusema, "Jambo kama hili kamwe halijapata kuonekana katika Israeli." Lakini Mafarisayo wakasema, *"Huyo anatoa pepo kwa uwezo wa mkuu wa pepo."* Yesu akazunguka katika miji yote na vijiji vyote, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri Habari Njema za Ufalme na kuponya kila ugonjwa na kila aina ya maradhi miongoni mwa watu. (Matt. 9:32–35, Mkazo umetiliwa)

Maneno yafuatayo ya Isaya yanafaa kutumiwa kwa wale waliomshtaki Yesu kuwa na ushirika na Shetani: "Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza; watiao uchungu badala ya utamu, na utamu badala ya uchungu! Ole wao walio wenye hekima katika macho yao wenyewe, na wenye busara katika fikira zao wenyewe!" (Isa. 5:20–21).

> Alikuwepo ulimwenguni na ingawa ulimwengu uliumbwa kwa Yeye, haukumtambua. Alikuja kwa walio Wake, lakini wao hawakumpokea. (Yohana 1:10–11)

Kifungu hiki hakirejelei historia ya kale tu. Mungu anaendelea kutotambuliwa, kutofahamika na kutojulikana. Tunakosa kumuelewa Mungu kwa sababu ya mazoea yetu ya kujijazia kimakosa kuwa ni mbinafsi kama sisi tulivyo:

> Mtu ambaye hana Roho wa Mungu hawezi kupokea mambo yatokayo kwa Roho wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa sababu hayo yanaeleweka tu kwa jinsi ya rohoni. (1 Kor. 2:14)

Jamii ya mwanadamu inavutiwa na dini ya nje. Badala yake tunachohitaji ni kubadilisha ubinafsi wetu na upendo wa Mungu. Wazo la kuwacha ubinafsi wetu linatisha sana kwa "mwanadamu asili." Dini ya nje *inaonekana* salama zaidi, lakini aina hii ya usalama ni udanganyifu wa ndani; dini ya nje mara nyingi inatumika kujificha kutoka kwa Mungu.

> Baadhi ya Mafarisayo wakamjia ili kumjaribu wakamwuliza, "Ni halali mtu kumwacha mke wake kwa sababu yo yote?'' Akawajibu, "Je, hamkusoma kwamba hapo mwanzo Mwumba aliwaumba mtu mume na mtu mke. Naye akasema, 'Kwa sababu hii mtu atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja?' Hivyo si wawili tena, bali ni mwili mmoja. Kwa hiyo kile alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe.'' Wakamwuliza, "Kwa nini basi Mose aliagiza mtu kumpa mkewe hati ya talaka na kumwacha?'' Yesu akawajibu, "Mose aliwaruhusu kuwaacha wake zenu kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu. Lakini tangu mwanzo haikuwa hivyo. (Matt. 19:3–8)

Mengi ya Agano la Kale huonyesha juhudi za Mungu za kuja karibu na watu wenye mioyo migumu. Mungu haeleweki katika mafungu ya maandiko ambayo anakumbatia mapenzi ya watu badala ya kuyaacha kama yasiyo na matumaini. Sisi ndio hukosa huruma – sio Mungu. Lakini bado mara nyingi tunasoma visivyo mwingiliano wa Mungu na watu wasio na huruma katika Agano la Kale. Kama tokeo, tunamshtumu Mungu kwa kuruhusu utumwa na kuwa na wake zaidi ya mmoja, kuendeleza vita vya ushindi, kuamurisha mauaji ya kimbari, na kutangaza adhabu kali kwa waasi wa sheria. Tunatoa mashtaka haya kwa sababu hatuelewi ukubwa wa tatizo linalohusishwa na moyo mgumu wa binadamu ambao Mungu alikubana nao daima katika mwingiliano wake na Israeli ya kale.

Yesu, katika mahubiri ya mlimani, alipanua sheria, akitoa matumizi halisi kutegemea sheria ya upendo:

> Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Jicho kwa jicho na jino kwa jino.' Lakini mimi nawaambia, msishindane na mtu mwovu. Lakini kama mtu akikupiga kwenye shavu la kuume, mgeuzie na la pili pia, Kama mtu akitaka kukushtaki na kuchukua shati lako, mwachie achukue na koti pia. Kama mtu akikulazimisha kwenda kilometa moja, nenda naye kilometa mbili. Mpe yeye akuombaye, wala usimgeuzie kisogo yeye atakaye kukukopa.'' (Matt. 5:38–42)

Katika maneno haya, Yesu alipanua juu ya mapenzi kamili kinyume na kukabiliana kwake na hali ya mapenzi ya mioyo migumu ya watu.

> Yesu akawaambia, ''Kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda, kwa maana nilitoka kwa Mungu na sasa niko hapa. Sikuja kwa ajili Yangu mwenyewe, ila Yeye

alinituma. Kwa nini hamwelewi ninayowaambia? Ni kwa sababu hamwezi kusikia nisemacho. *Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi,* nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba yenu. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hakushikana na kweli maana hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo uongo. Lakini kwa sababu nimewaambia kweli hamkuniamini! Je, kuna ye yote miongoni mwenu awezaye kunithibitisha kuwa mwenye dhambi? Kama nawaambia yaliyo kweli, mbona hamniamini? Yeye atokaye kwa Mungu husikia kile Mungu asemacho. Sababu ya ninyi kutosikia ni kwa kuwa hamtokani na Mungu.'' Wayahudi wakamjibu Yesu, "Je, hatuko sahihi tunaposema ya kwamba Wewe ni Msamaria na ya kwamba una pepo mchafu?" (Yohana 8:42–48, mkazo umetiliwa)

Baba yao alikuwa ibilisi kwa sababu walirithi sura ya Mungu iliyoumbuliwa na shetani na wakapinga badiliko lolote kwa sura hiyo.

Juu ya kichwa chake, kwenye msalaba, wakaandika shtaka lake: 'HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI.' Wanyang'anyi wawili walisulibiwa pamoja naye, mmoja kuume Kwake na mwingine kushoto Kwake. Watu waliokuwa wakipita njiani wakamvurumishia matukano huku wakatikisa vichwa vyao na kusema, "Wewe ambaye utalivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe basi! *Kama Wewe ni Mwana wa Mungu,* shuka kutoka msalabani.''

Vivyo hivyo, viongozi wa, makuhani, walimu wa sheria na wazee wakamdhihaki wakisema, "Aliwaokoa

> wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe!. *Yeye ni Mfalme wa Israeli!* Ashuke sasa kutoka msalabani, tutamwamini. Anamwamini Mungu, basi Mungu na amwokoe sasa *kama anamtaka*, kwa maana alisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.' '' (Matt. 27:37–43, mkazo umetiliwa)

Wale waliomdhihaki Yesu msalabani walitumia uchongezo sawa na ule ambao Shetani alitumia jangwani kumjaribu Kristo: "Kama Wewe ndiye Mwana wa Mungu" (Matt. 4:3).

> Hakuna mtu awekaye divai mpya kwenye viriba vikuukuu. Akifanya hivyo, hiyo divai mpya itapasua hivyo viriba nayo yote itamwagika. Divai mpya lazima iwekwe kwenye viriba vipya. (Luka 5:37–38)

Yesu katika mfano huu, anafananisha mafunzo yake mapya ya kiradikali na "divai mpya" ikipasua "viriba vizee." Yesu kwa neno na mfano alichora sura wazi ya upendo wa Mungu ambao ulionekana kuwa na tofauti kamili na *sura ya Mungu iliyoumbuliwa* ("divai ya kale") iliyoshikiliwa na viongozi wa dini ("viriba vya kale") alivyokumbana navyo. Mitazamo hii miwili kinzani haiwezi ikachanganywa pamoja. Na ndivyo ilivyo leo. Sura ya mungu katili lazima iende kufanya makao kwa Mungu wetu mpole mawazoni mwetu.

# 12

# Jinsi Mungu Huangamiza

Moja wapo wa mifano bayana ya jinsi Mungu huangamiza unapatikana katika kitabu cha 1 Mambo ya Nyakati. Sauli mfalme wa Israeli alikuwa akikiuka mashauri ya Mungu, aliyowasilisha kwake kupitia nabii Samueli, ageuke kutoka kwa mwendo wake wa uharibifu. Sauli alikuwa amefanya majaribio kadhaa ya kumuua Daudi, mtumishi wake mwaminifu. Pia alikuwa na hatia ya kusababisha mauaji ya kuhani wa Nob, alikuwa amepokea ushauri wa mchawi. Sauli alikuwa amepata jeraha katika vita na Wafilisti, na alikuwa na hofu ya kile ambacho kitatendeka kama angeshikwa. Katika kukata tamaa kwake, "Basi Sauli akautwaa upanga wake, akauangukia." (1 Nyak. 10:4).

Zingatia jinsi Bibilia inahitimisha kisa hiki cha kifo cha Sauli:

Basi Sauli alikufa kwa sababu ya kosa lake alilomkosa Bwana, kwa sababu ya neno la Bwana, asilolishika; na tena kwa kutaka shauri kwa mwenye pepo wa utambuzi, aulize kwake, asiulize kwa Bwana; kwa hiyo akamwua, na ufalme akamgeuzia Daudi, mwana wa Yese. (1 Nyak. 10:13–14)

Ni dhahiri kuwa katika kifo cha Sauli *jukumu* tu ambalo tunaona Mungu akitekeleza ni kumuacha Sauli kufuata njia yake mwenyewe na kukabiliana na matokeo ya matendo yake. Kisababishi cha kifo cha Sauli kilikuwa kujiiua, wala sio mauaji, na bado Bibilia inaarifu kuwa Mungu *alimuua*. Neno ambalo linatumika hapa kuelezea kile alichokifanya Mungu limeamuliwa tofauti na maana kutoka kwenye kamusi. Huu sio mfano pekee, katika sura ifuatayo, maneno katika Bibilia kama

vile hasira, ghadhabu, na wivu yatachunguzwa. Maandiko yanayapa maneno haya maana tofauti kabisa kutoka na ile ya matumizi ya kawaida tunaporejelea njia ya Mungu na mawazo ya Mungu.

*Mtafuteni Bwana, maadamu anapatikana, Mwiteni, maadamu yu karibu; Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa. Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.*

—Isaya 55:6–9

# 13

## Hasira ya Mungu ni Nini?

Swali la hasira ya Mungu hustajabisha wengi wetu tunaposoma Agano la Kale. Kuna marajeleo mengi kwa hasira ya Mungu na ghadhabu, lakini hasira yake *ni* nini? Kwa kujibu swali hili, itapendeza kuangalia mifano kadhaa katika Bibilia. Kutajwa kwa mara ya kwanza kwa hasira ya Mungu ilikuwa alipomwamuru Musa kuwaongoza wana wa Israeli kutoka utumwa wa Misri na kuwa huru. Ni mambo yepi ambayo yalimfanya Mungu kudhihirisha hasira yake wakati huo?

> Musa akamwambia Bwana Ee Bwana, mimi si msemaji, tokea zamani, wala tokea hapo uliposema na mtumishi wako; maana mimi si mwepesi wa kusema, na ulimi wangu ni mzito. Bwana akamwambia, Ni nani aliyekifanya kinywa cha mwanadamu? Au ni nani afanyaye mtu kuwa bubu au kiziwi, au mwenye kuona, au kuwa kipofu? Si mimi, Bwana? Basi sasa, enenda, nami nitakuwa pamoja na kinywa chako, na kukufundisha utakalolinena. Akasema, Ee Bwana, nakuomba, tuma kwa mkono wake huyo utakayemtuma. (Kut. 4:10–13)

Musa alikuwa amejawa na hofu ya kwenda mbele ya Farao peke yake na akaomba msemaji. Mungu alijibu vipi?

> Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Musa, akasema, Je! Hayuko Haruni, ndugu yako, Mlawi? Najua ya kuwa yeye aweza kusema vizuri. Pamoja na hayo, tazama, anakuja kukulaki; naye atakapokuona, atafurahi moyoni mwake. (Kut. 4:14)

Mungu alidhihirisha vipi hasira yake? Kwa kumpa Musa alichokuwa akitaka. Wacha tuangalie baadhi ya mafungu mengine ya Bibilia kwa kurejelea hasira ya Mungu:

> Kisha mkutano wa wafuasi waliokuwa kati yao, wakashikwa na tamaa; wana wa Israeli nao wakalia tena, wakasema, N'nani atakayetupa nyama tule? Basi Musa akawasikia watu wakilia katika jamaa zao zote, kila mtu mlangoni pa hema yake; na hasira za Bwana zikawaka sana; Musa naye akakasirika. Kisha upepo ukavuma kutoka kwa Bwana, nao ukaleta kware kutoka pande za baharini, nao ukawaacha wakaanguka karibu na kambi, kama kiasi cha mwendo wa siku moja upande huu, na kama kiasi cha mwendo wa siku moja upande huu, kuizunguka, nao wakafikilia kiasi cha dhiraa mbili juu ya uso wa nchi. Watu wakaondoka mchana huo wote, na usiku huo wote, na siku ya pili yote, kuwakusanya hao kware; yeye aliyepata ya upungufu kuliko wenziwe alipata kiasi cha homeri kumi; nao wakawaanika wote kandokando ya kambi kuizunguka pande zote. (Hes. 11:4, 10, 31–32)

Katika tukio hili, tunapata tena hasira ya Mungu ikitajwa. Alifanya nini? Aliwapa watu walichokuwa wakitaka.

> Hata Samweli alipokuwa mzee, aliwafanya wanawe wawe waamuzi juu ya Israeli. Na jina la mwanawe mzaliwa wa kwanza aliitwa Yoeli; na jina la wa pili Abiya; walikuwa waamuzi katika Beer-sheba. Ila wanawe hawakuenda katika njia zake, bali waliziacha, ili wapate faida; wakapokea rushwa, na kupotosha hukumu. Ndipo wazee wote wa Israeli wakakutana pamoja, wakamwendea Samweli huko Rama;

> wakamwambia, Angalia, wewe umekuwa mzee, na wanao hawaendi katika njia zako; basi, tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote. Lakini neno hilo likawa baya machoni pa Samweli, waliposema, Tupe mfalme atuamue. Naye Samweli akamwomba Bwana. Bwana akamwambia Samweli, Isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokuambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao. (1 Sam. 8:1–7)

Mungu alituma ujumbe kwa watu wake kupitia kwa nabii wake Samweli akiwapa sababu nyingi mbona haitakuwa kwa uzuri wao kwake kuwakabidhi hitaji lao la mfalme. Je, walimsikiliza Samweli?

> Walakini hao watu wakakataa kuisikiliza sauti ya Samweli; wakasema, Sivyo hivyo; lakini tunataka kuwa na mfalme juu yetu; ili sisi nasi tufanane na mataifa yote; tena ili mfalme wetu atuamue, tena atoke mbele yetu na kutupigia vita vyetu. (1 Sam. 8:19–20)

Mungu alijibu vipi kwa msisitizo huu wa watu? "Bwana akamwambia Samweli, Isikilize sauti yao, ukawafanyie mfalme." (v. 22). Tunajuaje kuwa Mungu aliwapa mfalme kwa hasira? Nabii Hosea, akirejelea tukio hili la kihistoria, anatupa mtazamo wa Mungu juu ya jukumu lake katika kuwapa hitaji lao:

> Haya ndiyo maangamizo yako, Ee Israeli, ya kuwa wewe u kinyume changu mimi, kinyume cha msaada wako. Yuko wapi sasa mfalme wako, apate kukuokoa katika miji yako yote? Na hao waamuzi wako, uliowanena hivi, Nipe mfalme na wakuu? *Nimekupa*

> *mfalme katika hasira yangu,* nikamwondoa katika ghadhabu yangu. (Hos. 13:9–11, mkazo umetiliwa)

Matukio haya matatu ya maandiko yanatuonyesha wazi kuwa hasira ya Mungu ilikuwa sawa na kuwapa watu wa Israeli walichokitaka ilhali hakikuwa kwa manufaa ya maahitaji yao kwake kufanya hivyo. Hili linatosha, angalau kidogo, kupendekeza kuwa hasira ya Mungu inaweza elezewa, kutoka kwenye Bibilia, kama kitu ambacho kimeamuliwa tofauti kutoka kwa maelezo yanayopatikana katika kamusi. Hata hivyo, kuna zaidi ya haya. Nini kilitendeka Yesu alipokasirika?

> Yesu akaingia tena ndani ya sinagogi na huko palikuwa na mtu mwenye mkono uliopooza. Wakawa wanamwangalia ili waone kama atamponya siku ya Sabato wapate sababu ya kumshtaki. Yesu akamwambia yule mwenye mkono uliopooza, ‘‘Njoo hapa mbele.” Kisha Yesu akawauliza, ‘‘Je ni lipi lililo halali siku ya Sabato, kufanya jema au baya”, kuokoa maisha au kuua?” Lakini wao wakanyamaza kimya. Yesu akawatazama pande zote kwa hasira, akahuzunika sana kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao. Akamwambia yule mtu mwenye mkono uliopooza, ‘‘Nyosha mkono wako.’’ Akaunyosha, nao ukapona kabisa! Kisha Mafarisayo wakatoka nje, mara wakaanza kufanya shauri la kumwua Yesu wakiwa na kundi la wafuasi wa Herode. (Marko 3:1–6)

Hili ni pambano ambalo Yesu alikuwa nalo na Mafarisayo. Ushikaji wao wa sheria za vizuio ulipiga marufuku uponyaji siku ya Sabato. Yesu kwa kuisoma mioyo yao, “Yesu akawatazama pande zote kwa hasira.” Yesu alikuwa na hasira ya aina gani? Aina ambayo inaelezewa kama “akahuzunika sana kwa ajili ya

ugumu wa mioyo yao." Yesu alikuwa katika huzuni au sikitiko la ndani kwa ukosefu wa upendo na huruma ulioonyeshwa na viongozi hawa wa dini wasiokuwa na huruma kwa mtu mwenye mkono uliopooza. Nini zaidi ambacho tunaweza gundua katika Bibilia kuhusu hasira na ghadhabu ya Mungu?

> *Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa* kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga kweli kwa uovu wao (Rom. 1:18, mkazo umetiliwa)
>
> *Ghadhabu ya Mungu inabainikaje*?
>
> Kwa hiyo, *Mungu akawaacha* wazifuate tamaa mbaya za mioyo yao. (Rom. 1:24, mkazo umetiliwa)
>
> Kwa sababu hii, *Mungu aliwaacha* wavunjiane heshima. (Rom. 1:26, emkazo umetiliwa)
>
> Nao kwa kuwa walikataa kumkubali Mungu, *Yeye akawaacha* wafuate akili zao za upotovu. (Rom. 1:28, mkazo umetiliwa)

Ghadhabu ya Mungu inaelezewa hapa kama kuwaacha ama kuwapeana – kwa njia nyingine, Mungu anawapa watu uhuru wajitenge kutoka kwake mwenyewe. Sio hasa ghadhabu ya kulipiza kisasi kwa kuangamiza mara nyingi tunavyomwelekezea Mungu. Wacha tuangalie mafungu mengine zaidi katika Agano la Kale.

> Watu wakaondoka mchana huo wote, na usiku huo wote, na siku ya pili yote, kuwakusanya hao kware; yeye aliyepata ya upungufu kuliko wenziwe alipata

> kiasi cha homeri kumi; nao wakawaanika wote kandokando ya kambi kuizunguka pande zote. Kisha hapo hiyo nyama ilipokuwa ikali kati ya meno yao, hawajaitafuna bado, hasira za Bwana ziliwaka juu ya watu, Bwana akawapiga watu kwa pigo kuu mno. (Hes. 11:32–33)

Tunarejea hapa katika tukio la kware ambao Mungu aliwapa watu kwa Hasira. Kulikuwa na tokeo la asili kutokana na tamaa ya watu: "Bwana akawapiga watu kwa pigo kuu mno."

Ni vyema kutambua kuwa tani ya nyama ya kware wambichi hawangekaa kwa muda mrefu katika mazingira ya jangwani mahali ambapo Waisraeli walikuwa wameweka kambi. Nyama ingeharibika upesi na kuwa mbaya kwa matumizi ya binadamu. Kwa kuzingatia ukweli huu, ni aina gani ya pigo ambayo ingetokea? Kwa uwepo wa kidudu sahihi na hali sahihi, kutiwa sumu kwa chakula ni mateso ya mauti: "Jina la mahali pale likaitwa Kibroth-hataava; maana, ni hapo walipowazika hao watu waliotamani." (v. 34). Nini kilikuwa "ghadhabu ya Bwana"? Haifuati kwa sababu kuwa ghadhabu ya Mungu ilikuwa kutoingilia kati katika tukio sababishi na tokeo?

> Ndipo hasira yangu itakapowaka juu yao siku hiyo, nami nitawaacha, nitawaficha uso wangu, nao wataliwa, tena watajiliwa na mambo maovu mengi na mashaka; hata waseme siku hiyo, Je! Kujiliwa kwetu na maovu haya si kwa sababu Mungu wetu hayumo kati yetu? Nami nitawaficha uso wangu kwa kweli siku hiyo, kwa maovu yote waliyoyafanya, kwa kuigeukia hiyo miungu mingine. (Kumb. 31:17–18)

Inamaanisha nini Mungu anapoficha uso wake? "Maovu haya si kwa sababu Mungu wetu hayumo kati yetu?" Hii tena ni

lugha ambayo inaelezea kutokuingilia kwa Mungu. Mbona Mungu akasema kuwa angeficha uso wake? “kwa maovu yote waliyoyafanya, kwa kuigeukia hiyo miungu mingine.” Na matokeo yangekuwa ni yepi? “Nao wataliwa, tena watajiliwa na mambo maovu mengi na mashaka.” Watu walipoigeukia miungu mingine, walitanga mbali na Mungu wa kweli, na hakuwa na uwezo wa kuwakinga dhidi ya matokeo yasiyoepukika.

> Wana wa Israeli walifanya yaliyokuwa ni maovu mbele za macho ya Bwana, nao wakawatumikia Mabaali. Wakamwacha Bwana, Mungu wa baba zao, aliyewaleta kutoka katika nchi ya Misri, wakafuata miungu mingine, baadhi ya miungu ya watu wale waliokaa karibu nao pande zote, wakajiinamisha mbele yao; wakamkasirisha Bwana, akaghadhibika. Wakamwacha Bwana, wakamtumikia Baali na Maashtorethi. Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, naye akawatia katika mikono ya watu waliowateka nyara, akawauza na kuwatia katika mikono ya adui zao pande zote; hata wasiweze tena kusimama mbele ya adui zao. (Waamuzi. 2:11–14)

Kifungu hiki kinaelezea watu wakiendelea na uasi kwa Bwana. Hapa Mungu “Naye akawatia katika mikono ya watu waliowateka nyara.” na “Akawauza na kuwatia katika mikono ya adui zao.” Hili tena ni pokeo ndogo la mgogoro. Kwa sababu ya uasi wao, Mungu hakuweza kuwakinga Israeli dhidi ya adui zao kuiteka nchi yao.

> Kwa kuwa Bwana atawapiga Israeli kama manyasi yatikiswavyo majini; naye atawang'oa Israeli katika nchi hii njema, aliyowapa baba zao, naye atawatawanya ng'ambo ya Mto; kwa sababu wamejifanyia maashera

> yao, wakimkasirisha Bwana. Naye atawatoa Israeli kwa ajili ya makosa ya Yeroboamu, aliyoyakosa, ambayo kwa hayo amewakosesha Israeli. (1 Wafalme 14:15–16)

Hapa hasira ya Mungu (na kuwapiga) *in kuiacha* Israeli potofu.

> Wakamkasirisha kwa mahali pao pa juu, Wakamtia wivu kwa sanamu zao. Mungu akasikia, akaghadhibika, Akamkataa Israeli kabisa. Akaiacha maskani ya Shilo, Hema aliyoiweka katikati ya wanadamu; Akaziacha nguvu zake kutekwa, Na fahari yake mkononi mwa mtesi. Akawatoa watu wake wapigwe kwa upanga; Akaughadhibikia urithi wake. (Zab. 78:58–62)

Hapa kijelezi cha ghadhabu ya Mungu kinahusisha: kuwakataa, *kuwatoa kuwa mateka*, na kuwaacha.

> Hasira ya Bwana ikawaka juu ya watu wake, Akauchukia urithi wake. Akawatia mikononi mwa mataifa, Nao waliowachukia wakawatawala. (Zab. 106:40–41)

Ghadhabu ya Mungu hapa inaelezewa kama "Akawatia mikononi mwa mataifa."

> Kwa ghadhabu ifurikayo nalikuficha uso wangu dakika moja; lakini kwa fadhili za milele nitakurehemu, asema Bwana, Mkombozi wako. (Isa. 54:8)

Katika kifungu hiki, “ghadhabu ifurikayo” inaelezewa kama kuficha uso wake “dakika moja,” lakini fadhili na huruma za Mungu kwetu ni za milele.

> Nami nitawatupa ninyi mbali na macho yangu, kama nilivyowatupa ndugu zenu wote, yaani, wazao wote wa Efraimu. Je! Watu hawa wanikasirisha mimi? Asema Bwana; hawajikasirishi nafsi zao, na kuzitia haya nyuso zao wenyewe? Kwa hiyo, Bwana MUNGU asema hivi, Tazama, hasira yangu na ghadhabu yangu zitamwagwa juu ya mahali hapa, juu ya wanadamu, na juu ya wanyama, na juu ya miti ya mashamba, na juu ya mazao ya nchi; nayo itateketea, isizimike. (Yer. 7:15, 19–20)

Mungu anauliza, “Je! Watu hawa wanikasirisha mimi? …hawajikasirishi nafsi zao, na kuzitia haya nyuso zao wenyewe?” Matatizo ya watu yaliletwa kama tokeo la ibada yao ya sanamu sio kama adhabu kutoka kwa Mungu.

> Zikate nywele zako, Ee Yerusalemu, uzitupe, Ukafanye maombolezo juu ya vilele vya milima; Kwa maana Bwana amekikataa na *kukitupa Kizazi cha ghadhabu yake*. (Yer. 7:29, mkazo umetiliwa)

Kuna mafungu zaidi ya Bibilia yanayotumia istilahi sawa, lakini haya ambayo tumeangalia yanatosha kukata kesi ya kulazimisha kuwa ghadhabu ya Mungu sio adhabu kutoka kwake. Mungu hutupa uhuru wa kumkubali au kumkataa. Ghadhabu ya Mungu ni tokeo asili la uchaguzi wetu mbaya, anapolazimishwa kutuacha tufuate njia zetu wenyewe. Jukumu la Mungu daima ni la kutazama tu linalorejelewa kama: *Kuwakataa, kuficha uso wake, kuwaacha, kukitupa, kuwapeana* na istilahi sawa.

Katika tangazo lake mbele ya Musa, Mungu hakutaja *ghadhabu* au *hasira* kama sifa ya tabia yake: "Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi" (Kut. 34:6–7).

> Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani? Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu. Bwana akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa. (Hes. 21:5–6)

Kifungu hiki kinatwalifu kuwa "Bwana akatuma nyoka za moto kati ya watu" kwa kuitikia manung'uniko yao. Kutoka kwenye ushahidi wa maandiko tumeangalia hadi sasa, kile kingekuwa kitendo cha Mungu "alipotuma" nyoka? Kwa maelewano na mafungu mengine ya Bibilia tumechunguza, Mungu alilazimishwa na ukosefu wa shukurani wa watu kwa uasi kuwapa uhuru kutoka kwa kinga yake ya kuingilia kati kwa niaba yao.

Nyoka za moto zilitokeaje? "[Bwana Mungu wako] aliyekuongoza katika jangwa lile kubwa lenye kitisho, *lenye nyoka za moto* na nge, nchi ya kiu isiyokuwa na maji; aliyekutolea maji katika mwamba mgumu" (Kumb. 8:15, mkazo umetiliwa).

Nyoka wa moto walikuwepo tangia mwanzo kama moja wapo ya vizuizi vingi ambavyo Mungu aliwakinga Waisraeli dhidi yake katika mazingira ya jangwani. Tukio hili la Mungu kuwatuma nyoka wa moto lingekuwa tatizo tu kama Mungu angetuma dubu wenye njaa badala yake.

Kuna matukio mengi katika Bibilia ya Mungu akituma adui wavamizi au majanga kadha dhidi ya watu. Kwa ufahamu huu, tunaweza hitimisha kimantiki kuwa katika kila tukio la maandiko ambapo Mungu *anatuma* kitu cha kudhuru, inamaanisha Mungu hakuweza kukikinga kisitokee bila kudanganya kisababishi na matokeo ya matukio. Sio kusudi la Mungu, wala sio katika tabia yake, kuonyesha utawala juu ya maswala ya binadamu

> Hapo ndipo Bwana alipoona wivu kwa ajili ya nchi yake, akawahurumia watu wake. Bwana akajibu, akawaambia watu wake; Tazameni, nitawaletea nafaka, na divai, na mafuta, nanyi mtashiba kwa vitu hivyo; wala sitawafanya tena kuwa aibu kati ya mataifa. (Yoeli 2:18–19)

> Basi yule malaika aliyesema nami akaniambia, Haya, piga kelele na kusema, Bwana wa majeshi asema hivi, Naona wivu kwa ajili ya Yerusalemu, na kwa ajili ya Sayuni; naona wivu mkuu sana. (Zek. 1:14)

> Ninawaonea wivu, wivu wa kimungu, kwa kuwa mimi niliwaposea mume mmoja, ili niwalete kwa Kristo kama mabikira safi. Lakini nina hofu kuwa, kama vile Eva alivyodanganywa kwa ujanja wa yule nyoka, mawazo yenu yasije yakapotoshwa, mkauacha unyofu na usafi wa upendo wenu kwa Kristo. (2 Kor. 11:2–3)

Wivu wa Mungu sio wa ubinafsi kabisa. Mungu ana wivu kwa wengine, sio kwake mwenyewe.

> Tena hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, akamtia Daudi nia juu yao, akisema, Nenda, ukawahesabu Israeli

> na Yuda. Basi mfalme akamwambia Yoabu, jemadari wa jeshi la askari, waliokuwa pamoja naye, Zunguka sasa katikati ya kabila zote za Israeli, tangu Dani mpaka Beer-sheba, mkawahesabu watu, nipate kujua jumla ya hao watu. Naye Yoabu akamwambia mfalme, Bwana, Mungu wako, na awaongeze watu, hesabu yao ikiwa yo yote, mara mia, tena macho ya bwana wangu mfalme na yawaone; ila kwa nini neno hili limempendeza bwana wangu mfalme? Lakini neno la mfalme likawa na nguvu juu ya Yoabu, na juu ya majemadari wa jeshi. Basi Yoabu akatoka na majemadari wa jeshi machoni pa mfalme, kwenda kuwahesabu watu wa Israeli. (2 Sam. 24:1–4)

Daudi alipowahesabu Israeli alikuwa akidhihirisha kiburi na kutomwamini Mungu kwa kutazama hesabu ya binadamu na nguvu za majeshi kuilinda Israeli. Hili kwa ufanisi halikuhusisha ulinzi wa Mungu usiokuwa wa vurugu, na kuwaacha katika mazingira ngumu kwa adui zao na vitisho vingine. Hata Yoabu jemedari wa vita aliona hatari katika ombi la mfalme la kuwahesabu watu wa Israeli na akamuuliza swali juu ya wazo hilo.

Mungu "akamtia Daudi nia juu yao." Kuna weza kuwa na tatizo kuelewa sentensi hii jinsi ilivyo? Mungu alikuwa akimnogonezea Daudi sikioni awahesabu Israeli ndivyo awe na udhuru mzuri wa kugeuka dhidi yao? Wacha tuangalia fungu hili kwa mwanga wa yale ambayo tumejifunza hadi sasa kuhusu jukumu la Mungu.

Mungu hachukui jukumu la utendaji katika uangamizi, na hachochei uovu, lakini kuna mtu ambaye hutenda. Inawezekana, katika tukio hili, kuwa Mungu "alimtia nia" Daudi kuwahesabu Israeli kwa kutomzuia kufanya hivyo? Na inaweza enda zaidi na kupendekeza kuwa haikuwa Mungu aliyekuwa akimnongonezea

Daudi sikioni bali Shetani? Tutajuaje? Tunaweza soma kuhusu tukio hili katika kitabu cha 1 Mambo ya nyakati: “Tena shetani akasimama juu ya Israeli, *akamshawishi* Daudi kuwahesabu Israeli” (1 Nyak. 21:1, mkazo umetiliwa).

Tunaweza shangaa mbona Bibilia haiji moja kwa moja na kusema wazi hasa kilichotendeka katika kila pambano ndani ya kurasa zake; si hilo linaweza fanya mafundisho ya Bibilia rahisi zaidi? Bila shaka, linaweza. Hata hivyo, tatizo la mawasiliano kati ya Mungu na binadamu halijawahi kuwa kwa sababu ya Mungu kukosa kufahamu, bali kwa sababu yetu. Mungu, katika hekima yake, hutupa uchaguzi wa kukubali au kukataa ukweli kumhusu. Bibilia iliandikwa kwa kanuni hii muhimu mawazoni. Tunapokuwa na fursa ya kuelewa ukweli wa kuokoa kumhusu Mungu na kuukataa, mwanga zaidi utatusongesha mbali naye zaidi. Utata wa uso wa Bibilia unaruhusu fasiri kinzana kwa sababu hiyo. Haiko katika tabia ya Mungu kutushawishi, dhidi ya mapenzi yetu, kumwamini na upendo wake usiobadilika. Kwa wakati huo huo, Bibilia hutupa ushahidi chungu nzima kwa wale wanaotafuta Mungu wetu mpole kumpata.

*Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.*

*—Yeremia 29:13*

# 14

# Jinsi Mungu Hufanya Vita

Mungu hufanya vita dhidi ya uovu kwa ukweli, upendo, huruma na msamaha.

> Yeye atendaye dhambi ni wa Ibilisi, kwa sababu Ibilisi amekuwa akitenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi za Ibilisi. (1 Yohana 3:8)

Kazi ya ibilisi tangia mwanzo wa uasi wake imekuwa kumshtaki na kumwakilisha Mungu visivyo. Yesu, Mwana wa Mungu, aliangamiza kazi za ibilisi kwa kuonyesha kuwa shutuma zake dhidi ya Mungu zilikuwa ni za uongo.

> Kwa nini hamwelewi ninayowaambia? Ni kwa sababu hamwezi kusikia nisemacho. Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba yenu. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hakushikana na kweli maana hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo uongo. (John 8:43–44)

Yesu anathibitisha kwamba silaha ya msingi ya ibilisi ni matumizi ya uongo. Ni “Mungu hawezi kusema uongo.” (Ebr. 6:18); Anapambana na uongo wa ibilisi kwa ukweli.

> Vaeni silaha zote za Mungu ili kwamba mweze kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu si juu ya nyama na damu, bali dhidi ya falme,

> mamlaka, dhidi ya wakuu wa giza na majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa hiyo vaeni silaha zote za Mungu ili mweze kushindana siku ya uovu itakapokuja nanyi mkiisha kufanya yote, simameni imara. Kwa hiyo simameni imara mkiwa mmejifunga kweli kiunoni na kuvaa dirii ya haki kifuani, nayo miguu yenu ifungiwe utayari tuupatao kwa Injili ya amani. Zaidi ya haya yote, twaeni ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Vaeni chapeo ya wokovu na mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu. (Efe. 6:11–17)

Yesu anaonyesha kwetu matumizi ya silaha za Mungu: habari njema ya ukweli kumhusu Mungu ("mkiwa mmejifunga kweli kiunoni"), utimizaji wake wa uaminifu wa agano ("dirii ya haki kifuani"), ujumbe wa upatanisho kwa Baba yetu wa mbinguni ("Injili ya amani"), hakikisho la uaminifu wa Mungu ("ngao ya imani"), na ahadi ya uzima wa milele kwa wale ambao wako huru kutoka kwa utumwa wa Shetani na uongo wake ("chapeo ya wokovu"). Tunahimizwa pia tuchukue silaha ile ile ambayo Yesu alitumia – Neno la Mungu ("upanga wa Roho").

> Wapendwa, msilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu, maana imeandikwa: "Kisasi ni juu Yangu, Mimi nitalipa, asema Bwana." Badala yake: "adui yako akiwa na njaa, mpe chakula, akiwa na kiu, mnyweshe. Maana ukifanya hivyo, utampalia makaa ya moto yanayowaka kichwani pake. Usishindwe na ubaya, bali uushindeni ubaya kwa wema. (Rom. 12:19–21)

Kisasi cha Mungu ni nini? Huyashinda maovu kwa mema, na anawakaribisha wana wake kufanya vile vile. Kuwahudumia

adui zetu kwa ukarimu badala ya kulipiza kisasi kunafananishwa na kuweka “kaa la moto” vichwani mwao. Kulipiza kisasi dhidi ya adui ni kushindwa na uovu. Hata hivyo, kuna njia ya kushinda uovu kikamilifu – “kwa wema.” Hiyo ndio njia ya Mungu ya kufanya vita.

Yesu akasema, “Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo!” Wakagawana nguo Zake kwa kupiga kura. (Luka 23:34)

Maneno haya ya Yesu ni kwa manufaa yetu. Baba hahitaji ushawishi wowote ili kusamehe. Tatizo haliko kwa Mungu, bali kwetu. Tunafikiria kwamba Mungu ni kama sisi. Yesu aliponena maneno, “Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo,” hakuwa akizungumza kwa niaba ya wale waliomsulubisha tu; alikuwa akizungumza kwa niaba yetu pia. Mungu anataka tufahamu kwamba anaelewa tatizo letu (hatujui tulitendalo); angali anatupenda bila mipaka na anatenda kazi bila kuchoka ili kutuokoa.

*Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, 23upole, kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria.*

*—Wagalatia 5:22-23*

# 15

# Sodoma and Gomora

Kuangamizwa kwa Sodoma na Gomora kuna dhaniwa kuwa mfano wa jadi wa Mungu mwenye hasira akinyesha mauti na maangamizi juu ya watu waovu. Tukichukua kisa hicho jinsi kilivyo katika Bibilia, kinachoonekana kutendeka ni kama ifuatavyo: Miji hiyo miwili inapatikana katika eneo ambalo linanawili katika kilimo na biashara, na maisha yanakuwa rahisi kabisa kwa wenyeji. Watu wana mpango mzuri wa wakati wa burudani na shughuli zisizo za Kiungu zikawa za kawaida katika maeneo hayo. Mungu anatazama kutoka mbinguni na anakasirishwa na kuenea kwa uovu wao. Anasita kuchukua hatua yoyote kwa muda, lakini hatimaye uasi unakuwa mbaya zaidi kiasi ya kwamba uvumilivu wa Mungu unaisha. Anatuma onyo kwa Loti mwenye haki na familia yake kuondoka kutoka Sodoma. Kisha, kwa onyesho la kuvutia la ghadhabu, Mungu ananyesha moto na kibiriti kutoka mbinguni. Waume, wake, na watoto wanakumbana na mauti ya kutisha. Sodoma na Gomora inaangamia, na kisasi cha Mungu kinaridhishwa.

Sasa, wacha tuchukue mtazamo mwingine kwa jambo hili hili kwa ufahamu kwamba Mungu hachukui jukumu la utendaji katika uangamizi. Chukua taswira ya miji hiyo miwili na wenyeji wake wakijihudumia binafsi, wakifurahia mafanikio yao na kwa raha: "Tazama, uovu wa umbu lako, Sodoma, ulikuwa huu; kiburi, na kushiba chakula, na kufanikiwa, hayo yalikuwa ndani yake na binti zake; tena hakuutia nguvu mkono wa maskini na mhitaji." (Ezek. 16:49). Watu hawafahamu kwamba chini ya miji yao (ambayo imejengwa katika maeno ya kijiolojia yasiyoimara) nguvu za volkano zinajengeka. Hawafahamu pia kuwa Mungu asiyeonekana, ambaye wanamkana, bado ni Mungu yule yule ambaye hadi wakati huo, amewakinga dhidi ya janga. Hatimaye

siku inafika ambayo Mungu lazima atambue haja yao ya kuwa huru kutoka kwake. Ili kukumbatia uhuru wao, anawaachilia bila kutaka, na kuwaacha bila kinga dhidi ya nguvu za maumbile bila udhibiti wake. Ufa ulio chini ya uso wa nchi unapasuka na kurusha miamba iliyoyeyuka maili maelfu na kunyesha chini "kiberiti na moto toka mbinguni kwa Bwana" (Mwan. 19:24*)*, ukiangamiza Sodoma na Gomora kwa dakika.

Tendo la Mungu la kuangamiza miji hiyo miwili ni kuwapa uhuru wa kweli – ukiwemo uhuru wa kufanya uchaguzi na matokeo ya janga: "Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako; kumpenda Bwana, Mungu wako, kuitii sauti yake, na kushikamana naye; kwani hiyo ndiyo uzima wako, na wingi wa siku zako" (Kumb. 30:19–20).

Magonjwa, ajali, vifo, vita, majanga ya kiasili, na mambo kama hayo yanatokea kwa sababu nyingi. Mara nyingi tunahusika moja kwa moja, wakati mwingine ni Shetani, na wakati mwingine nguvu za maumbile ni za kulaumiwa. Mara nyingi baadhi ya mwingiliano wa visababishi unahusika. Kwa sababu hatuwezi ona kwa uwazi mbona tukio fulani la kuteseka lilitendeka, tunamwelekezea Mungu lawama kwa hilo. Hilo ni haki? Hilo ni la busara? Tabia yetu ya kumgeuzia Mungu lawama imekuwepo kwa muda mrefu. Ni lini na wapi ndio ukwepaji huu wa majukumu ulianza? "Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. Bwana Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala." (Mwa. 3:12–13, mkazo umetiliwa).

Ee Bwana, fadhili zako zafika hata mbinguni, Uaminifu wako hata mawinguni. Haki yako ni kama milima ya Mungu, Hukumu zako ni vilindi vikuu, Ee Bwana, unawaokoa wanadamu na wanyama. Ee Mungu, jinsi zilivyo na thamani fadhili zako! Wanadamu huukimbilia uvuli wa mbawa zako.

—Zaburi 36:5–7

# 16

## Vipi Kuhusu Gharika?

Vipi kuhusu gharika ya siku ya Nuhu? Kama Mungu sio mwangamizi, nini kilitendeka na kuuletea ulimwengu wetu maafa makuu? Ni ushahidi upi tunaweza pata katika Bibilia na mahali kwingine kupata maelezo yenye mantiki ya kile kilichosababisha gharika hii kubwa ulimwenguni kote?

> Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini. (Mwan. 6:3)

Mungu inavyoonekana alikuwa akitazamia wakati ambao jamii ya mwanadamu ingejitenga mbali zaidi naye kwamba angelazimika kuwaacha waende kwa kudhoofisha nguvu zake za kuzuia na kushikilia nguvu za maumbile. Tunaweza shangaa kilichosababisha awaachilie. Mungu alipiga hesabu katika uamuzi wake wa kufanya hivyo, ama sababu nyingi ilihusika?

Fikiria una jirani ambaye ana matatizo kadhaa. Shida za kifedha, matatizo ya afya, na Pia hawezi kutembea mbali na nyumbani. Na zaidi ya hayo, hana gari lake, na kuifanya kuwa vigumu kwake kusafiri na kuafikia mahitaji yake.

Siku moja, katika mazungumzo naye, unagundua ukosefu wake wa usafiri na unajitolea kumsafirisha hadi sokoni na sehemu zingine. Kwa miezi michache unamsafirisha kwa gari lako kwenda kwa teuzi za daktari, maduka ya dawa na maduka makubwa. Mipango inaonekana kwenda sambamba, na unafurahia kumsaidia.

Kisha asubuhi moja tulivu jirani huyu huyu anajitokeza mlangoni pako kwa kile kinaonekana kama mchafuko wa

mawazo na anakuagiza umsafirishe kwa benki iliyoko mjini. Unagundua kuwa amebeba mkoba wa karatasi, kinyago, na kile kinachoonekana kama bunduki kikifungwa kwenye begi. Utafanya aje? Utachukua funguo za gari na kwa tabasamu kukimbia kwenye gari ili kumsafirisha rafiki yako kwenda kwenye hatima ya safari yake na kumrejesha?

Sisi sote tuna mipaka ambayo hatuko tayari kuivuka. Mipaka hii inahusisha maadili, nidhamu na mipaka ya mambo ya kibinafsi. Sio jambo lenye mantiki kuamini kuwa Mungu Pia ana mipaka ambayo hataivuka—au hawezi?

> Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote. Dunia ikaharibika mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma. Mungu akaiona dunia, na tazama, imeharibika; maana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani. Mungu akamwambia Nuhu, Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia. (Mwan. 6:5, 11–13)

Ulimwengu wetu ulikuwa jinsi gani kabla ya gharika? Mungu alimdhihirishia Nuhu, “*wameijaza* dunia dhuluma” (v 13, mkazo umetiliwa). Kwa sababu ya dhuluma ya wanadamu, dunia yenyewe ilikuwa *ikihifadhi* dhuluma. Nguvu kupita kiasi za dhuluma zilikuwa zijionyeshe upesi katika maafa yajayo. Jamii ya mwanadamu ilikuwa imepotoka kimaadili: “Mungu akaiona dunia, na tazama, imeharibika; maana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani.”

Ni wafuasi wangapi waaminifu ambao Mungu alikuwa nao katika wakati huu wa giza katika historia? Nuhu pekee ametajwa katika Bibilia. Ni nini ambacho kilileta hali hii ya

kuhuzunisha ya mambo? Mawazo ya binadamu yalikuwa "baya tu sikuzote." Bibilia inaelezea aje uovu? Adamu na Hawa walipokula tunda la "mti wa ujuzi wa mema na mabaya" (Mwanz. 2:17), mabadiriko yao ya mawzo kuhusu wema wa Mungu yanaelezea kikamilifu *uovu ni nini*. Sura ya Mungu wetu iliyoumbukwa na wazazi wetu wa kwanza ndio ulimwengu ulirithi. Wenyeji katili wa kabla ya gharika walifikiria kuwa Mungu alikubali dhuluma yao. Majibu yake yalikuwa yapi? "Akahuzunika moyo" (Mwan. 6:6).

Wanadamu walikuwa wamemsukuma Mungu katika mpaka ambao *hangeweza* kuuvuka pasipo kuwa mhusika wa kulazimishwa katika dhuluma yeye mwenyewe. Mungu alikuwa ameshurutishwa kulegeza ushikiliaje wake wa nguvu za maumbile. Wakati kipindi cha miaka 120 kilikamilika, na wasafiri walikuwa salama katika safina, mvua ilianza kunyesha, ikimwaga mito kwa siku arobaini usiku na mchana. Nini kilisababisha mvua hii kubwa? Tunapata vidokezo muhimu katika sura ya kwanza ya Mwanzo:

> Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji. Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo. Mungu akaliita lile anga Mbingu. (Mwan. 1:6–8)

Anga ni nini? Anga linamaanisha kuba. Kuba linarejelea kifunika juu ya dunia kikiniginizwa au kuwekwa katika mbingu au anga. Fungu linaendelea kuelezea kuba hili linatenganisha maji, na kiasi muhimu cha maji *juu* ya kuba hili.

Kifuniku kikubwa cha mvuke wa maji ya anga kilizunguka dunia yote kama chafu kubwa ikiupa ulimwengu wetu hali ya hewa sawasawa na tamu ya kitropiki kwanzia ncha ya kaskazini hadi ncha ya kusini. Mabaki ya mimea na wanyama wa hali ya

hewa ya joto yamepatikana katika maeneo haya yakitoa ushahidi kuwa hali ya hewa kama hiyo ilikuwepo katika sayari yetu wakati fulani. Bibilia pia inatupa kidokezo kingine muhimu kuhusu hali ya hewa ya dunia katika siku hizo za awali:

> Hivyo ndivyo vizazi vya mbingu na nchi zilipoumbwa. Siku ile Bwana Mungu alipoziumba mbingu na nchi hapakuwa na mche wa kondeni bado, wala mboga ya kondeni haijachipuka bado, kwa maana Bwana Mungu hajainyeshea nchi mvua, wala hapana mtu wa kuilima ardhi; ukungu ukapanda katika nchi, ukatia maji juu ya uso wote wa ardhi. (Mwan. 2:4–6)

Mafungu haya yanapendekeza ulimwengu tofauti kabisa na ule ambao tunafahamu leo. "Bwana Mungu hajainyeshea nchi mvua … Lakini ukungu ukapanda katika nchi, ukatia maji juu ya uso wote wa ardhi." Nchi ilikuwa na unyevu lakini ilikuwa joto na hali ya hewa ya kipekee, bila joto kugeuka ghafla. Na joto sawa kama hiyo hakungekuwa na radi, hakuna chemchela, hakuna tufani, hakuna mvua ya mawe, wala theluji, na inavyoonekana hakukuwa hata mvua. Na pia inaonekana kuwa uso wa nchi yenyewe ulikuwa tambarare kuliko ulivyo leo, bila minara ya milima au korongo kuu za vina virefu vya bahari. Kwa kuongezea, sehemu ndogo sana ya uso wa nchi ilifunikwa na maji.

Ni nini kiliyaweka maji kati hali ya kuniginia katika anga, na ni utaratibu upi uliyosababisha mvua kuanza? Tunajua kutoka kwa mtazamo rahisi kuwa joto husababisha maji kupanda. Maji yaliyochemshwa kwenye birika juu ya jiko hutoweka kama uvukizi. Sehemu za maji katika sayari yetu hutoa chembechembe nyingi za maji kila siku. Kadri joto linavyongezeka, ndivyo kasi ya kutoweka kwa maji inazidi. Kiasi kidogo cha chembechembe za maji hutoweka kutoka kwenye

uso wa ziwa lililohifadhiwa katika majira ya baridi ikilinganishwa na majira ya joto.

Na kama kungekuwa na joto jingi kabla ya gharika; si hilo lingesababisha maji mengi kwenye anga? Nchi yetu hupata joto yake karibu yote kutoka kwenye jua letu. Bila hilo ulimwengu wetu utakuwa umeganda na joto ya uso wake ikikaribia sifuri.

Mungu alipoumba ulimwengu wetu, aliweka kazini mfumo wa wazi wa kustajabisha wa joto unaoweza kuniginiza viwango vikubwa vya maji katika anga. Jua lingeweza kuwa mtambo muhimu katika utenda kazi wa mfumo huu. Pia ni mantiki kuamini kuwa jua kabla ya gharika lilitoa joto *jingi zaidi* kuliko litoavyo leo. Kama hili ni kweli, basi kuna mantiki kuamini kuwa wakati Mungu alishurutishwa kuregeza uhifadhi wake wa ulimwengu halisi utoaji wa nguvu wa jua ungeathiriwa.

Usawazishaji laini katika anga ulivurugika, na "Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi, siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka. Mvua ikanyesha juu ya nchi, siku arobaini mchana na usiku." (Mwan. 7:11–12). Mvua ya kwanza ya historia ilianza kunyesha, hatimaye ikimwaga maelfu ya mile ya ujazo wa maji juu ya nchi.

Ukosefu wa utulivu wa kijiolojia ulisadifiana na ukosefu wa utulivu wa anga na kusababisha ongezeko la msukumo wa maji katika hifadhi za ardhini: "siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu" (Mwan. 7:11). Hizi "chemchemi" zilichangia maji zaidi ya mafuriko.

Watu nane pekee katika safina walihifadhiwa kutoka kwenye gharika: Nuhu na familia yake. Aina mbalimbali za wanyama pia waliabiri meli hiyo kubwa kwa kusudi la kuongeza idadi ulimwenguni na kila aina ya mnyama baada ya gharika.

Mabaki ya safina yamehifadhiwa katika hifadhi ya kitaifa ambayo ni ari kwa tovuti ya safina katika Uturuki Mashariki, karibu na mji mdogo wa Dogubayazit. Ugunduzi huu wa

kustajabisha wa akiolojia, katika milima ya Ararati, ni ushahidi wa kusurutisha kuwa kisa cha Bibilia kuhusu gharika kuu *sio* hadithi ya kujitungia, lakini ni historia ya kuaminika ya janga pekee la kiasili ulimwenguni kote:

> *Maji yakadumu kuondoka katika nchi; na mwisho wa siku mia na hamsini maji yakapunguka. Mwezi wa saba, siku ya kumi na saba ya mwezi, safina ikatua juu ya milima ya Ararati.*
>
> —Mwanzo 8:3–4

# 17

# Ushuhuda wa Msalaba

Kwa ufahamu sahihi wa matendo ya Mungu katika Agano la Kale, tunahakikishiwa kuwa huwa haangamizi—pasipo kuzingatia hali. Hata hivyo, ushahidi wa kusurutisha zaidi kuwa Mungu hamkaribii mtu muovo ili kumuangamiza unapatikana katika Agano Jipya.

Imani kuwa Yesu alikufa kwa ajili yetu ni karibu kwa watu wote ambao ni wanafunzi wa Bibilia, ingawaje kuna mitazamo tofauti ya jinsi kifo cha Yesu kinatuokoa. Hata hivyo, wengi wanaamini kwamba wakati Yesu alikufa msalabani, alipitia yale ambayo tumewekewa kupitia pasipokuwa na kujitolea kwake nafsi kuingilia kati kwa niaba yetu.

Kama hili ni kweli, basi tutatarajia kupata kwamba Yesu alikufa njia sawa na ile ambayo tutakufa kwa uhusiano na kile ambacho Mungu "hufanya" ili kuleta mauti. Kama tunaamini kuwa ni Mungu ambaye humwangamiza mdhambi, basi pia tutatarajia kuwa Mungu Baba alimkaribia Yesu ili kumuua. Hiki ndicho tunapata? Injili ya Mathayo inatupa kisa cha kina kuhusu kusulubishwa kwa Yesu. Maneno ya mwisho ya Yesu yalikuwa yapi muda mchache kabla ya kifo chake? "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?'' (Matt. 27:46, mkazo umetiliwa).

Fungu hili linadhihirisha jinsi Yesu alikufa. Mungu Baba aliruhusu Mwanawe kuyapitia yale ambayo kila mtu ambaye anakataa upendo wake atayapitia mwishowe—kujitenga kutoka kwake, mpaji wa uzima. Mungu Baba hakumuua Yesu—dhambi zetu zilimuua: "Mshahara wa dhambi ni mauti" (Rom. 6:23). Dhambi inaweza sababisha kifo kikamilifu yenyewe, bila usaidizi wowote kutoka kwa Mungu. Uzima wote hutoka kwa Mungu bila kubagua. Mauti yote ni tokea la dhambi bila

kubagua. Kufikiria kuwa Mungu ni chanzo cha maiti ni kukosa mantiki—bila kubagua.

Haiwezekani katika tambo hili ndogo kuchunguza kila kisa cha uangamizi na mateso ambayo yanawekewa Mungu. Hata hivyo, kisa ambacho tumechunguza ni muhimu katika ufahamu sahihi wa jukumu la Mungu katika mauti na maafa katika Bibilia. Bibilia inaelezea Bibilia. Wakati Bibilia inavuta pazia katika kifungu fulani ili kuweka wazi matendo ya Mungu ni yapi, tunaweza tumia hilo kama kigezo cha kufahamu mafungu mengine ambayo sio wazi (kama wakati mafungu mawili ya Bibilia yanaonekana kukinzana). Kwa kuongezea, maneno ya Mungu kujihusu yeye Mwenyewe ni yenye thamani ya kipekee kuzingatiwa, kwa mfano: "Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu" (Mal. 3:6). Hatimaye, ukweli kumhusu Mungu, ambao Yesu alifunza na kuonyesha, ni ramani sahihi ya njia ya usomaji wa Bibilia nzima Kwanzia Mwanzo hadi Ufunuo.

*Ili kwamba, Kristo apate kukaa mioyoni mwenu kwa njia ya imani. Nami ninaomba kwamba ninyi mkiwa wenye mizizi tena imara katika upendo, 18mwe na uwezo wa kufahamu pamoja na watakatifu jinsi ulivyo upana na urefu na kimo na kina upendo wa Kristo na kujua upendo huu kwamba unapita fahamu, ili mpate kujazwa na kufikia kipimo cha ukamilifu wa Mungu..*

*—Waefeso 3:17–19*

# 18

## Mungu Sio Mtawala Jeuri

Kuna habari njema kwa kila mmoja ambaye amehusiana na mafundisho ya kuchomeka jehanamu milele. Mafundisho haya hayaungwi mkono na utafiti wa kina wa Bibilia. Maandiko yanaelezea kifo kama hali ya kuzirai. Ni *usingizi* wa muda tu ambao utadumu hadi ufufuo. Baada ya wakati huo, wale ambao wamepinga maridhiano na Mungu watavuna, kama tokeo halisi, kupotea milele.

Kupata ungwaji mkono wa mahali pa kuchomeka milele kwa adhabu katika Bibilia, lazima tufanye hivyo kwa kuyachukulie kwa uhalisia maneno ambayo yametumika kimfano. Neno moto linaweza kuwa na maana halisi au ya mfano. Katika kitabu cha Danieli, wakati Nebukadreza aliagiza Shadraka, Meshaki, and Abednego watupwe kwenye tanuru ya moto, ni dhahiri kuwa ni moto halisi ambao walishuhudia. Wakati Yohana mbatizaji, ambaye alibatiza kwa maji, alisema kuwa Yesu angebatiza kwa Roho Mtakatifu na moto, ni dhahiri kuwa hakuwa akirejelea moto halisi, bali alikuwa akitumia neno *moto* kimfano.

""Mungu wetu ni moto ulao," na "Mungu ni Upendo" (Ebr. 12:29, 1 Yohana 4:16). Je, kauli hizi mbili elezi kumhusu Mungu zinakinzana? Kama tu tutafikiria moto kama moto halisi. Moto ni mwitikio wa kemikali. Mungu ni mwitikio wa kemikali? Kauli hizi ziko katika uiano mkamilifu kama tutafahamu athari ya upendo wa Mungu kwa Mtu. Upendo wa Mungu huteketeza ubinafsi. Ubinafsi ni kinyume cha upendo wa kweli. Kama tuko wazi kwa upendo wa Mungu, upendo huo huo utakuja ndani yetu na kuteketeza ubinafsi wa kuangamiza mioyoni mwetu. Hili ni tukio litoalo uzima.

Iwapo tutapinga upendo wa Mungu, na badala yake kukumbatia ubinafsi wetu, upendo huo huo utakuwa chanzo cha adhabu. Tutajaribu kuuondokea na hata kukimbia au kujificha kutoka kwa Mungu. Hilo ndilo Adamu na Hawa walilopitia baada ya kuamini uongo wa nyoka kumhusu Mungu. Ifahamike kwa njia hii, tunaweza ona upendo wa Mungu kama moto ulao.

Mfano wa Yesu wa tajiri na Lazaro wakati mwingine unatumika kutetea mafundisho ya mahali halisi pa mateso:

> Palikuwa na mtu mmoja tajiri aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, ambaye aliishi kwa anasa, kila siku. Hapo penye mlango wake aliishi maskini mmoja, jina lake Lazaro, mwenye vidonda mwili mzima. Huyo Lazaro alitamani kujishibisha kwa makombo yaliyoanguka kutoka mezani kwa yule tajiri. Hata mbwa walikuwa wakija na kulamba vidonda vyake. Wakati ukafika yule maskini akafa, nao malaika wakamchukua akae pamoja na Abrahamu. Yule tajiri naye akafa na akazikwa. Kule kuzimu alipokuwa akiteseka, alitazama juu, akamwona Abrahamu kwa mbali, naye Lazaro alikuwa karibu yake. Hivyo yule tajiri akamwita, Baba Abrahamu, nihurumie na umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake ndani ya maji aupoze ulimi wangu, kwa sababu nina maumivu makuu kwenye moto huu. Lakini Abrahamu akamjibu, Mwanangu, kumbuka kwamba wakati wa uhai wako ulipata mambo mazuri, lakini Lazaro alipata mambo mabaya. Lakini sasa anafarijiwa hapa na wewe uko katika maumivu makuu. Zaidi ya hayo kati yetu na ninyi huko, kumewekwa shimo kubwa, ili wale wanaotaka kutoka huku kuja huko wasiweze, wala mtu ye yote asiweze kuvuka kutoka huko kuja kwetu. Akasema, Basi, nakuomba, umtume

> Lazaro aende nyumbani kwa baba yangu, maana ninao ndugu watano. Awaonye, ili wasije nao wakafika mahali hapa pa mateso. Abrahamu akamjibu, Ndugu zako wana Mose na Manabii, wawasikilize hao. Yule tajiri akasema, Hapana, baba Abrahamu, lakini mtu kutoka kwa wafu akiwaendea, watatubu. Abrahamu akamwambia, Kama wasipowasikiliza Mose na manabii, hawataweza kushawishiwa hata kama atafufuka mtu kutoka kwa wafu. (Luka 16:19–31)

Yesu alitoa mfano huu ili kuonyesha athari za ubinafsi na kutofautiana kwa mtu. Yesu alikuwa akiwazungumzia Mafarisayo ambao walijiona kuwa wakamilifu, na aliukita mfano wake katika imani potofu ya kawaida ambayo watu wanashikilia ya maisha ya baada ya kifo.

Wayahudi walihusisha utajiri na mibaraka ya Mungu. Mawazoni mwao mtu masikini, hasa yule ambaye aliteseka kimwili, alilaaniwa na Mungu; wazo likiwa kwamba mtu huyo alistahili sehemu hiyo katika maisha kwa sababu ya upungufu fulani wa kiroho au dhambi. Mtu tajiri, kwa upande mwingine, alikuwa na hakikisho la upendeleo wa kipekee kutoka kwa Mungu. Utajiri wa mtu au hali ilikuwa, kwa namna ya kuwaza kwa Mafarisayo, kipimo cha ukamilifu wao mbele za Mungu. Yesu aliwapa mfano huu ili kuweka wazi imani yao isiyo ya kweli ya mtazamo huu mwembamba na katili.

Mwanzo tutaangalia maelezo madogo ya kisa. Baada ya kifo chake, Lazaro, mwombaji, anajipata akistareheshwa "mapajani mwa Abrahamu." Tajiri naye anakufa na anaelekea jehanamu akiyapitia mateso; anatazama juu na kumuona Abrahamu na Lazaro kwa umbali. Mazungumzo kisha yanafuata kati ya tajiri na "Baba Abrahamu"

Sasa wacha tuchunguze kisa hiki kwa makini kwa kuuliza maswali yenye mantiki:

- Abraham na Lazaro wamewekwa wapi katika kisa hiki?
- Kama Abrahamu na Lazaro wako mbinguni au paradiso, inawezekanaje Abrahamu kuwa na mazungumzo na tajiri ambaye yuko jehanamu, na inawezekanaje kwa tajiri kuwaona?
- Kama Abrahamu na Lazaro wako jehanamu, wanafanya nini huko?
- Kama Abrahamu na Lazaro hawako mbinguni wala jehanamu, wako wapi?
- Ni uchungu kiasi gani utatulizwa na matone machache ya maji kwenye ulimi kwa mtu ambaye anateseka katika moto wa jehanamu?
- Lazaro anaweza muona tajiri akiteseka jehanamu na asikie ombi Lake?
- Ni jinsi gani Lazaro anastareheseshwa mapajani mwa Abrahamu?
- Lazaro anastareheseshwa *licha ya* ufahamu wake dhahiri wa kuteseka kwa tajiri au *kwa sababu* yake?
- Je, Lazaro anahimizwa kuendeleza tofauti yao sugu kwa tajiri sasa kwa kuwa hali zao zimegeuzwa?
- Ni upana kiasi gani wa "shimo kubwa" ambao unazuia usafiri kati ya maeneo hayo mawili?
- Ni upana kiasi gani ambao shimo hili kubwa lingehitaji ili kuzuia mawasiliano kati ya jehanamu na eneo la Abrahamu na Lazaro?
- Ni upana gani ambao shimo hili kubwa lingehitaji ili kuzuia ufahamu wa mateso ya wale ambao wanateswa katoka jehanamu na wale ambao wako kwenye upande wa starehe wa shimo? Yadi mia tatu? Maili mia tatu? Ulimwengu unaweza kuwa mpana kiasi cha kutosha?

- Je, kuna mantiki kuhitimisha kuwa kwa sababu Yesu alitumia marejeleo ya jehanamu katika mfano wa tajiri na Lazaro kuwa alikuwa akiunga mkono mafundisho ya kuchomeka milele katika jehanamu?

Haiyonekani kuwa yenye mantiki zaidi kuhitimisha kuwa Yesu alileta dhana hii ya mahali pa kuchomeka milele katika mfano wake ili kuondoa mafundisho haya ya huyawani badala ya kuyaidhinisha? Yesu alikuwa akifundisha kuwa haiwezekani kwa wale ambao wataishi milele kuwa na amani kamilifu na furaha ya kweli kama kungekuwa na jehanamu ya kweli katika ulimwengu.

Mafundisho kuwa kuna mahali pa kuteseka milele ni uongo wa Shetani ambao anamwekea Mungu wetu mpole, mwingi wa rehema, mwenye kusamehe, na mwenye upendo kama mtawala jeuri unayeweza fikiria na hesabu yake ya kutuondoa kwenye Baba yetu wa Mbinguni. Hakutakuwa *daima* na mahali pa kuteseka milele. Bibilia inazungumza badala yake, siku ambayo inakuja ambapo mateso yote yatakoma —milele:

> Nami nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, makao ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atakaa pamoja nao. Yeye atakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita. (Ufu. 21:3–4)

Wengi mara nyingi hushangaa ni katika umbo gani tutaishi milele. Tutakuwa na miili ya binadamu kama tuliyonaya sasa, au tutaishi katika uwepo bila miili? Na, nafsi yetu *ni* nini?

> Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai. (Mwan. 2:7)

> Roho ile itendayo dhambi itakufa. (Ezek. 18:4)

Maisha yetu yanahitaji "pumzi ya uhai," au roho, ambayo inatoka kwa Mungu. Hatuna nafsi hai. Kila mmoja wetu *ni* nafsi hai. Imani kuwa tuko na nafsi isiyokufa ambayo haiwezi tenganishwa haiungwi mkono na Bibilia. Katika marejeo ya pili ya Yesu Kristo miili yetu isiyokamilifu itabadilishwa "ghafla, kufumba na kufumbua" (1 Kor. 15:52) kwa ukamilifu.

> Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti. (Rom. 6:23)

Hakuna popote katika neno la Mungu ambapo kifo kimeelezewa kama kitu tofauti kuliko kifo. Maandiko yote, yakifahamika kwa usahihi, yanathibitisha kuwa *dhambi hupelekea kifo* na kuna sauti moja tu pinzani: "*Nyoka akamwambia* mwanamke, *Hakika hamtakufa*" (Mwan. 3:4, mkazo umetiliwa).

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. (Yohana 3:16)

Neno *kupotea* humaanisha kuwa katika hali ya kutokuwepo. Halimaanishi kuwepo mahali pengine katika hali ya kuteseka.

> Baada ya kusema haya, Yesu akawaambia, Rafiki yetu *Lazaro amelala*, lakini nakwenda kumwamsha. Wanafunzi wakamwambia, Bwana, kama amelala

> usingizi ataamka. Hata hivyo, Yesu alikuwa anazungumzia kuwa Lazaro amekufa, lakini wanafunzi wake hawakuelewa, walidhani kwamba anasema Lazaro amelala usingizi tu. Kwa hiyo Yesu akawaambia waziwazi, *Lazaro amekufa* (Yohana 11:11–14, mkazo umetiliwa)

Yesu alifananisha kifo na usingizi kwa sababu Mungu ana uwezo wa kumfufua mtu kutoka kwenye mauti. Yesu alipomfufua Lazaro baada ya siku nne kaburini, Lazaro hakuitwa kutoka Mbinguni. Aliamka kutoka katika hali ya kuzirai—kifo.

> Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, Siku hiyo mawazo yake yapotea. (Zab. 146:4)

> Katika kifo mawazo hayaendelei mahali pengine.

> Maana mautini hapana kumbukumbu lako; Katika kuzimu ni nani atakayekushukuru? (Zab. 6:5)

> kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. (Muhubiri. 9:5)

Tunapokufa shughuli zote za utambuzi hukoma wakati huo huo, ikiwemo ufahamu wowote wa wakati uliopita. Wakati wa ufufuo utaonekana kuja mara moja baada ya kupumua pumzi ya mwisho.

> Kwa maana Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni, akitoa amri kwa sauti kuu pamoja na sauti ya

> malaika mkuu na sauti ya tarumbeta ya Mungu, nao wale waliolala mauti wakiwa wanamwamini Kristo watafufuka kwanza. (1 Thess. 4:16)

Ufufuo huu utatendeka wakati wa marejeo ya Yesu mara ya pili.

> Tazama, naja upesi! nikiwa na mshahara wangu. (Ufunuo. 22:12)

Hatutapokea mshahara wetu wa milele *hadi* Yesu arejee mara ya pili.

> Aliye peke yake Mtawala, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Yeye peke yake hapatikani na mauti. (1 Tim. 6:15–16)

> Mungu pekee hapatwi na mauti. Sio sisi.

> Sikilizeni, nawaambia siri: Sote hatutalala, lakini sote tutabadilishwa ghafla, kufumba na kufumbua, parapanda ya mwisho itakapolia. Kwa kuwa parapanda italia, nao wafu watafufuliwa na miili isiyoharibika, nasi tutabadilishwa. Kwa maana mwili huu wa kuharibika lazima uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa lazima uvae kutokufa. Kwa hiyo, mwili huu wa kuharibika utakapovaa kutokuharibika, nao huu mwili wa kufa utakapovaa kutokufa, ndipo lile neno lililoandikwa litakapotimia: Mauti imemezwa kwa kushinda. (1 Kor. 15:51–54)

Hatuna udumu milele ndani yetu na wetu wenyewe. Kuishi milele kunawezekana *tu* kupitia kuunganishwa kwa Mungu:

"Huu mwili wa kufa utakapovaa kutokufa." Paulo pia anatangaza, "Sote hatutalala." Wale ambao watakuwa hai, katika Kristo, wakati wa marejeo ya pili hawatashuhudia kifo.

> Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi; ndama na mwana-simba na kinono watakuwa pamoja, na mtoto mdogo atawaongoza. Ng'ombe na dubu watalisha pamoja; watoto wao watalala pamoja; na simba atakula majani kama ng'ombe. Na mtoto anyonyaye atacheza penye tundu la nyoka, na mtoto aliyeachishwa atatia mkono wake katika pango la fira. Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua Bwana, kama vile maji yanavyoifunika bahari. (Isa. 11:6–9)

Katika nchi iliyofanywa upya uumbaji wote wa Mungu utarejeshwa katika ukamilifu wake wa asili wa Edeni. Wanyama hawatawaua wengine ili kuishi, na hakuna viumbe ambao watawatisha wanadamu. Hakutakuwa na hofu, wala mateso, wala mauti.

> *Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita.*
>
> *—Ufunuo 21:4*

# 19

# Muumbaji na Mpaji Wetu

Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.
—Mwanzo 1:1

Hapa ndipo penye msingi wa sayansi zote za kweli. Mungu aliuumba ulimwengu wetu. Mungu alituumba. Sisi sio tokeo la kubahatisha. Kuna kusudi takatifu kwa uwepo wetu. Hata hivyo, ulimwengu wetu leo umejazwa falsafa ambayo ni kinyume kwa kauli wazi ambayo inafungua Neno la Mungu. Walimwengu wamejaribu kuteka nyara sayansi katika lengo lake la kumuondoa Mungu. Falsafa hii imepelekea kuhodhi juu ya sayansi kwa zaidi ya karne.

Sio katika wigo la kitabu hiki kidogo kufikia mlengwa kwa kiasi kikubwa cha ushahidi wakuunga mkono sayansi yenye msingi wa uumbaji kama vile kuna vitabu vingi vizuri kuhusu mada hii. Hata hivyo, kuna vita ambavyo vinapiganwa leo kuhusu uwepo wa Mungu. Kuna waandishi maarufu na wanenaji ambao wanawafuasi wengi ambao wako katika huduma ya kumtupilia Mungu mbali. Ni nini kinachoendesha harakati hii, na mbona watu wengi wamekataa imani ya Mungu?

Watu wengi waaminifu wanaendelea kushikilia mtazamo potofu wa Mungu. Wengi wamekua wakisikia kuhusu upendo wa Mungu, na kupata tu sura ya Mungu mwenye upendo inayotofautiana kwa ufanisi na sura inyapingana ambayo inamuonyesha kama mungu ambaye anakasirika haraka. Ongeza kwa imani kuwa Mungu hulipiza kisasi dhidi ya adui zake kwa kupanga kifo, uangamizi na mateso ya milele; ni rahisi kuona mbona watu wengi wamepinga imani ya Mungu kwa jumla. Lakini pengine wale ambao wanapinga imani ya mungu wakati sura hii iliyoumbukwa ndiyo tu wanajua hawampingi

Mungu kabisa. Swali la pili la uwepo wa Mungu linapatikana tu kwa sababu swali la msingi kuhusu tabia ya Mungu halijatatuliwa kwa kila mawazo.

> Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana. (Mwan. 1:31)

Fungu hili linahitimisha kisa cha uumbaji. Mungu hangeona kila kitu duniani kama "chema sana" kama kungekuwa na kifo cha kiumbe chake chochote kabla ya kukamilika kwa kazi yake ya uumbaji. Kwa vile Mungu sio mwanzilishi wa mateso na kifo, hili linaondoa njia ya mwenye nguvu mpishe ya uwepo kabla ya anguko la mwanadamu wakati mateso na kifo kiliingia ulimwenguni mara ya kwanza.

Mtindo wa maisha wa mwenye nguvu mpishe ambao tunaona katika ulimwengu wetu leo ni pokeo la kikatili kwa ulimwengu ambalo limekuwa katika kuibuka kwa mbinu ya kuishi tangia kuingia kwa dhambi. Kuna habari njema! Ukengeufu wa viumbe kutoka kwa Muumba ambao ulitendeka katika anguko utaponywa katika nchi itakayofanywa upya. Sheria ya upendo kisha itakuwa jinsi ya maisha bila ushindani, hakuna hofu, wala mateso na wala kifo hakitakuwepo. Kusudi asilia la Mungu kwa ulimwengu wetu kisha litatambulika.

> Kwa maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu, asili ya Mungu asiyeonekana kwa macho, yaani, uwezo Wake wa milele na asili Yake ya Uungu, umeonekana waziwazi ukitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya ili wanadamu wasiwe na udhuru. (Rom. 1:20)

Wakati tumepata fursa ya kujifunza sayansi, tutathamini usahihi wa miujiza na utata unaoonekana katiaka uumbaji. Sahihi ya Mungu imeandikwa kila mahali. Tunapokataa uwepo

wa Mungu, ni lazima pia tukatae uwepo wa miujiza, lakini tunazungukwa na miujiza: miti mikubwa, maua laini ya msituni, nyimbo za ndege, utando wa buibui, ulimwengu mkubwa sana, tabasamu la mtoto anapomtambua mamake, pumzi unayopumua wakati huu. Hii yote ni miujiza ya hali ya juu. Haziwezi zikaelezewa kimantiki kama kitu kingine isipokuwa miujiza. Uzima wote *ni* miujiza. Ushahidi ni balaa kuwa Mungu alituumba sisi na kila kitu kingine ambacho kina uhai. Kuangalia ulimwengu wa kustajabisha unaotuzunguka na kuhitimisha kuwa Mungu hakuuumba ni jambo ambalo *halina* mantiki.

> Maana Bwana, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Mungu; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu; Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine. (Isa. 45:18)

Mungu aliumba dunia iwe nyumbani kwetu milele.

> Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Tangu mwanzo huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote viliumbwa kwa Yeye, wala pasipo Yeye hakuna cho chote kilichoumbwa ambacho kimeumbwaNeno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi takauona utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli. (Yohana 1:1–3, 14)

Muumbaji wetu alikuja akawa mmoja wetu ili kwa ukamilifu zaidi adhihirishe jinsi alivyo.

> Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako, Mwezi na nyota ulizoziratibisha; Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, Na binadamu hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu; Umemvika taji ya utukufu na heshima; Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; Umevitia vitu vyote chini ya miguu yake. (Zab. 8:3–6)

Jamii ya mwanadamu iliumbwa "chini kidogo kuliko malaika." Hata hivyo, wale ambao wameishi duniani na wameridhiana na Mungu watakuwa wameyapitia ambayo hata "malaika wanatamani kuyafahamu" (1 Peter 1:12). Maarifa yao ya uzoefu wa upendo wa kujikana nafsi wa Mungu utawapa nafasi ya kipekee ulimwenguni: "Nikaona Mji Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, ukiwa umeandaliwa kama bibi arusi aliyepambwa kwa ajili ya mumewe. Nami nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, makao ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atakaa pamoja nao. Yeye atakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao." (Ufu. 21:2–3)

> Ameiumba dunia kwa uweza wake, Ameuthibitisha ulimwengu kwa hekima yake, Na kwa ufahamu wake amezitandika mbingu. (Yer. 10:12)

> Kwa kuwa katika Yeye tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima wetu.
> (Matendo 17:28)

Ulimwengu, dunia, na viumbe vyote juu ya nchi hawadumu milele isipokuwa Mungu. Muumbaji wetu hakuinjeka nchi yetu, akauwekea upepo kama saa, Kisha akaiacha iiende kufanya kazi

kivyake bila usaidizi mwingine wowote. Mungu anaendelea "akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza" "na katika Yeye vitu vyote vinashikamana pamoja." (Ebr. 1:3; kol. 1:17).

Kama ulikuwa unashikilia glasi ya maji katika mkono wako wa kuume na ukaamua kuiangusha, utahitaji kutumia mkono wa kushoto kulazimisha mkono wa kuume kuiangusha? Mungu anatwambia, "Naam, mkono wangu umeuweka msingi wa dunia, na mkono wangu wa kuume umezitanda mbingu; niziitapo husimama pamoja" (Isa. 48:13).

Kufikiria kuwa Mungu ni mwangamizi hupuuzia nafasi yake kama mpaji wa uumbaji. Mungu hahitaji kuangamiza kikamilifu ili uharibifu utendeke. Kama kwa mfano, katika uharibifu wa Sodoma na Gomora, fasiri ya kawaida huona Mungu *akiumba* moto na kiberiti kwa kusudi la kuangamiza kile "anashikilia" au *kuhifadhi*. Sura hii ya Mungu kama mwangamizi inamweka katika pambano na nafsi yako kama ulitumia mkono wako wa kushoto kulazimisha mkono wa kuume kuangusha glasi ya maji.

Kwa Mungu kuangamiza anahitaji tu kuachilia. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa hufanya hata hili akiwa na mapenzi ya mauti au maangamizo yatendeke. Mungu huachilia tu kwa sababu yeye ni upendo, na upendo huhitaji uhuru wa kweli. Mungu humwachilia mtu au taifa tu bila kutaka na kwa uchungu mwingi: "Niwezeje kukuacha, Efraimu? Niwezeje kukuponya, Israeli? Niwezeje kukufanya kama Adma? Niwezeje kukuweka kama Seboimu? Moyo wangu umegeuka ndani yangu, huruma zangu zimewaka pamoja" (Hos. 11:8).

Yesu alinena maneno haya ya maombolezo juu ya Yerusalemu: "Ee Yerusalemu, mnaowaua manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwenu! Mara ngapi nimetamani kuwakusanya watoto wako, kama vile kuku akusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa zake, lakini hukutaka! Tazama nyumba yako imeachwa tupu na ukiwa." (Matt. 23:37–38).

> Kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa. (Luka 9:56)

> Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake. Mchana husemezana na mchana, Usiku hutolea usiku maarifa. Hakuna lugha wala maneno, Sauti yao haisikilikani. Sauti yao imeenea duniani mwote, Na maneno yao hata miisho ya ulimwengu. Katika hizo ameliwekea jua hema. (Zab. 19:1–3)

Mungu ananena kwa watu wote kupitia kwa uumbaji wake. Hakuna yeyote ambaye amefungiwa kutoka kwa makaribisho ya kujifunza kumhusu kwa sababu ya utata wa lugha au ukosefu wa neno lililochapishwa.

*Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi;*

*aletaye nje jeshi lao kwa hesabu; aziita zote kwa majina;*

*kwa ukuu wa uweza wake, na kwa kuwa yeye ni hodari*

*kwa nguvu zake; hapana moja isiyokuwapo mahali pake.*

*—Isaya 40:26*

# 20

## Tunawezaje Kuwa na Uzima wa Milele?

Awali katika kitabu tulisoma kuhusu anguko la mwanadamu ambalo limerekodiwa katika Mwanzo, sura 3. Joka, mdanganyifu akijificha, aliwaongoza Adamu na Hawa kuamini kuwa Mungu alikuwa mbinafsi na hawezi kuaminiwa. Walipoamini uongo huo, walitafuta kujitenga kutoka kwa mpaji wa uzima wao, na mchakato wa kufa ulianza kwao.

Vifo vyote tangu siku hiyo ni tokeo la kuamini uongo huo kumhusu Mungu. Jamii ya mwanadamu ilikengeuka kutoka kwa Mungu katika bustani ya Edeni kwa sababu Adamu na Hawa walibadili mawazo yao kumhusu Mungu. Mahali ambapo waliamini wakati mmoja, sasa wanashaka naye. *Hili bado ndilo tatizo letu sahihi.* Kile ambacho tunahitaji ni kubadilisha mawazo yetu kumhusu Mungu. Tutakapofanya hivi uwaaminifu utaondoa shaka, na upendo utaondoa wasiwasi kumhusu. Tutarejeshwa kwa muumbaji wetu, na tutakuwa na uzima wa milele.

Adamu na Hawa walipoamini uongo wa joka kumhusu Mungu na wakajaribu kujificha kutoka kwake, Mungu mwenye hakubadilishwa na yale yaliyotendeka. Upendo wake kwa wanawe waliojitenga haukuwa umedidimia hata kidogo. Mpango wowote wa wokovu ambao hutegemea juhudi zetu za kubadilisha mawazo ya Mungu kutuhusu hutafuta suluhisho la tatizo ambalo *haliko*. Mungu tayari anamawazo mema juu yetu na hahitaji ushawishi wowote ili kutuwazia mema. Tayari anatupenda na anathamini kila mmoja wetu.

Mungu alipowatoa wana wa Israeli kutoka nchi ya Misri, walionywa kuhusu hatari ya kuabudu sanamu. Miungu hii ya uongo ilikuwa kawaida katika kipindi cha Bibilia na ilikuwa zao la mawazo ya kupotosha. Mara nyingi ilijulikana kama yenye

hasira na katika hitaji la kutulizwa. Sadaka na kafara zilitolewa ili kuondoa hasira yao. Tunaweza uliza kwa makini: je, njia yetu ya mahusiano na Mungu inaazima chochote kutoka kwa ibada ya sanamu ya kale?

> Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. Nimekutukuza Wewe duniani kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye (Yohana 17:3–4)

Katika ombi hili la Yesu kwa Baba yake, anaelezea wazi uzima wa milele. Ni tukio la kuja kumjua Mungu. Maarifa haya ya uzoefu huturejesha kwa mpaji wetu wa uzima. Tunaanza kuona kusudi halisi la huduma ya Yesu ulimwenguni mwetu—kumdhihirisha Mungu kwa usahihi kama asiye na ubinafsi, mkarimu, mpole, mwenye rehema, na msamehevu. Watu walipoyasikiliza maneno ya Yesu, walikuwa wakiyasikia maneno ya Mungu. Watu walipomuona Yesu akiponya wagonjwa, akiwalisha wenye njaa, akiwatia moyo, akiwashika watoto wadogo mikononi mwake, na kuruhusu aeleweke visivyo na kuudhiwa, walikuwa wakimuona Mungu—Mungu katika utukufu wake.

Ili kuepuka utata, ni muhimu kufahamu kuwa kuna njia nyingi za kuonyesha wokovu, lakini hizi zote huwasilisha sura ya Mungu yenye mgogoro.  Somo hili, litaangazia njia moja maarufu ya wokovu ambayo karibu kila mmoja wa jamii ya magharibi anafahamiana nayo. Watu wengi wa kweli wanaambatana nayo. Haya ni maoni kuwa wokovu ni suala harali.

Baadhi ya sifa za maoni haya ni kama vile:

- Msisitizo juu ya utawala wa Mungu badala ya kipawa cha Mungu cha uhuru kwa wana wake.

- Msisitizo wa uwezo wa Mungu kuokoa badala ya mapenzi ya Mungu kuturejesha kwake.
- Imani kuwa Mungu ni mkamilifu na mtakatifu kwamba anakasirishwa na dhambi zetu badala ya kuamini upendo wa Mungu kwetu na hitaji la kuja kwetu jinsi tulivyo. Mungu anahuzunishwa na dhambi kwa sababu ya kile hutenda kwa wale anaowapenda, sio kwa sababu yeye mwenyewe anakasirishwa nayo.
- Imani kuwa Mungu anahitaji damu ili kutuliza ghadhabu yake badala ya kufahamu kuwa Mungu anataka kutuponya kutoka kwa hofu yake ya patholojia. Anataka tufahamu kuwa *dhambi* ni ya kufisha—sio yeye.
- Imani kuwa Mungu anaweka rekodi ya dhambi zetu ili kutumia dhidi yetu katika hukumu ijayo badala ya kufahamu kuwa kila rekodi inayohifadhiwa itakuwa ya kuonyesha kuwa Mungu alifanya kila kitu ambacho angeweza kufanya ili kumuokoa kila mtu.
- Mtazamo kuwa Mungu huweka ghadhabu kwa kuvunja sheria badala ya kufahamu kuwa ni ubinafsi wetu, katika kukosa uiano na sheria ya upendo, ambao hutuadhibu. Kama vile hatuwezi vunja sheria za maumbile kwa ukatili, vile vile hatuwezi ihalifu sheria ya upendo bila kupata adhabu.
- Kuelezea injili kama habari njema kumetoa njia ya kuepuka kupokea adhabu anayoweka kwa kuvunja sheria badala ya kujua habari njema halisi ni kumhusu Mungu mwenyewe. Kama Mungu angekuwa mtu ambaye angeweka adhabu ya kifo kwa kuvunja sheria, ingekuwa habari *mbaya*.
- Mawazo ya kukombolewa badala ya kumwona Mungu kama mtu wa kuaminiwa kabisa. Kwa kweli, zaidi tunavyoangazia ukweli kumhusu Mungu wetu mpole, ndivyo tutakavyopunguza wasiwasi wa wokovu *wetu*

> *wenyewe*, na ndivyo tutawapenda na kuwathamini wengine zaidi. "Kwa maana mtu yeyote anayetaka kuiokoa nafsi ataipoteza, lakini yeye ayapotezaye maisha yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili ataiokoa" (Marko 8:35).

Injili harali kamambe huunga mkono visivyofaa lengo la kuwa na hakikisho la wokovu. Mungu hajaweka kwetu mzigo wa kujua hali ya wokovu ya mtu yeyote—ikiwemo wetu wenyewe. Badala ya kuangazia hali yetu wenyewe ya kiroho, tunahitaji kuangazia yule ambaye daima anamuona kila mmoja wetu sio tu jinsi tulivyo bali pia kile ambacho tunaweza kuwa. Mungu anampenda na kumthamini kila mmoja wetu zaidi ya vile tunaweza jipenda na kujithamini sisi wenyewe. Bila tashwishi, Mungu anataka kila mmoja wetu kuishi naye milele. Anataka pia tufahamu kuwa niwakuaminiwa kabisa na ana zaidi ya uwezo wa kuponya mawazo yetu ya hofu: "Katika upendo hakuna hofu. Lakini upendo ulio kamili huitupa nje hofu" (1 Yohana 4:18).

Tumelinganisha kwa kifupi injili mbili tofauti kabisa: injili harali na injili ya uponyaji. Injili ya uponyaji iko katika uiano mkamilifu na mafunzo na mfano wa Yesu, ilihali injili harali ina mfanano mwingi na uamuzi wa mfumo wa mahakama ya mwanadamu ambayo yalitumika kumhukumu Yesu (mponyaji wetu mpole) kifo.

> Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho. (Yer. 29:11)

Wakati mwingi, juhudi, na gharama inayowekwa katika shughuli za dini, kwa azimio la kumshawishi Mungu kuwaza mema juu yetu, imekuwa ubadhirifu tu.

> Tupilieni mbali nanyi makosa yenu yote mliyoyakosa; jifanyieni moyo mpya na roho mpya; mbona mnataka kufa, enyi nyumba ya Israeli? Maana mimi sikufurahii kufa kwake afaye, asema Bwana MUNGU; basi ghairini, mkaishi. (Ezek. 18:31–32)

Ombi la Mungu kwa kila mmoja wetu ni kugeuka kutoka kwenye ubinafsi hadi kwa njia ya uzima.

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Kwa maana Mungu hakumtuma Mwanawe kuuhukumu ulimwengu, bali kwa Yeye ulimwengu upate kuokolewa. (Yohana 3:16–17)

Kumwamini Yesu ni kuamini alichodhihirisha kujihusu (Mwana wa Mungu) na Mungu Baba.

> Kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao. Naye ametukabidhi sisi ujumbe huu wa upatanisho. (2 Wakorintho 5:19)

Kama juhudi nzima ya Mungu kumwokoa mwanadamu kutoka kwenye mauti ya milele inaweza fupishwa kwa neno moja, neno linaweza kuwa *upatanisho*.

> Hapo kwanza ninyi mlikuwa mmetengana na Mungu na mlikuwa adui Zake katika nia zenu kwa sababu ya mwenendo wenu mbaya. (Kol. 1:21)

Tangia anguko la mwanadamu, mkao kuelekea ukengeufu uliingia katika akili zetu—kamwe sio katika ya Mungu.

> Kwa kuwa Mungu, Yeye aliyesema, Nuru na ing'ae gizani, ameifanya nuru Yake ing'ae mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo. (2 Kor. 4:6)

Giza ambalo fungu hili linarejelea ni kutomfamu Mungu vilivyo kwetu. Utukufu wa Mungu ni sifa na tabia yake, ambayo inaonekana katika uso wa Yesu.

> Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho. (2 Kor. 3:18)

Tunabadilishwa kwa kutazama. Kanuni hii hutenda kazi kwa njia zote. Kama tutamwamini Mungu kuwa mbinafsi, inatia nguvu ubinafsi wetu wenyewe. Kama tutamuona kama asiye mbinafsi kikamilifu, itafanya kazi kung'oa ubinafsi wetu tuliyoridhi. Kutafakari upendo, rehema na msamaha wa Mungu hufanya sifa sawa ziweze kuonekana ndani yetu.

> Nawaambieni, vivyo hivyo kutakuwa na furaha zaidi mbinguni kwa sababu ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa wenye haki tisini na tisa ambao hawana haja ya kutubu. (Luka 15:7)

Kutubu hakumaanishi kusema “pole” kwa Mungu. Kutubu kunamaanisha kugeuka, au kubadili mawazo. Kutubu kwa kweli, katika muktadha wa kile ambacho Yesu alifundisha, kunamaanisha kubadili mawazo kumhusu Mungu. Tutamuona jinsi Yesu alimwasilisha kikamilifu alivyo.

> Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi. (Matt. 11:28–30)

Hatuhitaji kutenda ili kuwa wema katika jaribio batili la kujiinua kiroho. Juhudi zetu zote za kujipima hutuongoza katika kujiangazia na itapelekea kwa kiburi au kuvunjika moyo. Yesu anasuluhisho la taharuki hii. Anasema tu, “mjifunze kutoka kwangu.”

> Naye akapewa kitabu cha nabii Isaya, akakifungua na kukuta mahali palipoandikwa: Roho wa Bwana yu juu Yangu, kwa sababu amenitia mafuta kuwaletea maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao na vipofu kupata kuona tena, kuwaweka huru wanaoonewa. (Luka 4:17–18)

Sote tunahitaji kile ambacho Yesu alikuja kukamilisha; *hakuna* kubagua.

# 21

## Lazima Tuogope Hukumu?

Tunapozingati hukumu, itasaidia kwanza kutambua ni nani anahukumiwa na ni nani ambaye anahukumu. Tukirejelea mazungumzo kati ya Hawa na joka katika bustani ya Edeni, kumbuka kuwa joka aliweka swali akilini mwa Hawa kuhusu haki, nia njema, na uaminifu wa Mungu. Kwa kuangazia kwa uaminifu kiasi, itaonekana dhahiri kuwa sio mwanadamu aliyekuwa akiwekwa katika majaribu hapo—ilikuwa Mungu.

Inaweza kuwa vigumu kwetu kuelewa wazo la Mungu *kuruhusu* yeye mwenyewe atiwe katika majaribu. Hata hivyo, mtazamo huu unafaida tu kwa yule ambaye atafika katika mzizi wa undani wa mafunzo ya Bibilia. Tumekuwa tukimhukumu Mungu bila kujua tangia dayolojia hiyo na ibilisi. Tumempa hukumu ya haki?

Wakati tunapotoshwa katika mwelekeo wetu wa kujiweka kati ya hukumu, hatujaachwa nje hata kidogo inapokuja katika suala la hukumu. Mungu hajatuweka katika jaribio; hata hivyo, tuko kati kutotambua hasa katika kujihukumu na kujilaani sisi wenyewe. Yesu alisema kuwa maneno aliyozungumza ni uzima. Tunauchaguzi wa kuyakubali au kuyakataa, je, hatujajifanyia hukumu yenye matokeo kwetu sisi wenyewe?

Mungu hakati kesi kama jinsi inavyotendeka katika mahakama ya sheria. Tunapoamua kuendelea katika njia ya kujihukumu na mauti, Mungu hawezi fanya kitu kingine zaidi ya kuridhia bila kutaka uamuzi wetu.

Kuna kipengele kingine cha hukumu cha kuzingatia. Tunapowahukumu wengine, inakuwa na matokeo hasi kwetu. Tunapowalaumu wengine, tunajilaumu sisi wenyewe katika mchakato huo. Ili kuona tunaye hitaji kumwogopa kwa *kweli* katika hukumu, tunahitaji tu kutazama kwenye kioo.

Injili ya kisa cha mwanamke aliyeshikwa katika uzinifu kinatupa mfano wa jinsi hukumu hutenda kazi:

> Lakini Yesu akaenda katika Mlima wa Mizeituni. Alfajiri na mapema Yesu akaja tena hekaluni, watu wote wakakusanyika, akakaa akaanza kuwafundisha. Walimu wa sheria na Mafarisayo wakamleta mwanamke mmoja aliyefumaniwa akizini. Wakamsimamisha katikati ya umati wa watu wote. Wakamwambia Yesu, Mwalimu, huyu mwanamke amekutwa akizini. Katika sheria, Mose alituamuru kuwapiga kwa mawe wanawake wa namna hii, mpaka wafe. Sasa Wewe wasemaje? Walimwuliza swali hili kama mtego ili wapate sababu ya kumshtaki. Lakini Yesu akainama akaanza kuandika ardhini kwa kidole Chake. Walipoendelea kumwulizauliza akainuka, akawaambia, Kama kuna mtu ye yote miongoni mwenu ambaye hana dhambi na awe wa kwanza kumtupia jiwe. Akainama tena na kuandika ardhini. Waliposikia haya, wakaanza kuondoka mmoja mmoja, wakianzia wazee, hadi Yesu akabaki peke Yake na yule mwanamke akiwa amesimama mbele Yake. Yesu akainuka na kumwambia, Wako wapi wale waliokuwa wanakuhukumu kuwa mwenye hatia? Yule mwanamke akajibu, "Hakuna hata mmoja Bwana. Yesu akamwambia, *Hata Mimi sikuhukumu*. Nenda zako, kuanzia sasa usitende dhambi tena. (Yohana 8:1–11, mkazo umetiliwa)

Mwanamke aliyeletwa mbele za Yesu na kuwasilishwa kama mvunja sheria alikuwa mwathiriwa aliyetumiwa na viongozi sugu wa dini katika jaribio lao la kumuangamiza Yesu ambaye walimhukumu kama tisho kwa dini yao. Washtaki wa

mwanamke walikata rufaa kwa sheria ya Musa. Katika pambano lingine na Mafarisayo, akishughulikia talaka, Yesu aliwaambia kuwa sheria ya Musa ilikuwa na makubaliano na mioyo yao migumu: "Yesu akawaambia, Musa aliwaandikia sheria hiyo kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu" (Marko 10:5).

Uzito wa kile ambacho kilitendeka katika *chumba hiki cha hukumu* utakuwa wazi tunapotambua kuwa Yesu alikuwa Mungu duniani na madaraka yote ya uungu, ikiwemo haki ya kutoa hukumu. Mungu hakutoa hukumu mara moja kwa shtaka ambalo alileteewa, lakini badala yake aliinama chini na kuandika ardhini kwa kidole chake. Walipomsukuma awape jibu, aliwaambia, "Kama kuna mtu ye yote miongoni mwenu ambaye hana dhambi na awe wa kwanza kumtupia jiwe." Kisha akaendela kuandika ardhini.

Yesu alikuwa na kusudi la kila jambo alilosema na kulitenda. Alipoandika ardhini, haikuwa kukwepa swali la viongozi wa dini. Alijua hali ambayo ilikuwa imemleta mwanamke mbele yake. Yesu pia alijua historia ya kila mmoja wa washtaki wake na akayasoma mawazo na nia yao. Angewashughulikia kwa mkemeo mkali wanafiki hawa mbele ya mashahidi. Badala yake, kwa neema aliwafanya viongozi wa dini wafahamu dhambi zao wenyewe kwa kuziandika ardhini—andiko la kipekee lisilo la kudumu la kurekodi dhambi zao.

Yesu alipenda na kuthamini vikubwa kila mmoja aliyemzunguka licha ya hali zilizokuwa zimewaleta pamoja. Kazi yake ilikuwa kuuokoa ulimwengu, na kuleta upatanisho wa mwanamke na *washtaki* wake, ambao hakuwa na hamu ya kuwatenganisha zaidi.

Yesu alisema kwa viongozi wa dini, "Kama kuna mtu ye yote miongoni mwenu ambaye hana dhambi na awe wa kwanza kumtupia jiwe." Hapa anapitisha jukumu la kuhukumu kwao tena. Yesu hakuja ulimwenguni kuhukumu na kulaumu, na hangetiwa katika jukumu la hakimu. Je, walimu wa sheria na

Mafarisayo walipokea makaribisho yake ya kuvurumiza mawe juu ya mwanamke? Inavyoonekana hapana, kwa vile waliondoka kwenye eneo "mmoja mmoja."

Yesu, kama Mungu, hakumkemea mwanamke, lakini katika maneno yake "ondoka, na usitende dhambi tena" aliweka wazi mlango wa uzima kwake. Hakuwa akimwamuru kuacha tu tendo lililomleta mbele zake; alikuwa akimpa uhuru kutoka kwa dhambi ya kufisha—imani kuwa Mungu hastahili uaminifu wetu.

Yesu alimpa mwanamke huyu njia ya kuepuka hukumu ya usoni. Alidhihirisha upendo wa Mungu kwake kama mtu. Mwanamke huyu alikuwa mbele ya mpaji wa uzima, na alijua kuwa angempenda na kumwamini. Mtazamo wake wa Mungu na uhusiano wake kwake ulibadilishwa kwa kiasi kikubwa kwa wema baada ya kutano hilo. Kwa mwanamke, hukumu iliyotendeka ilikuwa ya kubadilisha maisha na kutoa uzima.

Yesu hakuwakemea walimu wa sheria na Mafarisayo wenye mioyo migumu ambao walikuwa na haraka ya kumhukumu mwanamke huyu, lakini alishikilia kioo cha kiroho mbele yao ambacho kiliakisi tabia zao za giza. Na kama tokeo walikuwa "wametiwa hatiani na dhamiri yao wenyewe," na walihisi kulazimishwa kuondoka mbele ya mpaji wa uzima mtakatifu, mwenye upendo usio na ubinafsi. Walikuja kumhukumu mwingine, lakini wakamalizia kujihukumu wenyewe katika mchakato huo.

> Kwa hiyo huna udhuru wo wote, wewe mtu uwaye yote, utoaye hukumu kwa mwingine, kwa maana katika jambo lo lote unalowahukumu wengine, unajihukumu wewe mwenyewe kwa sababu wewe unayehukumu unafanya mambo yayo hayo. Basi tunajua kwamba hukumu ya Mungu dhidi ya wale wafanyao mambo kama hayo ni ya kweli. Hivyo wewe

> mwanadamu, utoapo hukumu juu yao na bado unafanya mambo yale yale, unadhani utaepuka hukumu ya Mungu? (Rom. 2:1–3)

Mungu humpa kila mmoja wetu uhuru wa kweli. Hawezi kuupa kipaumbele uamuzi wetu wa kujihukumu. Hukumu ya Mungu hapa ni kuridhia bila kutaka kujihukumu huku tunapochagua kukaa nje ya mduara wa kubadilishana upendo na uzima. Hakuna kuepuka kutoka kwa hukumu hii kwa vile Mungu hawezi tulazimisha, kinyume na mapenzi yetu, kufuata njia inayotwelekeza uzimani.

> Wala Baba hamhukumu mtu ye yote, lakini hukumu yote amempa Mwana. (Yohana 5:22)

> Mungu, Baba, hatuhukumu.

> Roho ndiye atiaye uzima, mwili haufai kitu. Maneno haya niliyowaambia ni Roho tena ni uzima (Yohana 6:63)

Maneno ya Yesu ni uzima. Katika kila neno ambalo Yesu alinena alidhihirisha upendo wa Mungu wakupatanisha.

> Yesu akapaza sauti akasema, Ye yote aniaminiye, haniamini Mimi peke Yangu, bali Yeye aliyenituma. Ye yote anionaye Mimi, amemwona Yeye aliyenituma. Mimi nimekuja kama nuru ulimwenguni, ili kwamba kila mtu aniaminiye asibaki gizani. Mimi simhukumu mtu ye yote anayesikia maneno Yangu na asiyatii, kwa maana sikuja kuuhukumu ulimwengu, bali kuuokoa. Yuko amhukumuye yeye anikataaye Mimi na kutokuyapokea maneno Yangu, yaani, yale maneno

> niliyosema yenyewe yatamhukumu siku ya mwisho. (Yohana 12:44–48, mkazo umetiliwa)

Yesu hatuhukumu, Mungu hutupa Neno la Uzima, lakini kamwe hatulazimishi kulikubali.

> Usihukumu ili usije ukahukumiwa. Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea.Kwa nini unatazama kibanzi kidogo kilichomo kwenye jicho la ndugu yako na wala huoni boriti iliyoko kwenye jicho lako? Au unawezaje kumwambia ndugu yako, ‘Acha nitoe kibanzi kwenye jicho lako wakati kuna boriti kwenye jicho lako mwenyewe? Ewe mnafiki, toa kwanza boriti kwenye jicho lako mwenyewe, nawe ndipo utakapoona wazi ili kuondoa kibanzi kilichoko kwenye jicho la ndugu yako. (Matt. 7:1–5)

Kama Mungu Baba hatuhukumu na Yesu hatuhukumu, mbona basi tufikirie kuwa tumehitimu kuwahukumu wengine tunapokuwa na roho ya kuhukumu (boriti ndani ya macho yetu wenyewe)?

> Amin, amin, ninawaambia, ye yote anayesikia maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenituma, anao uzima wa milele, naye hatahukumiwa, bali amepita kutoka mautini, na kuingia uzimani. (Yohana 5:24)

Kufahamu ukweli kumhusu Mungu na kujifunza kumwamini hupelekea kwa uzima. Yesu alisema, “Ye yote amwaminiye hahukumiwi” (Yohana 3:18)

> Ndipo Paulo na Barnaba wakawajibu kwa ujasiri, wakisema, “Ilitupasa kunena nanyi neno la Mungu kwanza. Lakini kwa kuwa mmelikataa, mkajihukumu wenyewe kuwa hamstahili uzima wa milele, sasa tunawageukia watu Mataifa. (Matendo 13:46)
>
> Huu ni mfano wenye mwanga wa kujihukumu.
>
> Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa. Msilaumu, nanyi hamtalaumiwa. Sameheni, nanyi mtasamehewa. (Luka 6:37)

Katika injili ya Luka, mfano wa mwana mpotevu unatufunza kuwa Mungu tayari ametusamehe hata kabla ya kuagiza. Kama tunahukumiwa, kulaumiwa, au kutosamehewa, tunasalia na nafsi yetu kujilaumu “Kwa kuwa kile apandacho mtu ndicho atakachovuna” (Gal. 6:7).

> Yesu akasema, Nimekuja ulimwenguni humu kwa ajili ya kuhukumu, ili wale walio vipofu wapate kuona, nao wale wanaoona, wawe vipofu. Baadhi ya Mafarisayo waliokuwa karibu naye wakamsikia na kumwambia, Je, kweli sisi ni vipofu? Yesu akawajibu, Kama mngekuwa vipofu kweli, msingekuwa na hatia ya dhambi, lakini kwa kuwa mnasema, Tunaona, basi mna hatia. (Yohana 9:39–41)

Ni nini “hukumu” ambayo Yesu alikuja ulimwenguni kwayo? Alikuja katika ulimwengu huu kudhihirisha upendo wa Mungu kwa mwanadamu na thamani kubwa anayoweka kwa kila mmoja wetu. Anataka sisi *kuona* wengine jinsi anavyotuona sisi, na kuwathamini wengine anavyotuthamini. Yesu anatufunza *kufumbia macho* dhambi za wengine na pia tofauti

zilizoundwa ambazo zilitutenganisha: matengano, utaifa, ukabila, siasa za usaidizi, au kifaa kingine chochote ambacho kinahimiza mawazo ya sisi dhidi yao.

Mafarisayo hawakufahamu somo hili ambalo Yesu alikuwa akifundisha. Walikuwa na madhehebu makali ya kidini na waliwatazama watu wa mataifa, ambao hawakuwa wa asili ya Wayahudi, kama mumbwa. Pia walikuwa wataalamu wa mtindo wa nafsi katika *kuona* dhambi za wengine na kuwahukumu kwazo.

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Kwa maana Mungu hakumtuma Mwanawe kuuhukumu ulimwengu, bali kwa Yeye ulimwengu upate kuokolewa. Ye yote amwaminiye hahukumiwi, lakini asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakumwamini Mwana pekee wa Mungu. *Hii ndiyo hukumu kwamba: Nuru imekuja ulimwenguni, nao watu wakapenda giza kuliko nuru* kwa sababu matendo yao ni maovu (Yohana 3:16–19, mkazo umetiliwa)

Katika fungu hili, *jina* humaanisha tabia au sifa. Kukataa ufunuo wa tabia ya Mungu ambao Yesu alileta katika nuru ni, kwa uhalisi, kumkataa Mungu. Kwa Yesu, Mungu anasema—Huyu ndiye *niliye kwa kweli*.

> Asubuhi na mapema, viongozi wa makuhani wote na wazee wa watu wakafanya shauri pamoja dhidi ya Yesu ili kumwua. Wakamfunga, wakampeleka na kumkabidhi kwa Pilato, ambaye alikuwa mtawala. (Matt. 27:1–2)

Hii ni picha ya aina gani! Washika-Dini waliojawa na dhambi wakitafuta kumuua mpaji wa uzima wao, na hawapingi wala hata kuwahukumu! Ni nani au ni nini ni cha kufisha—Mungu au dhambi?

Tunasoma na kusikia kuhusu saa za mwisho kumhusu Kristo kabla ya kufa kwake bila kutambua maana ya ndani ya kujaribiwa na kusulubishwa kwake. Yesu ni Mungu kamili na pia mwanadamu kamili. Wakati Yesu aliletwa mbele za Pontius Pilato ili kujaribiwa, alikuwa Mungu *kamili*. Alipohukumiwa na kulaumiwa, alikuwa Mungu *kamili*. Wakati alikuwa akiteswa, kukejeliwa, na kusulubishwa msalabani ili kufa bado alikuwa, wakati huo wote, Mungu *kamili*.

Mungu aliruhusu atiwe katika majaribu na kuhukumiwa na wale ambao aliwapenda na kutamani kuwarejesha kwake. Mbona? Kwa sababu tuna wakati mgumu ajabu *kuona* kile ambacho dhambi zetu zimefanya *kwake.*

Yesu, Mwana wa Mungu, alipitia mateso makubwa katika saa zake za mwisho za maisha yake duniani—zaidi ya vile tunaweza fikiria. Lakini mateso ya Yesu hayakuanzia katika bustani ya Gethsemane, na wala hayakuishia kwa maneno yake ya kifo chake msalabani. Mungu ameteseka nasi na kwa ajili yetu tangu kuingia kwa dhambi duniani, na atazidi kuteseka nasi na kwa ajili yetu hadi siku ambayo dhambi itakuwa imepokea uangamizo wake na mateso yote na mauti yamefika mwisho wake milele.

Kujaribiwa na kuteseka kwa Yesu mikononi mwa wale ambao aliumba ili kushiriki katika upendo wake mkuu kunapaswa kutupa picha ya mateso ambayo tumemsababishia kwa maelfu ya miaka. Tunaendelea kumsimamisha Mungu mbele ya mahakama yetu ya wanadamu ili kujibu mashtaka ya kutofautiana, kutochukua hatua, utengano, na hata utendaji, maangamizi ya kisasi. Wakati mwingi zaidi uamuzi wetu ni *hatia kama shtaka lilivyo*! Ni nini zaidi ambacho Mungu anaweza

fanya ili kupatanisha wana wake waliojitenga kuliko kile ambacho anafanya? Msalaba unageuza ubishi wa Shetani kuwa Mungu ni mbinafsi, asiyejali, na asiyeaminika.

Licha ya jinsi tumesawijika tabia na sifa ya Mungu, kuna habari njema—Mungu anajua mbona tunamuelewa visivyo, na hatulaumu kwa hilo. Ataendelea kutupenda licha ya kukosa shukurani kwetu kwa yale ambayo ametutendea na anazidi kututendea kila siku. Lakini silingekuwa jambo jema kwa Mungu kama tungetambua kuwa *yote sio kwa ajili yetu*; Muumbaji wetu anahusika kwa ukaribu katika taharuki yetu pia. Tunaweza waza kumhusu? Tunaweza ruhusu nafsi zetu kumuona kama jinsi alivyo kwa kweli—asiyebadilika, upendo kwa wengine, na kurejesha upendo anaostahili? Je, hilo ni jambo kubwa sana kuagiza? "Twampenda Yeye kwa sababu Yeye alitupenda kwanza" (1 Yohana 4:19).

*Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale.*—Isaya 63:9

# 22

## Hukumu Ya Mungu Inaonekana Jinsi Gani?

> Jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane.
>
> —Isaya 1:17

Hukumu ya Mungu kamwe haipitishi hukumu ya mahakama dhidi yetu. Inaelezewa hapa kama ya kusaidia mateso na kukuza *haki* katika ulimwengu isiokuwa na haki.

> Amin, nawaambieni, lo lote mtakalolifunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni na lo lote mtakalolifungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni. Tena nawaambia, ikiwa wawili wenu watakubaliana duniani kuhusu jambo lo lote watakaloomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa wanapokusanyika pamoja watu wawili au watatu kwa jina langu, mimi niko papo hapo pamoja nao. Ndipo Petro akamjia Yesu na kumwuliza, Bwana, ndugu yangu anikosee mara ngapi nami nimsamehe? Je, hata mara saba? (Matt. 12:18–21)

Hukumu ya haki, ya upole inaweza kuleta uaminifu.

> Na mtakapovuna mavuno ya nchi yenu, usivune kabisa kabisa pembe za shamba lako, wala usiyakusanye masazo ya mavuno yako; wala usiyakusanye masazo ya mizabibu yako, wala usiyaokote matunda ya mizabibu yako yaliyopukutika; uyaache kwa ajili ya maskini na

> mgeni; mimi ndimi Bwana, Mungu wenu. (Walawi. 19:9–10)

Mungu alitafuta kutoa usawa kwa walioonewa katika jamii ya kale.

> Na mgeni akikaa pamoja nawe katika nchi yako, usimdhulumu. Mgeni akaaye pamoja nawe atakuwa kama mzalia kwenu; mpende kama nafsi yako; kwa maana ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri; Mimi ndimi Bwana, Mungu wenu. Msifanye yasiyo haki katika hukumu, wala katika kupima, wala katika mizani, wala katika cheo. Mizani ya haki, vipimo vya haki, efa ya haki, hini ya haki, ndivyo mtakavyokuwa navyo. Mimi ndimi Bwana, Mungu wenu, niliyewatoa katika nchi ya Misri. (Walawi. 19:33–36)

> Ole wao wawekao amri zisizo za haki, na waandishi waandikao maneno ya ushupavu; ili kumpotosha mhitaji asipate haki yake, na kuwanyang'anya maskini wa watu wangu haki yao; ili wajane wawe mateka yao, na kuwafanya yatima waliofiwa na baba zao kuwa mawindo yao! (Isa. 10:1–2)

Mungu ni mjumlishi—kwake hakuna *wageni*. Mungu anafahamu sheria za wanadamu, tabia za biashara, na taasisi ambazo huwanufaisha matajiri kwa kuwanyanyasa masikini. Anaziita wizi. Aina yoyote ya ukiukaji wa haki katika biashara inaingia katika maelezo ya Bibilia ya wizi.

> Husema, Mbona tumefunga, lakini huoni? Mbona tumejitaabisha nafsi zetu, lakini huangalii? Fahamuni, siku ya kufunga kwenu mnatafuta anasa zenu

> wenyewe, na kuwalemea wote watendao kazi kwenu. Tazama, ninyi mwafunga mpate kushindana na kugombana, na kupiga kwa ngumi ya uovu. Hamfungi siku hii ya leo hata kuisikizisha sauti yenu juu. Je! Kufunga namna hii ni saumu niliyoichagua mimi? Je! Ni siku ya mtu kujitaabisha nafsi yake? Ni kuinama kichwa kama unyasi, na kutanda nguo za magunia na majivu chini yake? Je! Utasema ni siku ya kufunga, na ya kukubaliwa na Bwana? Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira? Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe? (Isa. 58:3–7)

Matendo ya kidini tu ni bure kama tukipuuza kuwasaidia wenye mahitaji. Yesu alitangaza, "Lakini ole wenu, Mafarisayo, kwa maana mnampa Mungu zaka za mnanaa, mchicha na kila aina ya mboga, lakini mnapuza haki na upendo wa Mungu." (Luka 11:42).

> Bwana wa majeshi amesema hivi, ya kwamba, Fanyeni hukumu za kweli, kila mtu na amwonee ndugu yake rehema na huruma; tena msimdhulumu mjane, wala yatima, wala mgeni, wala maskini; wala mtu awaye yote miongoni mwenu asiwaze mabaya juu ya ndugu yake moyoni mwake. (Zekaria. 7:9–10)

Mungu hakubali dhuluma ya namna yoyote, wala mpango wowote wa kujinufaisha kwa kuwaumiza wengine.

> Ndugu zangu, kama waaminio katika imani ya Bwana wetu Yesu Kristo, Bwana wa utukufu, msiwe na upendeleo kwa watu. Kwa maana kama akija mtu katika kusanyiko lenu akiwa amevaa pete ya dhahabu na mavazi mazuri, pia akaingia mtu maskini mwenye mavazi yaliyochakaa, nanyi mkampa heshima yule aliyevaa mavazi mazuri na kumwambia, ''Keti hapa mahali pazuri,'' lakini yule maskini mkamwambia, ''Wewe simama pale,'' au ''Keti hapa sakafuni, karibu na miguu yangu,'' je, hamjawabagua na kuwa mahakimu mioyoni mwenu mkihukumu kwa mawazo yenu maovu? Ndugu zangu, sikilizeni: Je, Mungu hakuwachagua wale walio maskini machoni pa ulimwengu kuwa matajiri katika imani na kuurithi Ufalme aliowaahidi wale wampendao? Lakini ninyi mmemdharau yule aliye maskini. Je, hao matajiri si ndio wanaowadhulumu na kuwapeleka mahakamani? Je, si wao wanaolikufuru Jina lile lililo bora sana mliloitiwa? Kama kweli mnaitimiza ile sheria ya kifalme inayopatikana katika Maandiko isemayo, ''Mpende jirani yako kama unavyoipenda nafsi yako,'' mnafanya vema. (Yakobo 2:1–8)

Kwa Mungu hakuna upendeleo; sisi sote ni sawa machoni pake: "Mungu hana upendeleo" (Matendo 10:34).

> Dini iliyo safi, isiyo na uchafu, inayokubalika mbele za Mungu Baba yetu, ndiyo hii: Kuwasaidia yatima na wajane katika dhiki zao na kujilinda usitiwe madoa na dunia. (Yakobo 1:27)

Dini iliyo safi sio madhehebu, kufuata utaratibu, udikteta, misisimko, au kulingana na kanisa.

> Ndipo Mfalme atawaambia wale walioko upande wake wa kuume, Njoni, ninyi mliobarikiwa na Baba yangu, urithini Ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Kwa maana nilikuwa na njaa mkanipa chakula, nilikuwa na kiu mkaninywesha, nilikuwa mgeni mkanikaribisha, nilikuwa uchi mkanivika, nilikuwa mgonjwa mkanitunza, nami nilikuwa kifungoni mkaja kunitembelea. Ndipo wale wenye haki watakapomjibu wakisema, Bwana, ni lini tulikuona una njaa tukakulisha au ukiwa na kiu tukakunywesha? Lini tulikuona ukiwa mgeni tukakukaribisha au ukiwa uchi tukakuvika? Tena ni lini tulikuona ukiwa mgonjwa tukakutunza au ukiwa kifungoni tukakutembelea? Naye Mfalme atawajibu, Amin, amin ninawaambia, kwa jinsi mlimvyotendea mmojawapo wa hawa ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi. (Matt. 25:34–40)

Ni sifa zipi unapaswa kuwa nazo ili kuwa ndugu au dada ya Yesu? Kuna njia moja tu: kuwa mshiriki wa jamii ya mwanadamu. Sisi *sote* ni washiriki wa familia ya Yesu.

> *Ninawaambia kwamba wengi watatoka mashariki na magharibi nao wataketi karamuni pamoja na Abrahamu, Isaki na Yakobo katika Ufalme wa Mbinguni.*
>
> —Yesu (Matthayo 8:11)

# 23

## Mungu Ni Mnyenyekevu

Ingawa Mungu ndiye mwenye uwezo zaidi ulimwenguni; bado ni, kwa wakati huo huo, mnyenyekevu zaidi.

> Lakini malaika akawaambia: Msiogope. Kwa maana tazama nawaletea habari njema za furaha itakayokuwa kwa watu wote. Leo katika mji wa Daudi kwa ajili yenu amezaliwa Mwokozi, ndiye Kristo Bwana. Hii ndiyo itakayokuwa ishara kwenu: Mtamkuta mtoto mchanga amefunikwa nguo za kitoto na kulazwa katika hori ya kulia ng'ombe. (Luka 2:10–12)

Mungu alichagua njia ya unyenyekevu kabisa iwezekanavyo ya kuingia katika ulimwengu wetu—kama mtoto asiye dhuru akilala horini.

> Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi. (Matt. 11: 28–30)

Yesu angewezaje, Mwana wa Mungu, kuwa wazi? Anasema, "Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo."

> Naye Yesu akamwambia, Mbweha wana mashimo, nao ndege wa angani wana viota vyao, lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa chake. (Matt. 8:20)

Hapa Yesu anajitambulisha na masikini zaidi katika jamii: wasiokuwa na kwao.

> Wakamvalisha Yesu joho la zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamvisha kichwani. Wakaanza kumsalimu kwa dhihaka, Salamu, Mfalme wa Wayahudi! Wakampiga kwa fimbo ya mwanzi tena na tena kichwani na kumtemea mate. Wakapiga magoti mbele Yake wakasujudia kwa kumdhihaki. Walipokwisha kumdhihaki, wakamvua lile joho la zambarau, wakamvika zile nguo Zake mwenyewe. Kisha wakamtoa nje ili wakamsulibishe. Kusulibiwa Kwa Yesu Basi wakamsulibisha, nazo nguo Zake wakagawana miongoni mwao kwa kuzipigia kura ili kuamua ni nini kila mtu atakachochukua. Pamoja naye walisulibiwa wanyag'anyi wawili mmoja upande Wake wa kuume na mwingine upande wa kushoto. Nayo maandiko yakatimizwa, yale yasemayo, Alihesabiwa pamoja na watenda dhambi. (Marko 15:17–20, 24, 27–28)

Kuanzia kwa kuzaliwa kwake kimasikini hadi kusulubishwa kwake katikati ya wezi wawili Yesu, Mwana wa Mungu, daima alionyesha unyenyekevu na uvumilivu.

> Ee mwanadamu, yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako! (Mika. 6:8)

> Je! Watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana? (Amosi 3:3)

Tutatembea kwa uiano na Mungu tutakapokuwa wanyenyekevu jinsi alivyo.

Tutakapofahamu uvumilivu ambao Mungu wetu mpole alidhihirisha, tunawezaje ruhusu hata chembe moja ya shaka kuhusu uaminifu wake?

*Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote. Alionewa, lakini alinyenyekea, Wala hakufunua kinywa chake; Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, Na kama vile kondoo anyamazavyo Mbele yao wakatao manyoya yake; Naam, hakufunua kinywa chake. Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; Na maisha yake ni nani atakayeisimulia? Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; Alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu. Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake.*

*—Isaya 53:6–9*

# 24

## Mungu Ni Mtumishi, Sio Bwana wa Mtumwa

> Siwaiti ninyi watumishi tena, kwa sababu watumishi hawajui bwana wao analofanya, bali nimewaita ninyi rafiki, kwa maana nimewajulisha mambo yote niliyoyasikia kutoka kwa Baba Yangu.
>
> —Yesu (Yohana 15:15)

Mungu hahitaji utiifu wa imani yetu ya kipofu. Anataka urafiki wetu. Tunapozungumza na rafiki, hatutumii urasmi au upagani. Mungu anataka tuzungumze naye kwa uaminifu kama tunavyozungumza na rafiki wa karibu—hii ndio maana ya kweli ya maombi. Mungu alituumba kwa kusudi, na anatukaribisha ili kutendea kazi uwezo huo: “Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana.” (Isaya 1:18).

> Lakini Yesu akawaita wote pamoja na kuwaambia, Mnafahamu kuwa watawala wa watu wasiomjua Mungu huwatawala kwa nguvu, nao wenye vyeo huonyesha mamlaka yao. Isiwe hivyo kwenu. Badala yake, ye yote anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi kuwa mtumishi wenu, Naye anayetaka kuwa wa kwanza miongoni mwenu ni lazima awe mtumwa wenu, kama vile ambavyo Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi. (Matt. 20:25–28)

Yesu alionyesha sheria ya uzima—alijitoa kuwahudumia wengine.

> Yesu akapita katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri Habari Njema za Ufalme wa Mungu, akiponya kila ugonjwa na kila aina ya maradhi miongoni mwa watu. Kwa hiyo sifa zake zikaenea sehemu zote za Shamu, nao watu wakamletea wote waliokuwa na magonjwa mbalimbali na maumivu, waliopagawa na pepo, wenye kifafa na waliopooza, naye akawaponya. Makutano makubwa ya watu yakawa yanamjia kutoka Galilaya, Dekapoli, Yerusalemu, Uyahudi na kutoka ng'ambo ya Mto Yordani. (Matt. 4:23–25).

> Mtu mmoja mwenye ukoma alimjia akamwomba akipiga magoti akamwambia Yesu, Ukitaka, waweza kunitakasa. Yesu akiwa amejawa na huruma, akanyosha mkono Wake akamgusa, akamwambia, Nataka takasika! Mara ukoma ukamtoka, naye akatakasika. (Marko 1:40–42).

Yesu alifanya kazi bila kuchoka na kwa huruma ili kusaidia aina zote za mateso. Hakuna yeyote aliyezidi utambuzi wake na upendo wake wa kujali: “Lakini kuna mambo mengine mengi ambayo Yesu alifanya, kama yote yangeliandikwa, nadhani hata ulimwengu wote usingekuwa na nafasi ya kutosha kuweka vitabu vyote ambavyo vingeandikwa. Amen.” (Yohana 21:25).

> Yesu akijua ya kwamba Baba ameweka vitu vyote chini ya mamlaka Yake na kwamba Yeye alitoka kwa Mungu na alikuwa anarudi kwa Mungu, hivyo aliondoka chakulani, akavua vazi Lake la nje, akajifunga kitambaa kiunoni. Kisha akamimina maji kwenye sinia na kuanza kuwanawisha wanafunzi Wake miguu na kuikausha

kwa kile kitambaa alichokuwa amejifunga kiunoni. (Yohana 13:3–5)

Kufunua huku "matendo ya Mungu" kunatendeka katika jioni ya mwisho ya Kristo saa chache kabla ya kujaribiwa na kusulubishwa kwake. Injili ya Luka inatoa maelezo hatari kuhusu wanafunzi wa Yesu wakati wa tukio hili: "Pia yakazuka mabishano katikati ya wanafunzi kwamba ni nani anayeonekana kuwa mkuu wa wote miongoni mwao." (Luka 22:24).

Hapa kuna mandhari: Yesu alijua kuwa alitoka kwa Mungu. Vitu vyote vilikuwa mikononi mwake. Kwa njia nyingine, Yesu alijua kikamilifu kuwa *alikuwa* Mungu, na uwezo wote wa Mungu. Pia alijua kuwa wanafunzi wake mwenyewe walikuwa katikati ya mgogoro kuhusu ni nani kati yao angekuwa mkuu katika Ufalme wa Mungu. Yesu alifanya nini? "Akajifunga kitambaa kiunoni." na akatawadha miguu ya wanafunzi wake wenye umuhimu wa kibinafsi (kazi ya mtumwa wa nyumbani katika utamaduni huo).

*Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu. Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya si kitu, akajifanya sawa na mtumwa, akazaliwa katika umbo la mwanadamu.*

—*Wafilipi 2:5–7*

# 25

## Upendo wa Mungu Hauna Mipaka

> Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini mimi sitakusahau wewe. 16 Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu; kuta zako ziko mbele zangu daima.
>
> —Isaya 49:15–16

Tunaweza kuwa na wakati ambao tunahisi kuwa Mungu ametusahau, lakini hisia daima sio kipimo halisi cha ukweli. Mungu anasema kuwa hawezi tusahau: "Mnajua kwamba shomoro watano huuzwa kwa senti mbili? Lakini Mungu hamsahau hata mmoja wao. Naam, hata idadi ya nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa. Kwa hiyo msiogope, ninyi ni wa thamani kuliko mashomoro wengi." (Luka 12:6–7).

> Kwa maana nimekwisha kujua kwa hakika ya kuwa wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuja, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kingine cho chote kitakachoweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu. (Rom. 8:38–39)

Inaweza kosa kuwezekana kuelezea upendo wa Mungu kwetu. Juhudi zetu zote za kuelezea upendo wake zinapungukiwa.

> Oneni ni pendo kuu namna gani alilotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu. (1 Yohana 3:1)

Tumaini la Mungu kwa kila mmoja wetu ni kuwa tutamtambua kama Baba yetu wa Mbinguni. Kisha tutatambua urithi wetu kama wana na binti za Mungu.

> Angalia ili usimdharau mmojawapo wa hawa wadogo, kwa maana nawaambia, malaika wao mbinguni daima wanauona uso wa Baba yangu aliye mbinguni. Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kuokoa kile kilichopotea. Mwaonaje? Ikiwa mtu anao kondoo mia moja na mmoja wao akapotea, hatawaacha wale tisini na tisa vilimani na kwenda kumtafuta huyo mmoja aliyepotea? Naye akisha mpata, amin, nawaambia, hufurahi zaidi kwa ajili ya huyo kondoo mmoja kuliko wale tisini na tisa ambao hawakupotea. Vivyo hivyo, Baba yenu wa mbinguni hapendi hata mmojawapo wa hawa wadogo apotee. (Matt. 18:10–14, mkazo umetiliwa)

Kila mtu, kuanzia wakuu katika kiti cha enzi cha ufalme hadi muombaji masikini kwenye mitaa, ni wathamani kwa Mungu. Thamani jinsi gani? Mungu angeacha mbingu; angeteseka na kufa kwa sababu ya *mmoja* wa familia yake ya mwanadamu—kama mtu huyo mmoja ndiye angekuwa na hitaji la upatanisho wa kuokoka.

> *Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu.*
>
> —*Yeremiah 31:3*

# 26

## Ufalme wa Mungu

> Ufalme wa Mungu hauji kwa kuchunguza kwa bidii, wala watu hawatasema, 'Huu hapa' au 'Ule kule,' kwa maana Ufalme wa Mungu umo ndani yenu.
>
> —Yesu (Luka 17:20–21)

Falme na taasisi za ulimwengu huu ni za kuonekana, na viti vya kuonekana vya serikali au makao makuu. Kama tunatafuta udhihirisho unaoonekana wa ufalme wa Mungu, hatutaupata. Ufalme wa Mungu ni dhahiri mioyoni mwetu tu kama upendo kwa Mungu na sisi kwa sisi unavyoondoa ubinafsi.

> Akawaambia tena, Tuufananishe Ufalme wa Mungu na nini? Au tutumie mfano gani ili kuueleza? (Marko 4:30)

Ni vigumu jinsi gani kupata maneno katika lugha ya mwanadamu ambayo yanaweza elezea kwa usahihi taswira ya ufalme wa Mungu kwa wale ambao wanaujua ufalme wa ulimwengu huu tu!

> Yesu akamjibu, Amin, amin nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili. (Yohana 3:3)

Ni kazi ya roho kufanya mambo ya kiroho yafahamike. Tunapokaribisha athari ya upole ya Roho Mtakatifu, ukweli wa kiroho huja kwenye nuru na kutuwezesha *kuona* au kufahamu ufalme wa Mungu. Badiliko katika mtazamo wa ukweli huu mpya ni wa kupatanisha na kutoa uzima, kama "kuzaliwa tena."

Roho Mtakatifu sio mpungufu ili kutenda kazi katika mipaka ya maeneo, kama tunavyowaza wakati mwingine. Anazungumza kwa kila mtu bila kuzingatia usuli, eneo katika sayari, au itikadi inayodaiwa. Hata wasioamini kuwa kuna Mungu hawajakingwa kutoka kwa kazi ya Roho Mtakatifu moyoni. Mungu hana mapendeleo kama yetu ya kuona karibu na hakasirishwi wakati mtu hakiri imani ya uwepo wake.

Kiini cha vitu vya kiroho ambavyo Roho Mtakatifu hufanya vifahamike sio tu maarifa ya akili, bali badiliko la moyo. Kama mfano, mkanamungu au mbishi mwenye huruma na mkarimu huathiriwa zaidi na athari ya Roho Mtakatifu na anakuwa karibu zaidi na ufalme wa Mungu kuliko mdini mwenye utakatifu wa nafsi na moyo mgumu. Ni nini kina weza kuwa kigumu zaidi kwa Mungu—kubadilisha mawazo ya mtu kuhusu uwepo wake au kubadili moyo mgumu wenye inda?

> Watu walikuwa wakimletea Yesu watoto wadogo ili awaguse lakini wanafunzi Wake wakawakemea. Yesu alipoona yaliyokuwa yakitukia akachukizwa, akawaambia wanafunzi Wake, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa watu kama hawa. Amin, amin nawaambia, mtu ye yote asiyeukubali Ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo, hatauingia kamwe. (Marko 10:13–15)

Inapofikia katika kujifunza ukweli kumhusu Mungu na ufalme wake, sehemu ngumu sio kujifunza bali *kuondoa uliojifunza* ambako lazima kufanyike. Wengi wetu wamewekeza vikubwa katika kukuza sura yetu ya Mungu. Kama sura hiyo imeumbuka, inaweza kuwa vigumu hasa kuiacha iondoke. Kwa vile sura iliyoumbuka ya Mungu imeingia katika dini maarufu kwa muda mrefu, inasimama kama kikwazo kikubwa cha

kufahamu ukweli kumhusu Mungu na ufalme wake. Watoto wamekuwa na mfichuo kiasi kidogo wa sura hii iliyoumbuka, na hivyo kuwa rahisi kwao kukubali ukweli kumhusu Mungu wetu mpole.

> Wakati huo, wanafunzi wakamjia Yesu na kumwuliza "Je, nani aliye mkuu kuliko wote katika Ufalme wa Mbinguni? Yesu akamwita mtoto mdogo na kumsimamisha katikati yao. Naye akasema: "Amin, nawaambia, msipoongoka na kuwa kama watoto wadogo, kamwe hamtaingia katika Ufalme wa Mbinguni. Kwa hiyo mtu yeyote ajinyenyekezaye kama huyu mtoto, ndiye aliye mkuu kuliko wote katika Ufalme wa Mbinguni. (Matt. 18:1–4)

Ufalme wa Mbinguni ni kinyume cha falme za ulimwengu. Hakuna nafasi ya kiburi, kudanganywa, kushurutisha, au fahari ya cheo. Tunahitaji kuwa na imani kama ya mtoto kwa Baba yetu wa Mbinguni na kuwa tayari kufunzwa.

> Ufalme wa Mbinguni unafanana na hazina iliyofichwa shambani, ambayo mtu mmoja alipoiona akaificha tena. Kisha katika furaha yake, akaenda akauza vyote alivyokuwa navyo, akalinunua lile shamba. Tena, Ufalme wa Mbinguni unafanana na mfanyi biashara aliyekuwa akitafuta lulu safi. Alipoipata lulu moja ya thamani kubwa, alikwenda akauza vyote alivyokuwa navyo akainunua.
> (Matt. 13:44–46)

Tutakapofahamu ukweli kumhusu Mungu—kuwa hana mipaka, ana upendo kwa wengine na kuwa ni wa kuaminika kabisa, mwenye Rehema, na mkarimu—tutakuwa na ufahamu

wazi kwa wakati huo huo wa jinsi ufalme wake ulivyo. Tutaona picha yetu ya sura ya Mungu iliyoumbuka kama isiyo na thamani na kwa furaha tutaiuza na kununua sura ya kweli ya Mungu na ufalme wake.

> Mwalimu mmoja wa sheria akaja akawasikia wakijadiliana. Akiona kwamba Yesu amewajibu vema, naye akamwuliza, "Katika amri zote, ni ipi iliyo kuu?" Yesu akajibu, "Amri iliyo kuu ndiyo hii, 'Sikiza Ee Israeli, Bwana Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote.' 31Ya pili ndiyo hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi." Yule mwalimu wa sheria akamwambia Yesu, "Mwalimu, umejibu vema kwamba Mungu ni mmoja wala hakuna mwingine ila Yeye. Kumpenda Mungu kwa moyo wote na kwa akili zote na kwa nguvu zote na kumpenda jirani kama mtu anavyojipenda mwenyewe ni bora zaidi kuliko kutoa sadaka ya kuteketezwa na dhabihu." Yesu alipoona kwamba amejibu kwa busara, akamwambia, "Wewe hauko mbali na Ufalme wa Mungu." (Marko 12:28–34)

Yesu alimtia moyo mwalimu wa sharia, alikuwa akijibu: "Wewe hauko mbali na Ufalme wa Mungu." Mwalimu wa sheria alionyesha ufahamu wa kina wa uhalisia wa kiroho kuliko wengi. Alienda zaidi ya kusoma maandiko kwa juu na kushika ruwaza ya sheria ya upendo ambayo Yesu alidhihirisha.

Nchi itakayofanywa upya itakuwa jinsi gani kama sheria ya upendo ndio sheria tu ya nchi? Upendo wa Mungu kwa watu wengine utaonekana kwa wanadamu wote. Kila mtu atampenda na kuthamini kila mtu mwingine kama "bora kuliko nafsi yake."

(Phil. 2:3). Kutakuwa na hali ya furaha na usalama mkubwa zaidi ya vile tunaweza fikiria.

> *Lakini ni kama ilivyoandikwa: Lile jambo ambalo jicho halijapata kuona, sikio halijapata kusikia, wala halikuingia moyoni lile Mungu alilowaandalia wale wampendao.*
>
> *—1 Wakorintho 2:9*

# 27

## Mungu Hutupa Uhuru wa Kweli

> Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.
>
> —Mwanzo 1:26

Utawala juu ya nchi ambao Mungu aliwapa wanadamu haukuweka unyanyasaji au ukandamizaji. Adamu na Hawa na kizazi chao wengekuwa walinzi wenye upendo kwa nchi na kila kiumbe ndani yake. Maandiko yananakiri, “Mbingu ni mbingu za Bwana, Bali nchi amewapa wanadamu.” *(*Zab. 115:16). Wakati wazazi wetu wa kwanza waliamini uongo kuwa Mungu ni mbinafsi na mwenye vikwazo, walilemewa na “Kwa maana mtu ni mtumwa wa kitu cho chote kinachomtawala.” (2 Petro 2:19). Pahali ambapo Adamu na Hawa wakati mmoja walikuwa na uhuru wao na wana wao sasa walikuwa kwenye utumwa wa ibilisi. Kwa kipindi cha kutisha baada ya anguko, ilionekana kuwa mwanadamu hana pa kukimbilia ila kupotea kwa udhaifu wa uharibifu sawa usioepukika kama Shetani na malaika wengine walioasi.

Bado kuna habari njema; Mungu alitoa njia ya kuondoka kwenye utumwa wao na kizazi chao. Kukabiliana na dharura hii, Mungu alinena maneno haya kwa Shetani: “nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.” (Mwan. 3:15). Uadui huu ni nini?

Wakati Shetani na wafuasi wake waliasi dhidi ya Mungu mbinguni, walifanya hivyo kutoka kwa nafasi ya uhusiano wa muda mrefu na Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Walikuwa na

muda wa kutosha kujua Upendo wa Mungu na hawakuwa na sababu ya kushuku wema wake. Walipojitenga kutoka kwa Mungu kama walivyofanya, walijiweka katika hali ambayo hawawezi pokea Roho Mtakatifu. Kwa kiburi chao cha inda, walikuwa wamejipoteza katika giza na hatimaye usahaulifu wa kutoweza kutubu na kumgeukia muumba wao.

Adamu na Hawa walipotenda dhambi, walifanya hivyo kutoka kwa mahali padogo pa maarifa ya Mungu na pa dogo pa kuzoeana naye. Walidanganywa na Shetani; *hawakuwa* wamepiga hesabu ya uamuzi wao wa kumkataa muumbaji wao. Ukengeufu wa mwanadamu kutoka kwa Mungu haukuwa bila tiba. Ahadi ya Mungu kuwa "ataweka uadui" Kati ya Shetani na mwanamke ilikuwa ujumbe asili wa injili ya dunia.

Rehema ya Mungu ilitoa tumaini kwa Adamu na Hawa na kizazi chao kuwa mioyo na mawazo yao yangeweza kumpokea Roho Mtakatifu—bado wangekuwa wazi kwa upendo wa Mungu. Utumwa wa mwanadamu kwa Shetani haungekuwa katika ujumla. Mapenzi huru ya kila mmoja yangesalia na kupunguza athari ya Shetani juu yetu na kuhakikisha uhuru wetu wakuchagua kupatanishwa na Muumbaji wetu.

> Ili kwamba viumbe vyote vipate kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa kuharibika na kupewa uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu. (Rom. 8:21)

> Kristo alitupa uhuru, akataka tubaki huru. Hivyo simameni imara wala msikubali tena kulemewa na kongwa la utumwa. (Gal. 5:1)

> Hivyo Mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli. (Yohana 8:36)

> Kwa habari yao, mungu wa dunia hii amepofusha akili za wasioamini, ili wasione nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye sura ya Mungu. Kwa kuwa Mungu, Yeye aliyesema, "Nuru na ing'ae gizani," ameifanya nuru Yake ing'ae mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo.
> (2 Kor. 4:4, 6)

Sio wakati wa kutupilia mbali upofu wa kufuata sheria na upayukaji ambao Shetani amepofusha injili ya Kristo nao na tuchague kutokuwa wahusika katika utouelewa uliopo wa Mungu wetu mpole?

> *Kama mkidumu katika maneno Yangu, mtakuwa wanafunzi wangu kweli kweli. Ndipo mtaijua kweli nayo kweli itawaweka huru.*
>
> *—Yesu (Yohana 8:31–32)*

Ukweli ni habari njema kumhusu Mungu wetu mpole!

Bwana asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana.

—Yeremia 9:23–24

# Vidokezo

1. Kwa usahihi fahamu, Bibilia ni yenye mantiki. Bibilia inajieleza na kujitafsiri yenyewe. (Isa. 1:18; 1 Kor. 2:13)
2. Njia zetu na mawazo yetu hazionyeshi njia na mawazo ya Mungu. (Isa. 55:8–9; Zab. 50:21)
3. Utukufu wa Mungu ni tabia yake. (Kut. 34:6–7; 2 Kor. 4:4, 6)
4. Mungu ni upendo. (1 Yohana 4:8, 16)
5. Upendo wa Mungu hauna ubinafsi kabisa. (Yohana 3:16–17; Rom. 5:8)
6. Upendo huhitaji uhuru. (Kumb. 30:19–20; Yohana 8:32, 36)
7. Yesu ni Mungu. (Yohana 1:1-3, 14; Kol. 1:13–17)
8. Yesu ni ufunuo dhahiri kabisa wa Mungu. (Ebr. 1:3)
9. Mungu habadiliki. (Mal. 3:6; Ebr. 13:8; Yakobo 1:17)
10. Mungu ni muumbaji na mpaji—sio mwangamizi. (Mwan. 1:1; Zab. 33:6, 9; Ebr. 1:3; Luka 9:56; Yohana 10:10)
11. Swali katika mgogoro ni msingi wa utawala wa Mungu— sio uwezo wake. (Mwan. 3:1–5)
12. Ufalme wa Mungu unatawaliwa na sheria ya upendo— sio kanuni ya sheria. (Matt. 22:37–40; Gal. 5:14, 22–23; 1 Kor. 13)
13. Mungu hatumii nguvu. Hushinda maovu kwa mema. (Matt. 5:43–48; Rom. 12:20–21; Luka 23:34)
14. Shetani ni adui wa Mungu na bwana wa udanganyifu. (Yohana 8:44; 2 Kor. 11:14; Ufu. 12:7–9; 1 Pet. 5:8)
15. Dhambi ni kumuona Mungu kama mbinafsi na asiye wa kuaminika. Mwan. 3:1–5; Kol. 1:21)
16. Dhambi ni ya kufisha—sio Mungu. (Rom. 6:23; Yakobo 1:13–15)
17. Mungu hatuhukumu—tunajihukumu wenyewe. (Yohana 3:17–21; 5:22; 12:44–48; Matt. 7:1–5; Luka 6:37; Rom. 2:1-3)

18. Injili ni habari njema kumhusu Mungu. (2 Kor. 4:3–6; Ufu. 14:6–7; Luka 15:11–32; Yohana 3:16–17; Rom. 5:8)
19. Ukombozi ni uponyaji wa upatanisho—sio suala la kisheria. (Marko 2:16–17; Luka 4:18–19; Matendo 28:27;2 Kor. 5:18)
20. Kumjua Mungu ni uzima wa milele. (Yohana 17:3)



***Matendo ya Mungu wetu mpole*** yanawasilisha ushahidi wa kutosha kuaminika kutoka kwenye Bibilia wa kumuondolea Mungu mashtaka kuwa yeye ni asiyejali, mwenye kuhukumu, mwenye kudhibiti, asiyehaki, mwenye hamaki, au katili. Kitabu kinadhihirisha kwamba Bibilia nzima, ikieleweka kwa usahihi, iko katika uiano na kifungu elezi: "Mungu ni Upendo" (1 Yohana 4:8)



Safari ya mwandishi mwenyewe kuelekea kwa safari ya sura halisi kabisa ya Mungu wetu mpole imechukua zaidi ya miaka 50. Jay anaishi na mke wake, Julie, katika kibanda chao cha "Mafundisho" yaliyovuviwa katika msitu wa boreali wa Minnesota kaskazini.